MID WEEK JACKPOT!
TZS. 575,472,890
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



RIPOTI MAALUM
**Usafiri** wa umma ulivyobeba hatari wenye ulemavu
UK. 4


# Nipashe

Jumanne Mei 9, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581305

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




KANE ATAKA TAJI LA EUROPA
UKURASA 22

# Kilimo chang'ara tena




• **Bashe** bungeni; bajeti pana, nyumba 4,000 za maofisa ugani, mazito matano kisekta yaja...

*Endelea ukurasa 2*












Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. **PICHA: MAKTABA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**MGOGORO WA TANGA, TWIGA CEMENT BADO NGOMA NZITO**

HATUA ya kampuni ya Saruji ya Twiga kununua hisa za Kampuni ya Saruji ya Tanga, bado ni kizungumkuti baada ya...

## Operesheni ya NEMC yasonga kelele kwenye nyumba ibada

UKURASA 3



## RC: Dampo pekee Dar limeelemewa

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAITUMIA MAMELODI KUINASA MARUMO UK.24

**KATUNI** UK.6

# Serikali kujenga nyumba 4,000 za maofisa ugani msimu 2023/2024

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amewasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, akija na mpango wa kujenga nyumba 4,000 kwa maofisa ugani kitaifa.

Katika hotuba yake, Bashe ameliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 970.7 kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vitano na mikakati 26 kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Pia, ametaja vipaumbele vingine ni: Kuongeza ajira na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na lishe, kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi, kuimarisha maendeleo ya ushirika pamoja na kuongeza tija na uzalishaji.

Bashe aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa wizara yake.

**TIJA NA UZALISHAJI**

Alisema mwaka 2023/24 wataongeza tija na uzalishaji kwa kufanya utafiti wa mbegu bora, uzalishaji wa mbegu na miche bora, usambazaji wa mbegu na miche ya ruzuku pamoja na uwekezaji kwenye huduma za ugani.

"Tutaongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 44,344 mwaka 2022/2023 hadi tani 127,650 mwaka 2023/2024".

Alisema pia watajenga nyumba za maofisa ugani katika kata 4,000, uwekezaji kwenye kupima afya ya udongo na utoaji wa ruzuku ya mbolea na viuatilifu.

Kadhalika, alisema watajenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji, kuanzisha vituo jumuishi vya kutoa huduma za zana za kilimo pamoja na kanda saba za kilimo za uzalishaji.

**AJIRA KWA VIJANA NA WANAWAKE**

Alisema watawezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja, kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo kupitia programu ya jenga kesho iliyo bora.

Pia, wataendeleza vituo mahiri vya kusambaza teknolojia na kuhamasisha uanzishaji wa kampuni za ugani za vijana.

**USALAMA WA CHAKULA**

Wizara itawekeza kwenye miundombinu ya uhifadhi kufikia uwezo wa kuhifadhi tani milioni tatu ifikapo mwaka 2030.

"Tutaongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 17.14 mwaka 2022 hadi tani milioni 18.7 mwaka 2023".

Vile vile, wataiongezea Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi hadi kufikia tani 500,000.

"Pia, tutaratibu Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika - 2023, pamoja na kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini," alisema Bashe.

**UPATIKANAJI MASOKO**

Mwaka 2023/24 watajenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa ajili ya wakulima katika halmashauri mbalimbali.

Pia, wataimarisha uongezaji thamani na uhifadhi pamoja na kuiwezesha sekta binafsi kwa kuijengea miundombinu ya masoko.

Alisema wataongeza mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi, kuimarisha upatikanaji wa mitaji, kuziwezesha maabara za serikali na sekta binafsi ziweze kufikia viwango vya ubora vinavyotakiwa kimataifa.

**KUENDELEZA USHIRIKA**

Waziri Bashe alisema watakwenda kuimarisha usimamizi na udhibiti wa vyama vya ushirika kuviwezesha kujiendesha kibiashara na kuvisaidia kupata mitaji.

Alisema wataimarisha na kupitia upya mifumo ya upatikanaji wa viongozi wa vyama vya ushirika, pamoja na kupitia upya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013.

*SOMA HOTUBA UK. 9-14



Wanajumuiya wa kanda ya Mwananyamala Dar es Salaam, wakiwa katika mkutano wao wa kila mwezi juzi, ambao Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), liliutumia kufanya kampeni inayodhaminiwa na Women Fund Tanzania (WFT) ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', kutoa elimu ya ulinzi na usalama wa watoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dampo kujaa Pugu kikwazo usafi Dar

**Na Christina Mwakangale**

KUTOONDOLEWA taka kwa wakati kwenye maeneo ya mtaani pamoja na kutegemea dampo la Pugu Kinyamwezi, ambalo pekee linategemewa na wakazi milioni 5.4 mkoani Dar es Salaam, ni kati ya vikwazo vinavyokwamisha mkoa huo kufikia viwango vya usafi na mji kupendeza.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Dar es Salaam imefikia wakazi 5,383,728 kutoka watu 4,364,541 mwaka 2012, huku uzalishaji wa taka ukiwa zaidi ya tani 4,600 na zinazofikishwa dampo ni kati ya asilimia 45 hadi 50 kwa siku.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akizungumza jana mkoani humo, baada ya kukutana na wadau wa mpango wa kampeni wa Safisha Dar es Salaam, pamoja na mafanikio ya kuwapanga wamachinga na kudhibiti biashara holela na usafi kila mwezi, bado kuna vikwazo.

"Jiji la Dar es Salaam limeendelea kufanya vizuri na kuwa miongoni mwa majiji bora 10 safi barani Afrika, suala la usafirishaji wa taka na kila halmashauri kuwa na dampo lake ni mikakati. Wote tunaendelea kutumia dampo moja la Pugu Kinyamwezi, ambalo wakati mwingine linashindwa kuhimili.

"Hii pia inasababisha gharama, tuliweka mikakati kwamba maeneo ambayo yapo pembezoni mwa jiji la Dar es Salaam, kila manispaa iwe na dampo lake. Usafirishaji kwenda dampo bado kikwazo, hamasa kwa wananchi ni kubwa, uzalishaji taka ni mkubwa taka zisiendelee kukaa mitaani," alisema Makalla.

Alisema lengo la mkutano huo na wadau ni kuangalia namna awamu ya pili ya kampeni hiyo itakavyodhibiti maeneo manne, ikiwamo udhibti wa biashara holela, kusafisha, usafirishaji na upendezaji kwa kupanda miti na bustani.

"Leo tupo hapa ili kila mmoja afahamu mikakati, mifumo isomane, TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania) wako hapa wajue na mshirikiane, sio manispaa inataka kufanya hiki TANROADS, TARURA (Wakala wa Barabara Vijijini) hawana taarifa, wajue majani yanafyekwa, barabara zinatunzwa," alisema Makalla. Pia, alisema kwamba Mamlaka ya Majisafi Dar es Salaam (DAWASA), watoe ushirikiano kwa sababu tayari wakuu wa wilaya wametenga maeneo ya kupendezesha mazingira hivyo na pia elimu iendelee kutolewa kwa jamii.

"Rwanda walianza kwa kuzomea, ukitupa taka unazomewa, huyooo huyooo...wakaona kumbe haitakiwi kutupwa taka, baadaye wakazoea. Zipo njia nyingi za kufanikisha usafi na mikakati ya kupendezesha Dar es Salaam," alisema Makalla.

## ...Kamati yataka somo kilimo kuanzia msingi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, imeishauri serikali kuanzisha somo la kilimo kuanzia ngazi ya msingi, liwe la lazima ili kuwajengea vijana uwezo wa kukifahamu.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, David Kihenzile, alisema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/23, maoni na ushauri kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo.

Kihenzile alisema sekta ya kilimo inachangia asilimia 26.1 ya Pato la Taifa, asilimia 65.5 ya ajira ya malighafi inayotumika katika sekta ya viwanda na mazao ya kilimo na kuchangia Dola za Marekani bilioni 1.2 ya mauzo nje ya nchi.

Alisema: "Kwa umuhimu huo kamati inaishauri serikali kuanzisha somo la kilimo kama somo la lazima kuanzia ngazi ya msingi, ili kuwajengea vijana wa kitanzania uwezo wa kukielewa na kushiriki kikamilifu katika sekta na kuongeza ajira."

Kuhusu uzalishaji wa mbegu, Kihenzile alisema kamati inaishauri serikali kuendelea kuziwezesha kifedha taasisi zinazohusika na uzalishaji wa mbegu pamoja na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, ili ziweze kuzalisha mbegu bora na kutosheleza mahitaji yaliyopo nchini.

Alisema nguvu zaidi za uzalishaji wa mazao mahsusi zielekezwe katika maeneo ambayo mazao hayo yanastawi kwa wingi ili kupata uzalishaji bora na wenye tija badala ya kuanzisha maeneo ambayo ni ya majaribio.

Kuhusu utafiti, Kihenzile alisema kamati inaishauri serikali kuendelea kuwekeza na kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo nchini ikiwa ni pamoja na kuwaongezea rasilimali watu na fedha.

Alisema kamati inaishauri serikali kuwajengea uwezo watafiti wa kilimo, ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kukuza sekta ya kilimo nchini.

Kihenzile alisema serikali inapaswa kuongeza kasi katika kufufua uzalishaji wa mbegu za asili kwa kufanyiwa utafiti, kuzalishwa kwa wingi ili kukidhi mahitaji na kuendelea kuboreshwa.

"Uzalishaji na utumiaji wa mbegu za asili utachangia katika kulinda utamaduni wetu, kuhakikisha uwapo wa usalama wa vyakula pamoja na kuinua kipato cha mkulima na uchumi wa taifa kwa ujumla," alisema Kihenzile.

Alisema pia serikali inapaswa kuhakikisha matokeo ya utafiti unaofanywa na taasisi za ndani yawafikie na kuwasaidia wakulima ili waweze kuzalisha kwa tija na kuongeza kipato.

Kuhusu mfumo wa ruzuku ya mbolea, Kihenzile alisema bado haujafahamika kwa wakulima wengi na hivyo kutoleta tija iliyokusudiwa.

"Kamati inaishauri serikali kuhakikisha kuwa elimu na taarifa ya uwapo wa mbolea ya ruzuku na namna ya kuipata inatolewa ili kudhibiti mianya ya inayotumiwa na watu wachache ya kuuza mbolea kwa bei ambayo ni nje ya bei ya ruzuku," alisema.

Pia alisema Wizara ya Kilimo inapaswa kupanua wigo na kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi bora na sahihi ya mbolea pamoja na viuatilifu.

Kihenzile alisema wizara ianze kuratibu na kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbolea na viuatilifu unazingatia muda sahihi wa kilimo ili kuongeza tija iliyokusudiwa.

## Samia ahudhuria mkutano wa ulinzi, usalama SADC

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, pamoja na viongozi wengine kutoka Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), wameshiriki mkutano unaohusu chombo maalum cha ulinzi na usalama kwenye ukanda huo.

Ni kikao kilichoongozwa na Rais Hage Geingob, wa Namibia mwenyeji na Mwenyekiti wa Siasa, Ulinzi na Usalama (TROIKA) wa SADC, kinachoundwa na viongozi kutoka nchi wanachama zinazounda Brigedi maalum ya Ulinzi na Usalama (FIB) inayojumuisha nchi zinazochangia vikosi (TCCs) kujadili mustakabali wao.

Kwa mujibu wa gazeti la Namibia Daily News, wajumbe wa kikao cha jana, walijumuishwa na Mwenyekiti aliyetamgulia, Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, na aliyetarajiwa kupewa kijiti cha kuongoza chombo hicho, Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema.

Kwa mujibu wa gazeti hilo, TROIKA ina wajibu wa kuimarisha amani na usalama miongoni mwa nchi wanachama wa SADC kwa kuzitaka serikali zao kuhakikisha wanalisimamia hilo kwa malengo hayo na kuwa mpango endelevu kwenye maeneo yao.

Viongozi wengine wanaotarajiwa kushiriki mkutano huo ni pamoja na Rais João Lourenço Angola na Rais wa Malawi, Lazarus Chakwera.

Vikosi vya FIB vipo nchini Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo (DRC), kwa kushrikiana na vile vya kutunza amani vya Umoja wa Mataifa (UN), huku mkutano ukiweka kipaumbele ajenda ya usalama kwenye ukanda huo, hasa eneo la Mashariki mwa DRC.



Mafundi wakichimba mtaro kwa ajili ya kuweka mabomba ya kusambazia maji kutoka Ziwa Victoria kwenda vijiji vya Bwasi, Bugunda na Kome, Musoma Vijijini mkoani Mara, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Operesheni NEMC yahamia kwenye nyumba za ibada

**Na Waandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limefungia nyumba za starehe na baa 89 nchini kutokana na kukiuka masharti ya leseni zao na kupiga kelele zilizovuka kiwango kisheria.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Samuel Gwamaka, alisema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni iliyofanyika kwa wiki moja kwenye mikoa mbalimbali nchini.

Alisema kwenye operesheni hiyo baa zilizofungwa Wilaya ya Kinondoni zilikuwa 19, Ilala (25), Kigamboni (22), Temeke (12), Dodoma (5) na Mwanza (6) na kwamba walianzia maeneo hayo kutokana na malalamiko mengi.

Alisema wenye kumbi za starehe na baa ambazo zimerudia kufanya makosa hayo watatozwa faini ya Shilingi milioni tano watakayopaswa kuilipa ndani ya siku 14.

Wakosaji wa mara ya kwanza watatakiwa kulipa faini ya Shilingi milioni mbili ndani ya siku 14 na wote watafunguliwa kuendelea na biashara zao iwapo watafuata masharti yaliyowekwa na Baraza.

"Sio kwamba NEMC inaona sifa kufunga biashara ya mtu, tunajua biashara hizo zimeajiri watu wengi sana na zinalipa kodi, lakini kelele nazo zimekuwa zikisababisha athari kubwa kwa wananchi kwa hiyo fanya biashara yako bila kuathiri maisha ya mtu mwingine," alifafanua.

Alisema kuna masharti wanayotakiwa kuyafuata kama wanataka kufunguliwa ambayo ni pamoja na kukiri makosa, kuahidi kufuata masharti ya leseni zao na kutorudia tena makosa hayo.

"Watuandikie barua waahidi kwamba hawatarudia na wakirudia tuwafutie leseni zao za biashara na wajenge miundombinu ya kudhibiti kelele ndani ya siku 30 na wapate ushauri kwa wahandisi wa sauti kuhusu kiwango kinachokubalika kisheria, wakifanya haya hata leo mimi mwenyewe nitawaandikia barua waendelee na biashara zao," alisisitiza.

Alisema, kwenye operesheni ya kuwasaka wachafuzi wa kelele lililofanyika kwa wiki moja wamebaini wafanyabiashara wengi wamekuwa wakifanya biashara kinyume na leseni zao jambo ambalo ni makosa.

Pia wamebaini kuwa matukio mengi ya kelele yanafanyika hasa wakati wa mwisho wa wiki, kutokana na watu wengi kupenda kupumzika baada ya kazi nyingi.

Alisema kuna maeneo ambayo waliwahi kuonywa, kufungiwa na kutozwa faini kutokana na kurudia makosa kama hayo, lakini hata kwenye operesheni ya wiki moja wamekutwa na makosa hayo hayo.

"Kuna baa ambazo ni sugu, yaani mnamfungia mnamtoza faini, lakini kesho mnakuta kafungua anaendelea na shughuli zake kama kawaida, mfano Element, Liquid, Havoc, Kitambaa Cheupe, Wavuvi Camp, Chako ni Chako, na wengine wengi tulishawaonya sana, lakini hawataki kufuata sheria," alisema.

Alisema operesheni hiyo ni endelevu na waliamua kuanza kwenye maeneo hayo kutokana na usugu wa wenye baa na kumbi za starehe na kwamba malalamiko yalikuwa ni mengi kutoka kwa wananchi.

"Baa na kumbi za starehe ziko kwenye makazi ya watu na hawapati usingizi, wanapata matatizo ya kisaikolojia kutokana na kelele za wenye baa na kumbi za starehe, kuna watu wanaumwa sasa mnapowapigia kelele mnawasababishia maumivu zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Gwamaka, hivi karibuni wataanza ukaguzi kwenye nyumba za ibada ambako alisema NEMC imekuwa ikipata malalamiko ya uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na kelele zilizovuka mipaka.

Kwa jijini Dodoma, juzi Ofisa Mkaguzi wa Mazingira wa NEMC, Saida Madusi, akizungumza na mwandishi wa gazeti hili alisema wamezifungia baa maarufu za Rainbow, Chako ni Chako, The Bistro zenye kelele na kuwa kero kwa wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira namba 20 ya mwaka 2004 na kanuni ya viwango vya udhibiti wa kelele na mitetemo ya Mwaka 2015.

"Katika ukaguzi wetu majira ya saa tisa usiku tumekuta ukiukwaji wa sheria. Sheria inasema maeneo ambayo yanazunguka maeneo ya watu na kuna biashara kelele zinatakiwa kuwa 60 DBA wakati wa mchana na 40 usiku," alisema.

Hata hivyo, alisema kwenye ukaguzi huo wamekuta kelele zimefikia 68 DBA na zilikuwa zinasikika hadi nje huku majirani wakilalamikia kelele hizo.

**WANANCHI WAFUNGUKA**

Lili Gumbo ni mmiliki wa baa ya Liquid iliyopo Kurasini alisema vipimo vya muziki vinafanyika kwa ndani badala ya nje na kupata matokeo ya sauti kubwa.

Alisema ni vizuri kuangalia upya vipimo vya upimaji kulingana na hali halisi ya sasa kuendana na mazingira.

"Hivi viwango vyao ni kwamba huwezi kuusikia muziki zaidi utasikia mazungumzo ya watu waliopo baa na watu wasiopikia muziki wanaondoka na baa inakosa wateja unatukuta tunadaiwa kodi na mahitaji mengine ni lazima yaende hata kama baa haina watu au wapo," alisema Gumbo.

Aidha, aliomba kuangalia viwango hivyo vya sauti huenda sheria hiyo inayotumika ni ya zamani.

Alisema baa yake haipo ndani ya makazi ya watu na kushangazwa kuona ikilalamikiwa kwa sauti kubwa.

"Mimi nimetajwa, lakini sina malalamiko na majirani. Majirani wote walishahama na hizi nyumba zipo kwa ajili ya biashara sina majirani ambao wanaweza kuja kulalamika NEMC wamenifungia kupiga muziki ila huduma nyingine naendelea nazo," alisema.

Vile vile, alisema masharti waliyopatiwa na NEMC ni magumu kuna uwezekano wa kufutiwa leseni ya biashara kutokana na maagizo waliyopatiwa.

Mmoja wa wananchi, Erick Saimon alisema ni jambo nzuri ambalo serikali imefanya kwa sababu kuna baadhi ya baa zimekuwa zikipiga muziki mkubwa na kusumbua nyumba za jirani.

Alisema kelele kubwa ni kero kwa wananchi na usumbufu kwa wanafunzi ambao wanataka kusoma usiku.

***Imeandikwa na Joseph Mwendapole, Beatrice Shayo (DAR) na Augusta Njoji (DODOMA)**

## RIPOTI MAALUM

# Usafiri wa umma ulivyobeba hatari kwa watu wenye ulemavu nchini

**Na Gwamaka Alipipi**




Magumu ya usafiri wa umma unaokuwa kikwazo kwa wenye ulemavu Dar es Salaam.

USAFIRI wa umma nchini si rafiki kwa watu wenye ulemavu. Miongozo na sheria za kimataifa, pia za nchini, zinaelekeza walindwe. Lakini mikono ya wanaopaswa kuzitekeleza inaonekana kukunjwa.

Mifumo mingi ya miundombinu ya usafirishaji nchini haikidhi mahitaji yao hata kuipa jamii hiyo ugumu wa mawasiliano.

Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2012 inaeleza kuwa, ulemavu ni hali inayotokana na dosari ya kimwili au ya kiakili ambayo inampunguzia mtu uwezo na fursa sawa katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali katika jamii.

Kwa mujibu wa sera hiyo, upungufu huo unaweza kuchochewa na mazingira na mtazamo wa jamii kuhusu ulemavu.

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 ilibainisha Tanzania ilikuwa na watu 44,928,923. Kati yao, wenye ualbino ni 16,477,000 (asilimia 0.04), wasiiona 848,530 (asilimia 1.19), viziwi 425,322 (asilimia 0.97), wenye ulemavu wa viungo 525,019 (asilimia 1.9), ulemavu wa kumbukumbu 401,931 (asilimia 0.9), ulemavu wa kushindwa kujihudumia 324,725 (asilimia 0.74) na ulemavu mwingine 99,798 (asilimia 0.23).

Ushuhuda wa mwandishi mkoani Dar es Salaam, umebaini ukiukwaji wa sheria za nchini na kimataifa kuhusu wenye ulemavu.

Kituoni Makumbusho wilayani Kinondoni, majira ya jioni, kwa takribani saa mbili anashuhudia Safia Jumbe, mwenye ulemavu wa viungo (miguu), anahangaika kupata usafiri wa kumpeleka kwao Mbezi wilayani Ubungo.

"Kila gari linalokuja linanipita. Linalosimama kondakta anasema sitoweza kupanda kwa sababu limejaa. Hakuna mahali pa kuweka baskeli yangu hii ndani ya daladala. Kwa ukweli sisi watu wenye ulemavu tunapata mateso kwenye usafiri wa umma," Safia anaeleza.

Safia, mama mwenye umri wa makamo, anaeleza zaidi "...hata nikishapanda gari, nyuso za abiria utaziona namna zilivyo... hawaniangalii usoni. Mwenye simu atakuwa 'bize' akichezea. Mwingine atajifanya amelala, mradi tu wasinipishe kwenye kiti.

"Daladala hazina viti maalum kwa ajili yetu sisi wenye ulemavu. Ni huruma ya abiria ndiyo inayokuwezesha kukaa, vinginevyo upande mwendokasi (Mabasi Yaendayo Haraka). Mabasi yao yana viti mahususi kwa ajili yetu. Hakuna usafiri mwingine zaidi ambao ni rafiki kwetu."

Katika eneo la Mbezi Luis, Nipashe inakutana na Sylvester Damian, mwenye ulemavu wa macho. Anasema ugumu unaomkabili katika usafiri wa umma ni baadhi ya makondakta kutotangaza vituo. Anashindwa kujua eneo alipo wakati wa safari.

Kuepuka asipitilize kituo cha kushuka, Damian anasema hulazimika kuuliza abiria mara kwa mara walio karibu naye ndani ya daladala.

"Ninatumia uzoefu na ninakariri sana. Iwe sauti, milio, kila kitu, ili kufika eneo fulani. Nikiwa kwenye daladala ninauliza abiria sehemu tuliyofika," anasema.

Mazingira hayo ya huduma za usafirishaji yanakinzana na Ibara ya 5 ya Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD) unaotambua kuwa kila mtu ana haki ya kuheshimiwa.

Pia yako kinyume cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya Mwaka 2010 ambayo katika Sehemu yake ya 6(b) inatamka "serikali itakataza aina zote ze ubaguzi zinazotokana na mtu kuwa ulemavu na itahakikishia watu wenye ulemavu haki sawa na mfumo mwafaka wa kisheria dhidi ya ubaguzi wa aina yoyote."

Katibu wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Jonas Lubagi, anasema daladala nyingi nchini hazitangazi vituo, hivyo kutokuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Pia anaeleza kuwa makondakta wengi hawawachukui watu wenye ulemavu vituoni kwa kuhofia kutokulipwa nauli.

"Watu wenye ulemavu wa miguu ambao wanatumia vitimwendo hawabebwi kwa sababu ya kuhofia kuchukua nafasi kubwa kwenye daladala," anafafanua.

Kulinusuru kundi hilo, Jonas anashauri huduma zote za umma, ukiwamo usafiri wa daladala, ziwe na miongozo. Serikali itanue huduma za umma sehemu zote. Kila eneo kuwe na huduma rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Daladala Dar es Salaam (UWADAR), Kismat Jafar, anakiri kuwapo manyanyaso kwa watu wenye ulemavu. Yanatendwa na baadhi ya makondakta. Chama kinakemea. Kinawapa elimu madereva na makondakta kuheshimu haki za watu wenye ulemavu.

Katibu wa Chama cha Waendesha Daladala Dar es Salaam (BASDA), Abdallah Mohamed, anakiri kupokea malalamiko yanayohusiana na vitendo vya unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu katika daladala. Vinafanywa na baadhi ya makondakta. Anawaita hawana utu.

Anasema BASDA inaheshimu sheria zilizowekwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Imekuwa inakemea tabia za ubaguzi na manyanyaso dhidi ya kundi hilo.

Mmoja wa makondakta wa daladala zinazofanya safari za kati ya Kariakoo na Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam, Kassim Mrija, amemwambia mwandishi kuwa: "...huwa ninawachukua watu wenye ulemavu nikiwakuta kituoni. Lakini miongoni mwetu, wapo wenzetu ambao wamekuwa wakiwabagua. Ninashauri serikali iweke utaratibu kama ilivyo kwenye mwendokasi."

Ally Kombo, dereva wa daladala (Buguruni - Mnazi Mmoja), anasema hakuna sheria wala mwongozo unaowalazimisha kuwa viti kwa ajili ya watu wenye ulemavu ndani ya mabasi yao. Kundi hilo kupata kiti ni huruma ya abiria wasio na ulemavu.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, anasema watu wenye ulemavu wanakabiliwa na ugumu kupata usafiri si tu kwa Jiji la Dar es Salaam, bali mikoa yote nchini.

Anasema sheria na Katiba ya nchi inatamka kuwapo na uwezeshaji rafiki wa miundombinu ya usafiri kwa watu wenye ulemavu.

"Ukiangalia kwa serikali imejenga Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka na wameweka miundombinu ya usafiri kwa watu wenye ulemavu. Lakini wamechelewa ilipaswa tangu miaka ya zamani iwapo.

"Sasa hivi wapo Dar es Salaam, vipi wanaoishi mikoani? Au vipi wanaoishi maeneo mengine ambayo mradi haujafika? Je, daladala zina hiyo huduma?" Anna anahoji.

Anasema njia pekee ya serikali kuwawezesha watu wenye ulemavu ni kuweka sheria itakayoruhusu kampuni binafsi ziwe na vyombo vya usafiri kama wa mabasi ya mwendokasi. Hapo itasaidia kupunguza hilo tatizo.

Mwandishi alipokwenda katika kituo cha Kimara Mwisho cha Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), alikuta kumetengwa eneo mahusui kwa ajili ya kuketi watu wenye ulemavu, wazee, wajawazito, wenye watoto wachanga na wagonjwa wanaposubiri mabasi. Ngazi ni rafiki kwa baiskeli za watu wenye ulemavu, maarufu vitimwendo.

Nipashe pia ilishuhudia kumewekwa utaratibu kundi hilo linaingiwa kwanza ndani ya basi kabla ya abiria wengine kuruhusiwa. Ndani ya basi mna viti mahusus kwa ajili ya watu wenye ulemavu, wazee, wajawazito, wenye watoto wachanga na wagonjwa.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dk. Edwin Mhede, anasema kwa sasa mradi huo unahudumia watu 180,000 kwa siku.

Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria ( CHAKUA), Hassan Mchanjama, anasema "...tumekuwa tukipigia kelele kwa miaka mingi kutetea haki za watu wenye ulemavu wawe na usafiri rafiki kwao.

"Serikali inapaswa kuruhusu watu binafsi kuagiza daladala au magari yenye miundombinu itakayokidhi haja ya watu wenye ulemavu. Magari hayo yaruhusiwe kwenda hadi katikati ya jiji."

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, anakiri kuwapo udhaifu katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu inayoelekeza haki na wajibu kwa watu wenye ulemavu.

"Tulitunga sheria lakini udhaifu upo katika usimamizi na utendaji. Ukiona kuna udhaifu katika mkoa, hawasimamii suala hilo, ujue kuna udhaifu katika usimamizi wa sheria hiyo," anaeleza.

Naibu Waziri huyo anasema hata katika miundombinu ya usafiri wa daladala kulipaswa kuwapo miundombinu rafiki itakayowawezesha kupanda na kushuka kwa urahisi kama ilivyo katika mradi wa mwendokasi.

Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, anasema wameshaanza kuchukua hatua kuhakikisha daladala zinakuwa na viti maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Anaeleza kuwa wameshaandika barua kwenda kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Wanataka lihakikishe daladala zote zitakazoagizwa na kuingizwa nchini ziwe na eneo maalum la kuketi watu wenye ulemavu.

DK. Athuman Ngenya, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, anakiri kupokea barua toka LATRA mwezi uliopita. Inashughulikiwa. Mwaka ujao wa fedha, suala hilo litakuwa limeshapatiwa ufumbuzi.

"Hili suala ni la kitaifa na kimataifa, hivyo lina utaratibu wake na linakwenda hatua kwa hatua. Lakini linashughulikiwa," anasema.

Meneja wa Walaka wa Barabara Tanzania (TANROADS), Haroun Senkuku, amemweleza mwandishi kuwa "...nimelichukua hili kama ushauri. Tutalifanyia kazi. Tuweke miundombinu rafiki kwa wenye ulemavu kwenye vituo vya daladala na ndani ya daladala."

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu Mwaka 2006 uliridhiwa na Tanzania Novemba 2009, nchi ikiahidi kuhakikisha kuna haki sawa kwa watu wenye ulemavu.

## HABARI KITAIFA

# Mgogoro Tanga, Twiga ngoma nzito

**Na Restuta James**

HATUA ya kampuni ya Saruji ya Twiga kununua hisa za Kampuni ya Saruji ya Tanga, bado ni kizungumkuti baada ya wadau kuendelea kudai kuwapo ukiukwaji mkubwa wa sheria katika mchakato wa muunganiko wa kampuni hizo.

Wadau hao wamesisitiza muunganiko mpya uliofanyika Februari mwaka huu ni batili kwa kuwa Baraza la Ushindani Kibiashara (FCT), katika uamuzi wake wa Septemba 23, 2022 lilitamka mchakato huo umekatwa, hivyo kuendelea kufanya jambo lililozuiwa kisheria ni kuvunja sheria na kudharau chombo kilichowekwa kisheria.

Pia wameainisha athari nyingi zinazoweza kujitokeza baadaye zikiwamo ukiritimba katika soko, kuwaminya washindani na hatimaye kufunga uzalishaji na kuwapo kwa uhaba wa bidhaa katika soko kutokana na mzalishaji kuamua anavyotaka.

Hali hiyo, kwa mujibu wa wadau hao, kama muungano huo utaendelea, kampuni ya Twiga Cement itamiliki soko kwa asilimia 47, kinyume cha sheria inayotaka mmiliki asizidi asilimia 35, ili kuruhusu ushindani kwenye soko.

Jijini Dar es Salaam jana, Wakili Mkuu wa Kampuni ya Mawakili ya MSL Attorneys, wanaowatetea wadau wa saruji nchini, Melchisedeck Lutema, aliwaambia waandishi wa habari kuwa ripoti ya uchunguzi wa kina wa soko, uliowasilishwa kwenye Baraza la Ushindani wa Biashara (FCT), ilieleza kwa kina athari za muunganiko huo, ikiwamo Twiga kuwa na ukiritimba sokoni.

"FCT katika uamuzi wake ilisema wazi kwamba muunganko wa Scancem International DA (inayomiliki Twiga Cement) na Twiga Cement umekatazwa. Sasa walichotakiwa kufanya ni kuomba FCC kufanya mapitio au marejeo badala ya kukaidi kama walivyofanya na kuendelea na mchakato.

"Lakini hata sababu ya iliyotolewa bungeni na Waziri wa (Uwekezaji), Viwanda na Biashara, (Dk. Ashatu Kijaji), wakati akifanya majumuisho ya makadirio ya wizara alisema kilichofanywa na FCC ni maombi ya pili kwa kuwa lile la kwanza lilishamalizika si kweli.

"Hapa ieleweke wazi kwamba hakuna kilichopingwa katika uamuzi wa FCC. Hakuna mtu anayeweza kuambiwa uvamizi aliofanya mara ya kwanza katika shamba ulishaisha, hivyo uvamizi wa pili ni halali wakati kisheria uliambiwa umekatazwa kuingia katika shamba," alisema.

Wakili Lutema alisisitiza kuwa kilichopaswa kufanywa kabla Tume ya Ushindani (FCC), kuruhusu muunganiko huo, ni kuomba mapitio ya hukumu ya FCT, ili ione kama inaweza kutengua uamuzi wake au vinginevyo.

Kutokana na ukiukwaji huo wa sheria, alisema tayari wadau, ikiwamo kampuni ya Chalinze pamoja na Chama cha Kutetea na Kusemea Watumiaji wa Bidhaa na Huduma Tanzania wameshakata rufani kuomba FCT, kukazia hukumu iliyotoa juu ya katazo la kuendelea kwa mchakato huo.

Alisema sheria zinazosimamia masuala ya miunganiko ya kampuni linazuia muungano utakaosababisha umiliki wa soko kwa zaidi ya asilimia 35.

Suala la kununuliwa kwa hisa na kufanya muunganiko wa kampuni kupitia Scancem International DA ambayo ni sehemu ya Heilderberg Cement inayomiliki Twiga Cement, lilipingwa FCT na wadau wa saruji ambao ni kampuni ya Saruji ya Chalinze, Chama cha Watumiaji wa Saruji na Peter Heller kwamba kunaweza kuleta athari katika soko la saruji.

"Katika uamuzi uliotolewa Desemba 22, 2022 na FCT chini ya Mwenyekiti Jaji Salma Maghimbi, iliamuliwa kwamba mchakato huo usitishwe lakini cha ajabu Februari 28, 2023 FCC waliendelea kwa kutoa hati ya muunganiko. Kwa nini FCC wasichukuliwe hatua za kisheria kwa kudharau na kukaidi amri halali ya chombo kilichowekwa kisheria?

"Kisheria, jambo lolote likitolewa uamuzi katika chombo chochote kilichowekwa kisheria, halipaswi kuendelea kufanyika. Na suala la muunganiko wa Twiga na Tanga Cement limezuiwa na hakuna mtu aliyepinga kwa kukata rufani, kuomba mapitio.

"Ni muhimu ikaeleweka kuwa uamuzi uwe sawa au si sawa na hakuna mtu aliyeupinga ni lazima uheshimiwe; Kwa hiyo mtu yeyote anayeendelea anakiuka sheria na anapaswa kuchukuliwa hatua. Kwa hili tumeiomba FCT kukazia hukumu ili uvunjaji huu wa sheria usiendelee," alisisitiza.

### MCHAKATO FEBRUARI

Wakili Lutema alisema baada ya FCT kuamuru kusimamishwa, Februari 11, 2023 FCC ilitangaza kurejewa uuzwaji wa Tanga Cement na kuwapo muunganiko jambo ambalo pia linakiuka sheria kwa sababu kuna amri ya kisheria inayokataza kuendelea kwa mchakato huo.

Licha ya kukiukwa kwa sheria, alisema baada ya kutangazwa, FCC iliwataka wanaopinga mchakato huo wapeleke mapingamizi yao Dodoma, lakini hayakusikilizwa. Katika hilo, alisema wadau hawakutendewa haki.

Kuhusu madai kwamba Chalinze Cement haina nguvu za kisheria kupinga mchakato huo kwa kuwa haijawahi kuzalisha hata mfuko wa saruji, Lutema alisema hayana mashiko kwa sababu inawezakana ilikuwa katika mchakato wa uzalishaji, hivyo inataka kuwe na mazingira rafiki katika biashara badala ya ukiritimba aliodai unaandaliwa hivi sasa.

Aidha, alisema kuhusu madai kwamba Chalinze imefutwa katika orodha ya kampuni kwenye daftari la Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA), hilo pia halina mashiko kwa sababu hakuiondolei sifa ya kuendelea kupinga.

### HOFU YA WAWEKEZAJI

Mwanasheria huyo nguli pia alisema kumekuwa na madai kwamba kutokana na upinzani unaoendelea dhidi ya mchakato wa kuuzwa kwa hisa za Tanga Cement unaweza kukimbiza wawekezaji ambayo hayana ukweli na yanajaribu kupotosha umma.

Alisema jambo lolote katika nchi yoyote linatakiwa kufanyika kwa kufuata sheria, kanuni, miongozo na taratibu. Kwa mantiki hiyo, alisema hata wawekezaji wanatakiwa kufuata sheria za nchi husika na si kuzisigina.

Lutema alisema suala la uuzwaji wa hisa na muunganiko wa kampuni kama unavyoendelea, umegubikwa na usiri mkubwa hali inayoibua maswali mengi kwa nini Twiga Cement pekee inunue Tanga Cement badala ya kualika wadau na kampuni zingine kujitolea na kuonyesha nia ya kununua hisa hizo.

"Nini kimejificha nyuma ya pazia kutaka Twiga Cement pekee ipewe kipaumbele wakati duniani kuna kampuni nyingi za kuzalisha saruji? Kama kweli tunataka kuwe na ushindani wa haki, litolewe tangazo kualika wadau mbalimbali ili washindane na Twiga badala ya upekee unaofanywa kwa Twiga," alisisitiza.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio mchakato Katiba mpya kimesikika

**HATIMAYE** kile kilio cha kuanza kwa mchakato wa Katiba mpya kimeanza kupata jibu baada ya mwishoni mwa wiki, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kumwagiza Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Mutungi, kuitisha kikao maalum cha Baraza la Vyama vya Siasa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Ikulu,

lengo ni kuwashirikisha wadau katika kutathmini utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi kilichokuwa kikiratibu maoni ya watu kuhusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

Imeelezwa kuwa Rais Samia ametoa maelekezo hayo wakati wa kikao kilichofanyika Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma, kilichohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali kuhusu kuanza kwa mchakato wa Katiba mpya.

Kikao hicho kimejadili namna ya kushirikisha wadau mbalimbali na hasa ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato huo kutoka pande zote mbili Tanzania Bara na Zanzibar.

Mbali na mchakato huo wa Katiba mpya, masuala mengine yanayotarajiwa kushughulikiwa ni marekebisho ya sheria mbalimbali zinazohusiana na uchaguzi; zikiwamo Sheria ya Tume ya Uchaguzi, Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria kikao hicho ni pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Jenista Mhagama, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro na watendaji wa taasisi mbalimbali.

Tunasema hatua hii iliyochukuliwa na Rais Samia, inarejesha matumaini ya kuanza mchakato huo ambao umekuwa kilio kikubwa cha Watanzania cha kutaka Katiba mpya.

Vyama vya siasa hasa vya upinzani ndiyo kimekuwa kilio chao katika mikutano yao ya kutaka Katiba iliyopo sasa ifanyiwe marekebisho ili iweze kutoa haki sawa kwa Watanzania wote na kuondoa sheria zinazoonekana kuwa na upungufu na kulalamikiwa na watu wengi.

Rais Samia anarejesha imani kwa Watanzania ya kuwapo na matumaini ya kupata Katiba mpya, ikizingatiwa kuwa wakati mchakato huo ulipoanzishwa na Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, mwaka 2014 yeye (Rais Samia) ndiye aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba, Mwenyekiti akiwa Samuel Sitta (marehemu).

Hata hivyo, mchakato huo hakuweza kufikiwa lengo lake, baada ya baadhi ya vyama vya upinzani kujitoa na kuanzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA).


Licha ya kujitoa, Mwenyekiti wa Umoja huo, Freeman Mbowe, alisema wataendelea kushiriki kwenye vikao, ingawa wataendelea kupigania mageuzi ya msingi uendeshaji wa Bunge hilo ambalo lilitakiwa kutoka na Katiba mpya itakayopigiwa kura ya maoni ndani ya kipindi kisichozidi miezi miwili katika kipindi hicho cha mchakato.

Jaji Joseph Warioba, ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Katiba. Bunge hilo la kwanza la aina yake ndani ya kipindi cha miaka 50 ya Muungano wa Tanzania.

Mchakato wa kupata Katiba mpya ulikwama baada ya kikao cha Bunge Maalum la Katiba, kuahirishwa mara kadhaa na dalili zikionesha kuwapo hali ngumu na uwezekano wa kufikia muafaka kwa hatima ya Taifa la Tanzania.

Hatua ya Rais Samia sasa imefungua nuru mpya, Mungu ibariki Tanzania iweze kusonga mbele.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Utoro huu 'form one' upate dawa ya kudumu

**MIAKA** ya hivi karibuni, umeibuka mtindo wa baadhi ya wanafunzi wanaochagulia kuanza kidato cha kwanza kutoripoti katika shule walizopangiwa, huku kukiwa hakuna taarifa zozote za kutoripoti.

Mtindo huo umekuwa ukisababisha serikali za wilaya na mikoa katika maeneo yenye utoro kuanzisha msako wa dhidi yao, ili wapatikane waende shule kuendelea na masomo.

Inawezekana wapo wale ambao wazazi wao huwahamishia katika shule nyingine badala ya zile walizochaguliwa, lakini ninadhani si wengi kwani unaweza kukuta shule moja wanafunzi zaidi ya 200 hawajaripoti.

Ikumbukwe serikali imeongeza nafasi ya elimu ya sekondari, ili kusaidia watoto wa Kitanzania kupata elimu hiyo, lakini ajabu ni hao wanaochaguliwa lakini wanaingia 'mitini'.

Ili kukabiliana na hali hii ipo haja kwa serikali kufuatilia zaidi ili kupata kiini cha utoro huo na kukipatia ufumbuzi wa kudumu na kuachana na msako wa kila mwaka dhidi ya wazazi na wanafunzi wenyewe.

Wakati mwingine inawezekana miongoni mwa wanaofaulu ni wale wasio na mwamko wa elimu au ugumu wa maisha, wazazi wako tayari kuwaozesha binti zao ama kuruhusu wakafanye kazi za ndani ili wapate chochote cha kulisha familia.

Lakini inawezekana wengine wanalazimishwa na wazazi kubaki wakifanya shughuli za nyumbani, kutokana na kwamba hawana mwamko wa elimu hivyo wanaona elimu ya msingi inatosha.

Aidha, wakati mwingine mazingira ya sekondari za kata yanaweza kuwa chanzo kutokana na kwamba baadhi si rafiki kwa wanafunzi, kwa kukosa mabweni, umbali na pia ubovu wa miundombinu ya shule zenyewe.

Hilo halina ubishi, kwani unakuta mwanafunzi anatembea umbali wa kilomita 10 kwenda shule na kurudi nyumbani, halafu shuleni hakuna walimu wa kutosha, wala vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

> **Ni kupitia elimu watu wanafahamu masuala ya afya, kilimo, chakula bora, usafi wao na mazingira.**

Hata hivyo, pamoja na yote hayo, sidhani kwamba yanaweza kuwa kigezo cha mwanafunzi kuacha kwenda shule, kwani wapo waliosoma katika mazingira hayo na wakafanya vizuri.

Ingekuwa vyema kama wazazi na walezi watawakazania watoto wao kwenda shule wakati taratibu nyingine za kuboresha mazingira ya shule zikiendelea, badala ya kuruhusu wawe watoro.

Lakini shule za umma ni mali ya wazazi na walezi, hivyo hawana budi kuzihudumia ili ziwe katika mazingira bora kwa manufaa ya watoto wao badala ya kujiweka pembeni na kudhani hawahusiki.

Sidhani kama ni sahihi wanafunzi kuziona sekondari za kata kana kwamba haziwafai, kwani zimekuwa ni mkombozi wa watoto wa maskini na ninaamini wapo waliofika mbali kupitia shule hizo.

Hivyo, wazazi na walezi wa wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kisha wanakaa nyumbani, ni vyema wakatambua kuwa pamoja na changamoto katika shule hizo, elimu bado ni ya muhimu.

Kwa maana hiyo, wakati serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya shule zake ili iwe rafiki kwa wanafunzi, ni muhimu wanafunzi nao kutokubali kuwa watoro kwa kisingizio kisicho na msingi.

Ingekuwa vyema kama wanafunzi wataacha kudharau elimu kwa visingizio kuwa haiwasaidii, bali watambue kuwa mataifa yaliyoendelea, wananchi wake wamesoma lakini wafahamu kuwa elimu ni ufunguo wa maisha ya kila mmoja.

Ni kupitia elimu watu wanafahamu masuala ya afya, kilimo, chakula bora, usafi wao na mazingira.

Aidha, ni kupitia elimu hiyo kuna wasomi na wataalamu wa kada zote kuanzia wahandisi, wabunge, matabibu, walimu, wanahabari, wachumi, wakulima, wanasayansi na wafugaji pamoja na wataalamu wengine wote si wa Tanzania hata duniani kote.

# Serikali kuwapa kifuta jasho waliovamia Shamba la Utegi

**Na Munir Shemweta,** RORYA

SERIKALI itatoa fidia ya kifuta jasho kwa wananchi watakaobainika kuvamia eneo la Shamba la Utegi lililopo wilayani Rorya mkoani Mara baada ya kufanyiwa utambuzi.

Eneo lililovamiwa lina ukubwa wa hekta 476.52 limezingirwa na vitongoji vya Kibinyongo, Mabatini, Oringa, Denga na Omuga. Pia kuna Shule ya Msingi Utegi iliyoko karibu na ofisi za utawala za shamba.

Uongozi wa Wilaya ya Rorya pia umesitisha mipango ya kuboresha miundombinu ya Shule ya Msingi Utegi licha ya kupewa kiasi kikubwa cha fedha. Unasubiri mchakato wa kuhamisha shule hiyo kupisha shughuli za shamba.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula alibainisha hayo juzi alipotoa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu mgogoro wa matumizi ya ardhi baina ya wananchi na Shamba la Utegi katika Halmashauri ya Rorya.

Pamoja na kutambua uvamizi uliofanyika ndani ya shamba hilo, Dk. Mabula aliwaeleza wananchi kuwa serikali imedhamiria kulipa kifuta jasho kwa kulipa fidia ya maendeleo ya wananchi watakaobainika kuvamia shamba hilo.

Alisema uthamini wa maendeleo ya wananchi utafanywa kwa njia shirikishi. Utahusisha wathamini kutoka Mkoa wa Mara na wizarani.

"Timu ya wataalamu imeandaa mpango kazi na bajeti ya kuendesha uthamini na serikali itahakikisha kazi hii inatekelezwa kwa uwazi mkubwa na inakuwa shirikishi kwa wananchi wa ngazi zote," alisema.

Waziri huyo pia alisema serikali itazingatia maslahi ya wananchi ikiwamo kuhakikisha ulinzi na usalama wakati wote wa uthamini.

Kwa mujibu wa waziri huyo, utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu migogoro ya matumizi ya ardhi utaimarisha usimamizi wa maeneo mbalimbali ya serikali, ukuaji wa uchumi na usalama wa wananchi na mali zao.

Shamba la Utegi ni eneo lililotumika kwa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa lengo la kupata malighafi ya maziwa ya kiwanda na kuzalisha mitamba bora kwa ajili ya wananchi wa maeneo yanayozunguka shamba.

Eneo hilo lilitwaliwa kutoka sehemu ya vijiji sita vya Utegi, Mika, Omuga, Nyasoro, Nyanduga na Igri ambavyo vinaunda umoja wa vijiji ujulikanao kwa jina la UMONI mwaka 1969. Lililimwa kama shamba la mifugo Utegi Na. 168 mwaka 1974 likiwa na ukubwa wa hekta 5,048.02.

# Lissu ataka Katiba mpya kabla ya 2025

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema hawatokubali kuingia katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kama nchi itakuwa haijapata Katiba mpya.

Msimamo wa kiongozi huyu ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, umekuja siku moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kumwagiza Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kuitisha kikao maalum cha Baraza la Vyama vya Siasa, ili kuwashirikisha wadau kufanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi kilichoratibu maoni ya watu kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini.

Lissu aliyasema hayo juzi alipozungumza na wakazi wa Mkoa wa Morogoro kwenye uwanja wa Shule ya Msingi K, ndege, akiwataka kushirikiana na CHADEMA kudai Katiba mpya kwa kuwa ni haki ya msingi.

Alisema Katiba mpya itasaidia kupata viongozi thabiti watakaochaguliwa kupitia uchaguzi sahihi na wakiikosa ni wazi watakwenda kwenye uchaguzi mkuu mgumu kama uliopitishwa mwaka 2020 kwa wagombea kukatwa na kupitishwa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) pekee.

Lissu alisema Katiba mpya ndio itakayoonyesha kama kuna suala la upatanisho, lakini kwa sasa hakuna upatanisho wala maridhiano kama wanavyosema kupitia mabango kwenye barabara mbalimbali. Alisema hakuna kinachotekelezwa kikiwa cha haki.

Alisema ni mwaka mmoja umepita sasa tangu wapeleke mapendelezo yao ya kutaka Katiba mpya ambayo yamebeba mambo mbalimbali muhimu, lakini hawajajibiwa hata moja huku wakiambiwa kuendelea kutulia "wakati wananchi wanaendelea kunyanyaswa pamoja na kuporwa ardhi yao katika maeneo mbalimbali ya nchi".

Kiongozi huyo aliwataka wananchi kudai Katiba mpya yenye mfumo mpya wa uchaguzi na haki zao kwa ujumla.

Aliyekuwa mgombe Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini kwa tiketi ya CHADEMA, Devotha Minja,

aliwaomba wananchi kushirikiana naye kwenda mahakama kuu kufungua kesi ya kudai viwanda kwa madai kuwa viwanda vimejengwa kwa jasho la wananchi ambao ndio walipakodi na kufungwa kwake kunahatarisha maisha ya wananchi ambao walivitegemea kwa ajili ya kujikimu.

"Miaka ya 1990, Morogoro ilikuwa ni vifijo kwa kufanya kazi kwenye viwanda, kulikuwa na viwanda vya kutosha. Ilikuwa huwezi kupata dada wala kaka wa kazi, lakini kwa sasa vijana wanapishana tu vijiweni, twende tukadai viwanda vyetu," alisema Minja.

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mlimba, Susan Kiwanga, aliwataka wananchi, hasa wanawake, kubadilika na kuipigia kura CHADEMA kwenye uchaguzi mkuu ujao, ili waepukane na alichokiita adha ya kulipia gharama za matibabu wakati wa kujifungua kwa kawaida au kwa upasuaji.

"Tangu mwaka 1960, CCM inasema huduma za mama na mtoto ni bure, lakini mpaka sasa hakuna ukweli huo. Watu wanalipishwa kila huduma wanayopewa sambamba na wanaofanyiwa upasuaji kulipishwa Sh. 300,000. Hiyo sahihi?" alihoji Kiwanga.

Mch. Peter Msingwa, aliyekuwa Mbunge wa Iringa Mjini, alitoa wito kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuwa makini wanaposhughulikia kodi kwa kuwa wanatakiwa kujua nchi zenye viwanda na zinazoingiza bidhaa hazipaswi kulipa kodi sawa, lakini kwa Tanzania wafanyabiashara wanaumia kutokana na kodi kubwa inayotozwa kwenye bidhaa.




MAKALA

# Mzimu wa kufeli mitihani unavyoing'ang'ania 'Law School'

## •Mwaka huu wametisha zaidi, mawakili 301 chali 'wamedisco'



Kada ya wanasheria, mawakili na majaji wanaosimamia sheria na haki mahakamani. **PICHA: MTANDAO**

**NA JORAN HERMAN**

MATOKEO ya mitihani ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria The Law School of Tanzania (TLS) yameendelea kuibua mitizamo tofauti kutokana na kufeli kila wakati.

Ijapokuwa Wizara ya Sheria na Katiba iliunda Tume kufuatilia tatizo hilo, anguko kubwa la wanachuo shuleni hapo mwaka huu, linameendelea licha ya tume kubaini chanzo cha kufeli na kutoa mapendekezo.

Itakumbukwa kuwa wiki kadhaa zilizopita TLS au Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo, ilitoa matokeo ya wanachuo walianza masomo Januari 2022 na kuhitimu Desemba mwaka jana.

Ufaulu wao, umepungua zaidi ikilinganisha na matokeo yaliyopita, safari hii waliofaulu 23 pekee, wanaorudia mitihani ni 497 na waliofeli na kufukuzwa au 'discontinued' ni 301.

Mwaka jana waliofaulu walikuwa 26, waliorudia walikuwa 484 na waliofeli 265.

Ufaulu, unazidi kupungua na wanaofeli wanazidi kuongezeka, hivyo wadau wa elimu na wanafunzi baada ya matokeo hayo wanaendelea kujiuliza na kuhoji chanzo cha kufeli na wanasahau kuwa serikali iliunda tume ya kuchunguza kufeli kwa wanafunzi.

Ikiongozwa na Mwenyekiti Dk. Harrison Mwakyembe, tume hiyo iliyoundwa mwaka jana baada ya matokeo mabovu ili kubaini chanzo kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa ili kuondoa hali hiyo.

ILICHOPENDEKEZA TUME

Ikiangalia vyanzo vya kufeli, Tume ya Mwakyembe, ilisema ni uwezo mdogo wa wanafunzi ikiwamo kujua Kiingereza na vyuo walivyotoka kutowaandaa au kutowafundisha kikamilifu. Sina uhakika kama mapendekezo yaliyotolewa na tume yameshaanza kufanyiwa kazi au kutekelezwa.

Ingawa Tume ya Mwakyembe ilibaini vyanzo vya wanafunzi kufeli lakini kuna wanaokubaliana na ripoti hiyo na wasiokubaliana nayo. Hao wanaibua mitazamo na maoni tofauti baada ya matokeo haya kutoka wiki iliyopita. Kuna kundi linalosema na kuamini kuwa Law School inafelisha makusudi kwa sababu zipo ajenda za siri za kutoruhusu mawakili wawe wengi mitaani.

Aidha, wanadai kwamba wameshapanga mipango ya kuweka idadi ya mawakili kila mwaka. Hili ni kundi la kwanza linaloamini hivyo na serikali kiujumla wameshapanga idadi ya wanafunzi wanaopaswa kuapishwa na kuwa mawakili kila mwaka na idadi hiyo ni ndogo ndiyo maana wanaofaulu ni kiduchu.

Kundi lingine limeendelea kusema kuwa walimu wa Law School hawana sifa na hawastahili kuwa wahadhiri. Wanamaanisha kuwa kama mwanafunzi anafeli basi mwalimu naye kafeli, kwa imani kuwa hawawezi kufeli kama mwalimu wake ni mahiri.

Wanakundi wanaamini kwamba mwalimu bora ni yule anayetumia kila njia kumwelewesha mwanafunzi na kutafuta mbinu za kufanikisha mwanafunzi huyo kufaulu. Wapo wanaosema kuwa baadhi ya walimu wa Law School wana hila na chuki binafsi, kwamba wanatunga mitihani migumu ili kuwakomoa wanafunzi na wanaofeli.

Wanaamini kuwa baadhi ya walimu hufurahi pale wanapoona wanafunzi wengi wamefeli na linaendelea kusema kuwa walimu hao hutunga mitihani vigongo tena wanajua kuwa wanafunzi hawataiweza, ili mradi tu wafeli.

Lipo kundi lingine linaloamini ripoti na maoni ya Tume ya Mwakyembe kuwa TLS haina tatizo lolote ila shida ni wanafunzi wenyewe na vyuo walivyotoka. Wadau wake wanaamini kuwa ili uwe wakili lazima uive kisheria na kazi ya Law School ni kuwaandaa mawakili wenye ustadi na weledi wa hali ya juu na kuhakikisha inatoa mawakili waliofaulu na wenye sifa.

Kwa hiyo TLS inatimiza wajibu wake kikamilifu isipokuwa inaletewa watu ambao hawajaivishwa kwenye vyuo walivyotoka. Nichukue fursa hii kwa mujibu wa katiba kutoa maoni binafsi kama Mtanzania na mdau wa elimu kuwa shule ya sheria ni taasisi bora, inafundisha vizuri, wanaeleleza vizuri na wanawaandaa kikamilifu kwenda kuutumikia umma kwa weledi na maadili.

Shule hiyo wanakufundisha kwa nadharia na kwa vitendo. Baada ya kukupika kikamilifu kuhakikisha umefanya vitendo na mazoezi, ndipo wanapokupima kupitia mitihani ambayo ni ya kiutendaji na kimbinu siyo ya lelemama.

Mitihani ipo ' too technical' siyo ya kukimbilia kujibu, usipokuwa makini ni rahisi kwenda chaka au mchomo na usijue pa kutokea. Kujibu mitihani ya TLS kunahitaji utulivu wa hali ya juu wa akili na mwili, nikimaanisha kuwa unaweza kuwa umesoma vizuri na kukesha kila siku maktaba lakini ukafeli kwa sababu mitihani hiyo inahitaji umakini na utulivu ili kuelewa swali na kulijibu vizuri kwa mujibu wa maelekezo ya kimtihani.

Tuelewane kuwa kusoma ni jambo moja na kujibu mtihani na kufaulu mtihani jingine. Unaweza kuwa umesoma sana lakini bado ukafeli mtihani. Sina ubishi kwenye usomaji wa wanafunzi wa TLS. Wengi wao wanasoma tena sana lakini linapokuja suala la kujibu mtihani wanafeli, kwa uzoefu wangu licha ya kusoma kwa bidii shule ya sheria inahitaji utulivu na umakini wakati wa kujibu mitihani kwa sababu siyo rahisi kujibu ni ya kiutendaji zaidi na kimbinu.

Tofauti na kusoma kwa bidii, mwanafunzi ili afaulu anapaswa kuondoa hofu ya kufeli, kujiamini, kuwa mtulivu wa hali ya juu utakaoleta umakini na hatimaye kuelewa maswali na kuyajibu kwa ufasaha.

**Mwandishi ni wakili, aliyefuzu The Law School of Tanzania.**



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Wizara ya Kilimo**

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, HUSSEIN MOHAMMED BASHE (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2023/2024



Mhe. Hussein Mohammed Bashe (Mb)
**Waziri wa Kilimo**



Mhe. Anthony Peter Mavunde (Mb)
**Naibu Waziri wa Kilimo**



Gerald Geofrey Mweli
**Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo**



Dkt Hussein Mohamed Omar
**Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo**

#BAJETIKILIMO2024

AJENDA 10/30 KILIMO NI BIASHARA | www.kilimo.go.tz | YouTube kilimo Tv | Wizara_ya_kilimo | tzagriculture | bbt



# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, HUSSEIN MOHAMMED BASHE (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2023/2024

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wazima wa afya na kwa kuendelea kuijalia nchi yetu amani na mshikamano na kujadili bajeti hii inayolenga kusukuma mbele kasi ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo na wakulima kwa ujumla wao.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kusimamia shughuli za kilimo nchini. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa weledi, uaminifu na ubunifu mkubwa ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa na uhakika wa chakula, kulisha wengine kibiashara lakini pia wakulima wanapata kipato cha kutosha ili kupunguza umaskini.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuanza utekelezaji wa mageuzi kwenye sekta ya kilimo kwa kuwekeza katika miradi ya muda mrefu na maeneo ya msingi ya kutatua changamoto za kilimo kuanzia shambani hadi sokoni na kuitekeleza dhana na falsafa ya msingi kabisa kwenye kilimo kuwa ''kilimo ni uwekezaji wa muda mrefu''. Ni dhahiri kuwa chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita kumekuwepo msukumo wa kipekee katika kuendeleza sekta ya kilimo.

5. Watanzania wanashuhudia sasa kasi kubwa ya uwekezaji mkubwa wa Serikali kwenye rasilimali fedha na watu pamoja na uhamasishaji wa sekta binafsi kuwekeza na kukifanya kilimo kuanza kutoa ajira zenye staha kwa vijana na wanawake, ikiwa ni pamoja na hatua ya kuongeza kwa kiasi kikubwa bajeti ya Wizara ya Kilimo kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023 na kujenga msingi imara wa utekelezaji wa mipango ya kilimo yenye kutazama Tanzania ifikapo mwaka 2050. Ninamuahidi tena Mheshimiwa Rais, Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kuwa, Wizara itaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha sekta ya kilimo inafikia ukuaji wa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 na kujenga msingi imara wa kulinda uchumi wetu kuelekea mwaka 2050.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipekee, ninapenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ushiriki wake na kuwa mstari wa mbele katika duru za majadiliano ya masuala ya kilimo kimataifa na kuifanya nchi yetu kushinda kuwa mwenyeji wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (Africa Food Systems Forum) litakalofanyika tarehe 5 hadi 8 Septemba, 2023 Jijini Dar es Salaam na kuzifanya taasisi za kimataifa na wadau wa maendeleo kama vile Benki ya Dunia, AFDB, USAID, IFAD, FAO, AGRA na wadau wengine kuanza uwekezaji na Tanzania kurudishwa kwenye Mpango wa Feed the Future. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania kuwa mwenyeji wa Jukwaa hili, ni fursa kubwa kwa nchi yetu kuvutia uwekezaji katika nyanja mbalimbali ikiwemo sekta ya kilimo na biashara. Nitoe wito kwa wadau wote wa sekta ya kilimo hususan sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika jukwaa hilo ambalo litaleta pamoja zaidi ya washiriki 3,000 kutoka nchi mbalimbali duniani.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa akisisitiza na kutoa maelekezo kuhusu umuhimu wa kilimo endelevu na kinachozingatia hifadhi ya mazingira na kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na kuwa muumini mkubwa wa masuala ya utafiti na yeye mwenyewe kuwa mkulima. Maelekezo hayo yamezingatiwa katika mipango na utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni. Hotuba hiyo imegusa maeneo mengi ya Sekta ya Kilimo. Mhe. Waziri Mkuu amekuwa mstari wa mbele kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji, maendeleo ya Vyama vya Ushirika pamoja na upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo hususan mazao ya kimkakati ya mkonge, chikichi, alizeti, zabibu, ngano, miwa, korosho, kahawa, chai, pamba na tumbaku. Pia, ninamshukuru na yeye mwenyewe kuwa mkulima na mbanguaji wa korosho.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kukupongeza wewe binafsi, na Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb.) pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu tukufu kwa umahiri mkubwa. Uongozi wenu mahiri umewezesha utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo ikiwemo sekta ya kilimo. Aidha, nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote kwa umahiri wao mkubwa katika kuchangia mijadala inayoendelea katika Bunge hili la 12 la Bajeti.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee na kwa dhati ninapenda nikushukuru wewe binafsi kwa kuunda Kamati moja inayosimamia viwanda, biashara, kilimo na mifugo. Hatua hii, inajenga msingi imara wa sekta za uzalishaji na biashara katika kusimamia kwa pamoja, kupanga, kutekeleza na kuratibu na hivyo kuongeza tija na thamani ya mazao ya wakulima wa nchi hii.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo na Mbunge wa Jimbo la Dodoma mjini kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Kilimo. Pia, ninampongeza Bw. Gerald Geofrey Mweli kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo. Vilevile, ninampongeza Dkt. Hussein Mohamed Omar kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo. Ninawashukuru kwa ushirikiano wanaonipatia, ninawashukuru kwa wao kutambua majukumu, wajibu na matarajio ya Mhe. Rais, Bunge lako Tukufu na watanzania kwa ujumla. Aidha, ninapenda kumshukuru Bw. Andrew Wilson Massawe, Katibu Mkuu mstaafu kwa ushirikiano wake alionipatia wakati akiwa katika utumishi wa umma.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa Mufindi Kusini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo na Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Vilevile, ninawapongeza wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo na Kamati ya Kudumu ya Bajeti kwa ushauri wao mzuri ambao umeboresha utekelezaji wa mipango na mikakati ya Wizara.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.) pamoja na timu ya wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango ikiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Natu El-maamry Mwamba na Manaibu Katibu Wakuu Wizara ya Fedha na Mipango Bi. Jenifa C. Omolo, Bi. Amina K. Shaaban na Bw. Lawrence N. Mafuru; na Kamishna wa Bajeti Bw. Meshack J. Anyingisye kwa kutupa nafasi ya kujadiliana na kushauriana kuhusu namna bora ya kutekeleza vipaumbele vya Sekta ya Kilimo na kuipa kipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Serikali. Ninawashukuru sana kwani hii ni hatua sahihi kwa maslahi ya nchi yetu na kulinda uchumi wetu.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Abdul Yussuf Maalim kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Amani - Zanzibar. Aidha, ninatoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani - Zanzibar, Mhe. Mussa Hassan Mussa. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, Amina.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda Waziri Mkuu Mstaafu kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Kumshauri Rais kuhusu masuala ya chakula na kilimo (Presidential Food and Agriculture Delivery Council) na Makamu Mwenyekiti wa Baraza Mhe. Hailemarian Dessalegn Waziri Mkuu Mstaafu wa Ethiopia. Ninaahidi kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Kilimo.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee ninawashukuru wakulima wa nchi hii na sekta binafsi ya kilimo, kwa mchango wao mkubwa katika kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula na kuongeza uuzaji wa mazao nje ya nchi kutoka Dola za marekani Milioni 994.5 mwaka 2021 hadi Dola za Marekani Bilioni 1.38 kufikia Aprili mwaka 2023. Aidha, ninawashukuru viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano wao na bidii yao katika kazi. Vilevile, ninawashukuru Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara na watumishi wake kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa. Pia, ninawashukuru kwa dhati taasisi za fedha, sekta binafsi, wabia wa maendeleo na Asasi zisizo za Kiserikali kwa mchango wao katika kukuza sekta ya kilimo nchini.

18. ***Mheshimiwa Spika***, ninatoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Nzega – Mjini kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, ninawapongeza kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo yao wenyewe na Jimbo letu.

19. Ninawashukuru sana watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Nzega inayoongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Bi. Belbara Kasindi Makono na Mkurugenzi Bw. Shomary Salim Mndolwa, Viongozi na Madiwani wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Nzega kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia hata pale ninapokuwa sipatikani Jimboni nikitekeleza majukumu yangu ya kuwahudumia wakulima na watanzania kwa ujumla. Viongozi hawa wameendelea kuwahudumia wananchi na shughuli za maendeleo hazijasimama. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa uaminifu kwa maendeleo ya Jimbo letu la Nzega – Mjini.

## 1.0 HALI YA UPATIKANAJI WA CHAKULA

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Taifa letu limetoka kufanya sensa ya watu na makazi na takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watanzania ni Milioni 61.74. Kati ya hao asilimia 65.6 sawa na zaidi ya Watanzania milioni 40 maisha yao ya kila siku yanategemea sekta ya kilimo moja kwa moja na watanzania wote Milioni 61.74 wanahitaji chakula.

21. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na matokeo ya Sensa ya kilimo ya mwaka 2020, takwimu zinaonesha kuwa Tanzania bara ina jumla ya kaya 11,659,589. Kati ya hizo, kaya 5,088,135 zinategemea kilimo moja kwa moja sawa na asilimia 43.6 ya kaya zote. Aidha, ifikapo mwaka 2030, Taifa letu linakadiriwa kuwa na watanzania Milioni 71 na mwaka 2050 watanzania tunakadiriwa kufikia Milioni 136. Vilevile, wakati wastani wa umri wa Mtanzania ni miaka 18, Afrika ni miaka 20, Ulaya miaka 40 na Asia miaka 30, maana yake Tanzania ni Taifa la vijana. Hii inamaanisha kuwa Taifa letu lina hazina kubwa ya nguvu kazi kwa ajili ya kuzalisha chakula chetu na ziada kuuza nje ya nchi.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula katika mwaka 2021/2022 ni tani Milioni 17.14 ambapo mahitaji ya chakula kwa mwaka 2022/2023 ni tani milioni 15.05. Kutokana na uzalishaji huo, Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 114. Aidha, makadirio ya mahitaji ya chakula ifikapo mwaka 2030 yatakuwa tani milioni 20 na mwaka 2050 yatakuwa tani milioni 33.7. Hali hii inaleta changamoto kwa nchi yetu kuwa na mikakati ya uwekezaji ya muda mrefu kwenye Sekta ya Kilimo ili kuhakikisha utoshelevu wa chakula kwa miaka hiyo na ziada kwa ajili ya kuuza nje ya nchi.

### Mchango wa Kilimo katika Uchumi

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2021 ilikua kwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2020. Vilevile, Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 26.1 katika Pato la Taifa; imetoa ajira kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 65.6 na kuchangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda na asilimia 100 ya chakula nchini.

24. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa mwenendo wa ukuaji wa idadi ya watu ndani ya nchi na duniani ifikapo mwaka 2050, nchi yetu itakuwa na idadi ya watu milioni 136 na dunia itakuwa na watu bilioni 9.7. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa chakula duniani unakadiriwa kupungua kwa asilimia 4 wakati mahitaji halisi ya chakula yanakadiriwa kuongezeka kwa zaidi ya asilimia 50.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** kihatarishi namba moja kwa taifa letu itakuwa ni mabadiliko ya tabianchi ambayo yanasababisha kupungua kwa uzalishaji wa chakula na hivyo kuhatarisha uimara wa uchumi wetu na usalama wa Taifa letu. Ili kuwa salama kwenye eneo hili ni lazima kuendelea kuwekeza katika mifumo imara na himilivu ya kilimo inayotumia teknolojia za umwagiliaji za kisasa, uwezo wa kuhifadhi mbegu zetu za asili ili kuwa msingi imara wa kufanya utafiti kupata teknolojia bora za uzalishaji wa mbegu ili kujihakikishia usalama wa chakula na ulinzi wa uchumi wetu.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Taifa lolote ambalo liko huru, lenye kulinda heshima na utu wa watu wake, ni lile ambalo linajitosheleza kwa chakula na uchumi imara. Ili uwe na uhakika wa chakula ni lazima kuimarisha uzalishaji, tija na kuwa na umiliki wa mbegu zetu kwani atakayetawala dunia hii ni yule ambaye ana umiliki wa mbegu bora na utoshelevu wa chakula.

27. ***Mheshimiwa Spika***, Tathmini ya Kina ya Hali ya Chakula na Lishe imebaini kuwa na upungufu wa uzalishaji katika baadhi ya maeneo katika msimu wa 2021/2022 uliotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na hivyo kusababisha kupanda bei kwa baadhi ya mazao ya chakula. Ili kukabiliana na hali hiyo, Wizara kupitia NFRA ilichukua hatua za kusambaza chakula wastani wa tani 75,282.30 za mahindi na kuuzwa kwa bei ya chini ya soko kati ya Shilingi 680 hadi 920 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya soko ya Shilingi 1,200 hadi 1,500 lengo likiwa ni kumlinda mlaji na kudhibiti mfumuko wa bei.

28. ***Mheshimiwa Spika***, ili kukabiliana na upungufu wa chakula, Serikali inaendelea kuongeza uwezo wake wa kuhifadhi chakula kutoka tani 251,000 za sasa hadi tani 506,000. Aidha, kwa sasa Serikali imeanza shughuli ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga miundombinu ya uhifadhi itakayoongeza uwezo wa kuhifadhi kufikia tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030. Lengo ni kuhakikisha kuwa, Taifa letu linauwezo wa kuhifadhi chakula cha kutumia miezi sita (6) pindi inapotokea janga ili kulinda uchumi wetu, heshima yetu, utu wetu na uhuru wetu. ***(Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 01 hadi 15 wa kitabu cha hotuba yangu).***

## UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/2023

### Maeneo ya kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2022/2023

29. ***Mheshimiwa Spika,*** utakumbuka wewe na Bunge lako Tukufu tarehe 17 Mei mwaka 2022, nilisimama hapa kuomba idhini ya kupitishiwa bajeti ya Shilingi **Bilioni 751** na Bunge lako likaidhinisha ili kutekeleza Mpango wa mwaka 2022/2023. Katika mpango huo tulikuwa na maeneo ya vipaumbele vya kimkakati 13 (13 Strategic Priorities).
30. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa mwaka 2022/2023 na unaokuja wa mwaka 2023/2024, msingi wake mkuu ni Dira ya Maendeleo ya Taifa Mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2020/2021 – 2025/2026), Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Hotuba ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa Bungeni tarehe 22 Aprili 2021, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) Mwaka 2017/2018 – 2027/2028 na Mpango wa Kuimarisha Sekta ya Kilimo (Agenda 10/30).
31. ***Mheshimiwa Spika,*** leo nipo mbele yako kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa kile ambacho tuliahidi mbele ya Bunge lako tukufu. Maeneo hayo ni;
    (i) Kuimarisha utafiti;
    (ii) Kutoa ruzuku ya mbegu za alizeti, ngano na miche ya chikichi;
    (iii) Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo;
    (iv) Kuimarisha na kutoa huduma ya upimaji wa afya ya udongo;
    (v) Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji;
    (vi) Kuimarisha huduma za ugani na kuhamasisha kilimo cha ukanda kutokana na Ikolojia za kilimo;
    (vii) Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo;
    (viii) Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa Mitaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo;
    (ix) Kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya kilimo;
    (x) Kuhamasisha na kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa ya pamoja;
    (xi) Kuanza kutoa ruzuku ya mbolea mwaka 2022/2023;
    (xii) Kuimarisha Kilimo Anga; na
    (xiii) Kuimarisha maendeleo ya ushirika.

32. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa tumetekeleza mikakati na miradi yote tuliyoahidi ndani ya Bunge lako kama nitakavyotoa maelezo huko mbele.

### 1.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Fungu 43**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **5,017,732,000.00** kupitia Fungu 43, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 2023, Wizara imekusanya Shilingi **3,964,278,605.12** sawa na asilimia **79** ya makadirio. Inatarajiwa kuwa malengo yaliyowekwa yatafikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Fungu 05**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **126,100,000,000.00** kupitia Fungu 05, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 2023, Wizara imekusanya Shilingi **679,574,980.00** sawa na asilimia **0.5** ya makadirio. Ukusanyaji huo mdogo umechangiwa na kutokuwepo kwa Ofisi za umwagiliaji za Wilaya, kutokusajili skimu za umwagiliaji na wakulima, uelewa mdogo wa wakulima kuhusu umuhimu wa ada ya huduma za umwagiliaji, ukosefu wa mfumo wa kielektroniki wa makusanyo na ukosefu wa wahandisi wa umwagiliaji wa wilaya ambao ndio wenye jukumu la msingi la ukusanyaji wa maduhuli hayo.

35. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imefungua ofisi 121 za Wilaya za umwagiliaji na kuajiri wataalam 320 ambao hivi sasa wamepangwa katika wilaya kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. Vilevile, tarehe 20 Machi 2023, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua na kugawa magari 53 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za umwagiliaji ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli.

### 1.2 Fedha Zilizoidhinishwa kwa Mafungu Yote (43, 24 na 05)

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara ya Kilimo ilitengewa jumla ya Shilingi **751,123,280,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24. Kati ya Bajeti hiyo, Shilingi **569,970,337,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **181,152,943,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

### 1.3 Fedha zilizotolewa

37. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2023, Shilingi **549,955,905,275.02** sawa na asilimia **73.22** ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **470,755,975,006.63** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **79,199,930,268.39** ni kwa ya matumizi ya kawaida. Fedha za maendeleo zilizotolewa zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na uhifadhi, kuimarisha utafiti na uzalishaji wa mbegu bora, kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja na kugharamia ruzuku ya mbolea.

38. ***Mheshimiwa Spika***, bajeti ya maendeleo kwa ajili ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ilikuwa ni Shilingi **Bilioni 361.5** kwa ajili ya kuendeleza miradi 69 ya umwagiliaji kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 95,005 ili kuongeza mtandao wetu wa umwagiliaji kutoka hekta 727,280.6 hadi kufikia hekta 822,285.6**.**

39. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia Aprili, 2023 miradi 48 kati ya 69 sawa na asilimia 70 ya miradi ya ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 58,807 yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 234.127** imeanza kutekelezwa ambapo jumla ya wakandarasi 48 wanaendelea na utekelezaji katika Mikoa 15 kwenye Wilaya 31, Halmashauri 31 na Majimbo 32.

40. Vilevile, Shilingi **Bilioni 85.16** zimeshalipwa na fedha zingine zinaendelea kulipwa kulingana na wakandarasi watakavyoendelea kuwasilisha hati za madai (Interim certificates). Miradi yote inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 18 hadi 24. Kadhalika, utekelezaji wa miradi hiyo umezalisha ajira 298,835 za moja kwa moja za kudumu na za muda mfupi.

### Utekelezaji wa Maeneo ya Kipaumbele kwa mwaka 2022/2023

### 1.1 Kuimarisha Utafiti

41. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Shilingi **Bilioni 40.73** ili kutekeleza maeneo ya msingi katika utafiti kama ifuatavyo:-
    i. Kuongeza uzalishaji wa mbegu za awali za mazao ya kimkakati kutoka tani 226.5 mwaka 2020/2021 hadi tani 1,453.
    ii. Kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika eneo la ekari 2,135 kwenye vituo 16 vya Utafiti wa Kilimo.
    iii. Kujenga, kukarabati, kununua vifaa na vitendanishi vya maabara tatu (3) za utafiti.
    iv. Kujenga ghala tano (5) katika vituo vitano (5) vya utafiti zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 2,075 za mbegu.
    v. Kujenga uzio katika kituo cha TARI Uyole kwa ajili ya kuzuia uvamizi wa maeneo ya utafiti.
    vi. Kuanza kukusanya na kusafisha mbegu za asili.

42. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia Aprili, 2023, Wizara imezalisha mbegu za awali tani 519.112 sawa na asilimia 36 ya lengo na uzalishaji unaendelea. Mbegu hizo zina uwezo wa kuzalisha tani 210,607 za mbegu zilizothibitishwa ifikapo mwaka 2024/2025 kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima.

43. Vilevile, mkandarasi kwa ajili ya kuchimba visima 25 kwenye vituo 17, mabwawa manne (4) kwenye vituo vinne (4), kujenga matenki 25 kwenye vituo 17 na kununua na kusimika vifaa vya umwagiliaji yupo kwenye eneo la mradi (site) na ameanza kazi. Kazi hiyo itakamilika mwaka 2024 na inakadiriwa kuzalisha ajira 1,000 na itaongeza uzalishaji wa mbegu za awali kutoka tani 1,225.872 mwaka 2021/2022 hadi tani 26,311 zenye uwezo wa kuzalisha mbegu zilizothibitishwa tani 452,650 ifikapo mwaka 2030.

44. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2023, ukarabati wa maabara ya TARI Tengeru umekamilika; ukarabati wa maabara za TARI Mlingano na TARI Mikocheni unaendelea; ujenzi wa maabara ya TARI Mlingano kwa ajili ya uzalishaji wa miche kwa njia ya chupa (tissue culture) umefikia asilimia 20; na vifaa na vitendanishi vya maabara za TARI Mlingano, Ukiriguru na Mikocheni vimenunuliwa. Vilevile, ujenzi wa ghala tano (5) zenye vyumba vya ubaridi katika vituo vya TARI Hombolo, Tumbi, Naliendele, Selian na Dakawa umefikia asilimia 22. Pia, ujenzi wa uzio katika eneo la kituo cha TARI Uyole lenye ekari 2,605 unaendelea.

45. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2023, TARI imekusanya aina 337 za mbegu za asili za mpunga na mbogamboga. Kati ya hizo, aina 74 zimeanza kusafishwa na kuzalishwa kwa ajili ya kuwafikia wakulima na kuhifadhi. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 16 hadi 26 wa kitabu cha hotuba yangu).***

### 1.2 Kuimarisha Kilimo cha Umwagiliaji

46. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Shilingi **Bilioni 361.5** kwa ajili ya kutekeleza maeneo ya kipaumbele ya umwagiliaji kama ifuatavyo:-
    i. Kujenga skimu 25 mpya zenye jumla ya hekta 53,234 ;
    ii. Kujenga mabwawa 14 ya kuvunia maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji yenye jumla ya mita za ujazo 131,535,000;
    iii. Kukarabati na kukamilisha skimu 30 zenye jumla ya hekta 41,771;
    iv. Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mabonde ya kimkakati 22 yenye jumla ya hekta 306,361 na skimu 42 zenye jumla ya hekta 91,357;
    v. Kununua magari 38 kwa ajili ya kusimamia kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika ofisi za umwagiliaji za mikoa na wilaya;
    vi. Kununua mitambo 12 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; na
    vii. Kufungua ofisi 146 za Umwagiliaji za Wilaya na kuajiri wahandisi na wataalam mbalimbali wa kilimo 320.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia Aprili 2023, mikataba 48 yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 234.12** kwa mwaka imesainiwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika miradi 48 sawa na asilimia 70 ya lengo la kujenga na kukarabati miradi 69. Kati ya miradi hiyo, miradi 19 ni ya ujenzi wa skimu mpya sawa na asilimia 76 ya lengo la ujenzi wa skimu mpya, miradi 19 ni ya ukarabati wa skimu sawa na asilimia 63.3 ya lengo la ukarabati wa skimu na miradi 10 ni ya ujenzi wa mabwawa sawa na asilimia 71.4 ya lengo la ujenzi wa mabwawa. Utekelezaji wa miradi hiyo utafanyika kwa kipindi cha miezi 18 hadi 24 kwa mujibu wa mikataba.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji iliyopangwa kutaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 95,005 na hivyo kufanya eneo la umwagiliaji kuwa hekta 822,285.6 sawa na asilimia 68.5 ya lengo la kufikia hekta 1,200,000 za umwagiliaji ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025. Aidha, utekelezaji huo utatengeneza ajira 475,025 za kudumu na za muda mfupi.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2023, mikataba 22 yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 25** imesainiwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mabonde 22 ya kimkakati sawa na asilimia 100 ya lengo na kazi inaendelea. Aidha, Tume imesaini mikataba 13 yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 3.93** kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika miradi 13 sawa na asilimia 30.95 ya lengo la kufanya upembuzi yakinifu katika 42 na utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika skimu hizo umeanza. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde na skimu hizo utafanyika katika kipindi cha mwaka 2023/2024 na 2024/2025.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imefungua ofisi 121 za umwagiliaji za Wilaya sawa na asilimia 82.87 ya lengo na kuajiri watumishi wapya 320 ambao wamepelekwa katika ofisi za umwagiliaji za Wilaya kusimamia miradi ya umwagiliaji; imenunua magari 53 sawa na asilimia 139.5 ya lengo kwa bajeti ileile ya thamani ya Shilingi **Bilioni 8.34** kwa ajili ya kuimarisha ofisi za umwagiliaji za Wilaya; na imenunua mitambo 15 sawa na asilimia 125 ya lengo na magari makubwa (heavy trucks) 17 kwa bajeti ileile ya thamani ya Shilingi **Bilioni 15.6** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji.

51. ***Mheshimiwa spika,*** Tume imesaini hati ya makubaliano (MoU) na kampuni mbili (2) kutoka nchi za Italia na Uhispania kwa ajili ya kuendeleza mradi wa Bonde la Mto Mara na mradi wa Kisegese katika Bonde la Kilombero. Utaratibu utakaotumika katika kutekeleza miradi hiyo ni ''Engineering Procurement Construction and Financing'' -EPCF. (**Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 26 hadi 32 wa kitabu cha hotuba yangu).**

### 1.3 Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo

**Mbegu bora**

52. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Bunge lako





Tukufu liliidhinisha Shilingi **Bilioni 43.03** kutekeleza maeneo ya msingi ya kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora kama ifuatavyo;

i. Kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 1,791.5 katika mashamba ya mbegu ya Tengeru, Mwele, Arusha na Kilimi;
ii. Kuongeza eneo jipya hekta 4,000 katika mashamba ya Msimba, Kilimi, Mwele na Mbozi kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora;
iii. Kujenga uzio katika mashamba ya mbegu kwa ajili ya kuzuia uvamizi;
iv. Kujenga bwawa lenye mita za ujazo 82,000 katika shamba la Arusha; na kuchimba visima virefu nane (8); na
v. Kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali tani 127,650 kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) na Sekta Binafsi.

***53. Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia Aprili 2023, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba matano (5) ya mbegu yenye ukubwa wa ekari 2,025 umefikia asilimia 25; uchimbaji wa visima virefu sita (6) sawa na asilimia 75 ya lengo la kuchimba visima vinane (8) katika shamba la mbegu la Msimba umekamilika; mashamba pori yenye ukubwa wa ekari 1,250 ya Kilimi-Nzega; Msimba-Kilosa; Mwele-Tanga na Namtumbo-Ruvuma yameendelezwa; na ujenzi wa uzio wenye urefu wa Kilomita 23 kwenye shamba la Msimba na Kilomita 12 katika shamba la Kilimi-Nzega kwa ajili ya kuzuia uvamizi umefika asilimia 60 na 70, mtawalia.

***54. Mheshimiwa Spika***, upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani 64,152.11 sawa na asilimia 50.25 ya lengo la tani 127,650. Kati ya kiasi hicho, tani 44,344.4 zimezalishwa nchini, tani 14,690.41 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na tani 5,117.3 ni bakaa ya msimu wa 2021/2022 na uzalishaji unaendelea. Vilevile, Wizara imeanza kuwapatia ardhi Sekta binafsi ya kitanzania ndani ya mashamba ya ASA kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora. Jumla ya Kampuni tisa (9) zimepatiwa ardhi yenye ukubwa wa ekari 5,477.5 katika mashamba ya mbegu ya Mbozi na Dabaga. Hatua hii imewezesha uzalishaji wa mbegu bora tani 7,536 na kuzalisha ajira 3,750.

**Miche bora**

***55. Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Taasisi zake, Halmashauri na Sekta binafsi ilipanga kuzalisha jumla ya miche ya mazao mbalimbali 101,000,000 na kusambaza kwa wakulima. Hadi kufikia Aprili, 2023 miche 61,486,921 sawa na asilimia 60.87 ya lengo imezalishwa na kusambaza kwa wakulima na usambazaji unaendelea.

**Mbolea**

***56. Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TFRA ilipanga kuratibu uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa tani 650,000 za mbolea kwa msimu wa kilimo 2022/2023 unaoishia mwezi Juni 2023. Hadi kufikia Aprili 2023, upatikanaji wa mbolea umefikia tani 819,442 ikiwa ni asilimia 126 ya lengo. Kiasi hicho kimetokana na tani 75,399 zilizozalishwa nchini, tani 617,079 zilizoagizwa nje ya nchi na tani 126,964 bakaa ya msimu wa mwaka 2021/2022. Hili ni ongezeko la asilimia 46 ikilinganishwa na msimu wa 2021/2022 ambapo upatikanaji wa mbolea ulikuwa tani 560,551.

**Viuatilifu**

***57. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara ilipanga kununua lita 118,500 kwa ajili ya kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mazao na mimea. Hadi kufikia Aprili, 2023 Wizara kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) imenunua lita 106,000 sawa na asilimia 89.45 ya lengo. Aidha, lita 82,424 na kilo 2,000 za viuatilifu zimesambazwa katika Halmashauri 58 za mikoa 10 na kudhibiti milipuko ya viwavijeshi, nzi wa matunda na panya na kuweza kuokoa upotevu wa mazao ya mpunga, mahindi, mtama na uwele katika eneo la hekta 110,000 za mashamba ya wakulima. Vilevile, Wizara imedhibiti milipuko ya ndege waharibifu wa mazao (kwelea kwelea) katika Halmashauri 11 za Mikoa mitano (5) ambapo lita 2,670 za viutailifu zimetumika.

***58. Mheshimiwa Spika***, Wizara imewezesha upatikanaji na usambazaji wa ekapaki 1,823,688 kwa wakulima wa zao la pamba sawa na asilimia 40.5 ya lengo la ekapaki 4,500,000 na ambapo jumla ya wakulima 550,000 wamenufaika. Aidha, imewezesha upatikanaji na usambazaji wa viuatilifu vya korosho tani 15,015.03 sawa na asilimia 60 ya lengo la kusambaza tani 25,000 za salfa ya unga na lita 2,684,470.5 sawa na asilimia 178.9 ya lengo la lita 1,500,000 za viuatilifu vya maji ambapo wakulima 483,000 wamenufaika. Pia, Wizara imewezesha upatikanaji wa viuatilifu vya tumbaku lita 84,938.48 (Yamaotea na Deltamethrine), pakiti 480,721 za imidacloprid 70% WG ambapo jumla ya wakulima 70,318 wamenufaika.

***59. Mheshimiwa Spika***, TPHPA imekagua maduka 314 katika Mikoa 12 kwa lengo la kudhibiti ubora wa viuatilifu na kutoa mafunzo kuhusu matumizi salama na sahihi ya viuatilifu kwa wadau 711. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba ….. hadi …… wa kitabu cha hotuba yangu).***

**Zana za Kilimo**

***60. Mheshimiwa Spika***, Sekta binafsi kwa kushirikiana na taasisi za fedha na *guarantee schemes* imetengeneza mfumo wa wakulima kukopeshwa zana za kilimo kwa kutumia dhamana ya zana zenyewe hii imeongeza idadi ya matrekta kufikia matreka 614. Hivyo, hadi kufikia Aprili, 2023 idadi ya matreka makubwa imeongezeka kutoka 21,149 mwaka 2021/2022 hadi 22,849 na matrekta madogo kutoka 9,420 mwaka 2021/2022 hadi 11,379. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 32 hadi 47 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**1.4 Ruzuku ya Mbegu na Miche**

***61. Mheshimiwa Spika***, Wizara ilipanga kutoa mbegu za alizeti tani 5,000 kupitia mpango wa ruzuku. Hadi kufikia Aprili 2023, Wizara kupitia ASA imesambaza mbegu bora za alizeti tani 1,004 kwa wakulima katika Halmashauri 39 ili kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti. Vilevile, tani 80 za mbegu bora za ngano zimesambazwa katika Wilaya ya Makete kwa mpango wa ruzuku.

***62.*** Vilevile, Wizara ilipanga kuzalisha na kusambaza miche ya mazao mbalimbali kwa mpango wa ruzuku. Hadi kufikia Aprili, 2023, ASA kwa kushirikiana na JKT, Magereza, TARI na Halmashauri za Mikoa saba (7) imezalisha na kusambaza miche ya chikichi 1,158,313 inayotosheleza kupandwa katika eneo la hekta 9,266.49. Miche hiyo inatarajiwa kuzalisha tani 37,065.96 za mafuta ifikapo mwaka 2030 na kuzalisha ajira takribani 46,000. Pia, TARI imezalisha miche ya zabibu 210,523 na kusambaza miche 98,815 kwa wakulima katika Wilaya nne (4) za Mkoa wa Dodoma na usambazaji unaendelea. Miche hiyo inatosheleza kupandwa katika eneo lenye ukubwa wa ekari 197.25.

***63. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kusambaza mbegu na miche bora kwa mpango ruzuku ya mazao kujigharamia yenyewe kupitia Bodi za Mazao. Hadi kufikia Aprili, 2023, Bodi ya Pamba Tanzania imesambaza mbegu za pamba tani 22,146 katika Wilaya 56 kwenye Mikoa 17 inayolima zao la pamba; Bodi ya Korosho Tanzania imesambaza miche bora ya korosho 11,000 katika Mikoa 13; Bodi ya Mkonge Tanzania imesambaza miche ya Mkonge 12,633,536 katika Halmashauri 15; na Bodi ya Kahawa Tanzania kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imezalisha na kusambaza miche bora ya kahawa 8,784,146 sawa na asilima 43.9 ya lengo la kuzalisha miche 20,000,000 na uzalishaji wa miche unaendelea ili kufikia lengo hilo.

**1.5 Ruzuku ya Mbolea**

***64. Mheshimiwa Spika***, Wizara ilipanga kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wote kwa mazao yote nchini na kusajili wakulima. Hadi kufikia Aprili, 2023 tani 449,795 za mbolea ya ruzuku zimesambazwa. Takwimu zinaonesha kuwa matumizi ya mbolea yameongezeka kutoka tani 363,599 mwaka 2021/2022 hadi tani 449,795 mwaka 2022/2023 na matarajio ni kufikia tani 500,000 ifikapo Juni 2023. Kadhalika, timu yetu ya tathmini inafuatilia usambazaji wa mbolea ya ruzuku na matumizi yake.

***65. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya wakulima 3,050,621 wamesajiliwa ambapo wakulima 801,776 wamenufaika na mpango wa ruzuku ya mbolea kwenye mikoa 26. Aidha, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu tumewatambua wakulima wanaonufaika na mbolea ya ruzuku kwa majina yao kamili, mahali walipo, aina ya mazao, ukubwa wa mashamba yao na maeneo wanayofanyia shughuli za kilimo. Lengo ni kusajili wakulima wasiopungua 7,000,000 na zoezi hili la kusajili na kutoa kadi litakamilika mwaka 2025 na kuunganisha kanzidata hii na satellite, taarifa za afya ya udongo kwa kila mkulima na huduma za ugani ili taifa letu kuwa na uhakika wa takwimu na taarifa za wakulima.

***66. Mheshimiwa Spika***, Pia, waingizaji wakubwa wa mbolea 28, mawakala wadogo 3,265 na wazalishaji watatu (3) ndani ya nchi wamesajiliwa katika mfumo wa ruzuku ya mbolea ili kuhakikisha usambazaji wa mbolea unafanikiwa. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 48 hadi 51 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**1.6 Kuimarisha Huduma za Ugani, Mafunzo na Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo**

***67. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Shilingi **Bilioni 15** kwa ajili ya kuimarisha huduma za ugani, mafunzo na Vyuo na Vituo vya Mafunzo kama ifuatavyo:-

i. Kufunga GPS kwenye pikipiki za maafisa ugani na kuweka mfumo wa usimamizi wa huduma za ugani;
ii. Kusambaza vitendea kazi vya kupimia afya ya udongo kwa maafisa ugani wa Halmashauri 122; vishikwambi 6,377; visanduku vya ugani (Extension Kits) 400 katika Halmashauri 46;
iii. Kuanzisha kituo cha huduma za mawasiliano ya kilimo (Call centre) kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa ushauri wa kitaalam na taarifa za masoko kwa wadau wa kilimo;
iv. Kudahili wanafunzi 2,200 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada; na
v. Kukarabati wa miundombinu ya Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo Uyole, KATRIN, Inyala, Ukiriguru, Igurusi, Mtwara, Mlingano, HORTI – Tengeru na Vituo vya Mafunzo kwa Wakulima vya Bihawana, Ichenga na Mkindo.

***68. Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia Aprili, 2023 pikipiki 5,889 sawa na asilimia 84.12 ya lengo la kusambaza pikipiki 7,000 zimesambazwa katika Mikoa 25 ili kuwawezesha maafisa ugani kutoa huduma kwa wakulima kwa ufanisi; Kituo cha ufuatiliaji (Control Center) wa matumizi ya pikipiki za maafisa ugani kimenzishwa; na GPS 979 zimefungwa kwenye pikipiki za maafisa ugani katika Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Morogoro na Iringa na zoezi linaendelea. Aidha, Kituo cha Huduma kwa Wateja (Kilimo Call Centre) kimeanzishwa.

***69. Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2022/2023, imedahili wanafunzi 3,151 sawa na asilimia 143 ya lengo la kudahili wanafunzi 2,200 katika Vyuo 14 vya Mafunzo ya Kilimo vya Umma ngazi ya Astashahada na Stashahada katika fani za Kilimo. Vilevile, Vyuo Binafsi 14 ambavyo vinatumia mitaala ya Wizara katika kutoa mafunzo ya kilimo vimedahili jumla ya wanafunzi 1,031. Kadhalika, ukarabati wa miundombinu ya majengo katika Vyuo vya NSI Kidatu, Ilonga, Tumbi, Uyole, Ukiriguru, Mubondo na KATRIN unaendelea. Aidha, Ukarabati wa Kituo cha Mafunzo ya Kilimo kwa Wakulima Bihawana umekamilika na kuzalisha ajira 1,109 za vijana. Vilevile, Wizara imenunua na kusambaza samani katika Vituo vitano (5) vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (WARCs) katika mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu. Vilevile, Wizara imesambaza matrekta madogo (powertiller) 11 katika WARCs za Mikoa tisa (9). Vilevile, Wizara imenunua vishikwambi 580, kompyuta 143 na *printer* 143. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 54 hadi 61 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**1.7 Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo**

***70. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara ilipanga kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi; kuhamasisha uwekaji chapa (branding) kwenye bidhaa za kilimo; na kuimarisha mauzo ya mazao; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kituo mahiri cha usimamizi wa mazao baada ya kuvuna; kukamilisha ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mazao kibiolojia na kuanza ujenzi wa maabara kuu ya kilimo kwa ajili ya kudhibiti ubora wa mazao.

***71. Mheshimiwa Spika***, ninaomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia Aprili, 2023, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na Sekta binafsi imewezesha kupatikana kwa fursa za masoko mapya ya mazao nje ya nchi ikiwemo soko la korosho katika nchi ya Marekani ambapo tani 74.19 za korosho iliyobanguliwa zenye thamani ya Dola za Marekani **Milioni 455.72** zimeuzwa; na Soko la tumbaku nchini Japan.

***72.*** Aidha, kiwanda cha tumbaku cha TLTC kilichokuwa kimefungwa kimepata mwekezaji mpya ambaye ni Kampuni ya Mkwawa Leafy Tobacco Processor Limited (MLTL). Kampuni hiyo imenunua na kusindika tani 7,518 za tumbaku na imeingia mkataba wa kununua tani 41,605 za tumbaku kutoka kwa wakulima katika msimu wa kilimo 2022/2023. Vilevile, Kampuni hiyo imeanza ujenzi wa Kiwanda cha sigara katika Mkoa wa Morogoro na kitazinduliwa na kuwekwa jiwe la Msingi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Julai, 2023.

***73. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi imewezesha uwekaji wa chapa kwenye mazao ikiwemo korosho zinazobanguliwa na parachichi na kuuzwa nje ya nchi ili kuyatambulisha na kuyatofautisha na mazao yanayozalishwa nchi nyingine. Aidha, Wizara inaendelea na jitihada za uwekaji chapa kwenye mazao mengine yanayosafirishwa nje ya nchi.

***74. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha soko la ndani Wizara kupitia NFRA na CPB imenunua nafaka tani 69,166.19 za mazao mbalimbali kutoka kwa wakulima. Vilevile, soko la nje limeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Aprili 2023, tani 767,840 za mahindi na mchele zenye thamani ya Dola za Marekani **Milioni 252.55** zimeuzwa nje ya nchi. Pia, tani 396,756 za mazao ya mbaazi, ufuta na dengu zenye thamani ya Dola za Marekani **Milioni 279.41** na parachichi tani 29,031 zenye thamani ya Dola za Marekani **Milioni 52.25** zimeuzwa nje ya nchi. Kadhalika, tani 363,061 za mazao asilia ya biashara zenye thamani ya Dola za Marekani **Milioni 693** zimeuzwa nje ya nchi.

***75. Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa Kituo cha Udhibiti wa Visumbufu Kibaolojia (Kibaha) umefikia asilimia 99; ujenzi wa Kituo Mahiri cha Usimamizi wa Mazao Baada ya Kuvuna (Mtanana – Kongwa) umefikia wastani wa asilimia 70; ujenzi wa Maabara Kuu ya Kilimo iliyopo Mtumba - Dodoma umefikia asilimia sita (6); na ujenzi wa masoko ya kuuzia mbogamboga, matunda na viungo katika Halmashauri za Rungwe, Busokelo na Ileje kuipitia mradi wa AGRI Connect umekamilika. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 61 hadi 65 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**1.8 Kuimarisha Mifumo ya Upatikanaji wa Mitaji**

***76. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ambapo, Amri (Sehemu ya Kanuni za Sheria ya Fedha ya mwaka 2022) ya kuanzishwa mfuko huo imeidhinishwa na Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya kuchapwa kwenye Gazeti la Serikali. Mfuko huo utachochea ukuaji wa maendeleo ya sekta ya mazao ya kilimo; kufidia bei za mazao inaposhuka; kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo (mbolea, mbegu bora, viuatilifu); kuchochea uwekezaji katika shughuli za utafiti wa kilimo; na kuwajengea uwezo wakulima, wasindikaji, maafisa ugani na watafiti wa kilimo.

***77. Mheshimiwa Spika***, katika kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imetoa mikopo ya Shilingi **Bilioni 169.656** kwa ajili ya kufanikisha uzalishaji katika Sekta ya Kilimo. Aidha, mikopo ya Shilingi **Bilioni 57.486** imetolewa kwa Vyama vya Ushirika vitano (5) na kampuni mbili (2) kwa ajili ya ununuzi wa kahawa katika Mikoa ya Kagera, Mara na Mbeya kwa msimu wa mwaka 2022/2023. Pia, mikopo ya Shilingi **Bilioni 21.71** imetolewa kwa Vyama vya Ushirika vitatu (3) na kampuni moja (1) kwa ajili ya ununuzi wa pamba katika msimu wa mwaka 2022/2023. Kadhalika, TADB imetoa Shilingi **Bilioni 17.52** kwa ajili ya ununuzi wa mazao mbalimbali.

***78. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Benki ya CRDB imetoa mikopo ya kilimo yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 801**. Kati ya mikopo hiyo, Shilingi **Bilioni 494** wamepatiwa AMCOS 472 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kilimo, mifugo, misitu na uvuvi. Vilevile, Benki ya NMB imetoa mikopo katika Sekta ya Kilimo yenye thamani ya Shilingi **Trilioni 1.62**.

**Mfuko wa Pembejeo za Kilimo**

***79. Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2022/2023, kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo imetoa mikopo nafuu 20 yenye thamani ya Shilingi **Milioni 704.278**. Vilevile, Wizara kupitia AGITF imeanzisha huduma ya *soft loan* kwa ajili ya vijana na wanawake kupata mitaji na kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kilimo kupitia programu ya BBT. Kwa kuanzia huduma hiyo imewezesha upatikanaji wa mikopo ya Shilingi **Milioni 200**. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 66 hadi 68 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**1.9 Kuimarisha Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya kilimo**

***80. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Shilingi **Bilioni 24** kwa ajili ya ujenzi wa ghala 70 za kuhifadhi mazao katika ngazi ya Kata na Kijiji. Hadi kufikia Aprili 2023, ujenzi wa ghala 28 katika Halmashauri za Wilaya za Songea, Madaba na Namtumbo umeanza.

***81. Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara ilipanga kukamilisha ujenzi wa ghala 14 kupitia mradi wa TANIPAC; kukamilisha ujenzi wa ghala tisa (9) na vihenge 56 kupitia mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi unaotekelezwa na NFRA; na kukamilisha ukarabati wa ghala 17 katika Halmashauri za Songea na Madaba.

***82. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2023 Wizara kupitia mradi wa TANIPAC imekamilisha ujenzi wa ghala 10 kati ya ghala 14 sawa na asilimia 71.4 ya lengo. Aidha, ujenzi wa ghala nne (4) zilizobaki za Engusero - Kiteto, Endanoga - Babati, Ole-Dodeani - Pemba na Lumecha - Namtumbo umefikia wastani wa asilimia 82. Kadhalika, utekelezaji wa Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka umefikia wastani wa asilimia 85. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 69 hadi 72 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**1.10 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika**

***83. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilipanga kuendelea kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Ushirika; kukagua Vyama vya Ushirika 6,150; kuiwezesha COASCO kufanya ukaguzi wa Vyama; kuratibu na kusimamia uendeshwaji wa minada, masoko na mauzo ya mazao ya wakulima kupitia Vyama vya Ushirika; na kuanzisha mfumo wa TEHAMA wa usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU).

***84. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2023, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika. Uhamasishaji huo umewezesha mtaji wa benki hiyo kuongezeka kutoka Shilingi **Bilioni 1.7** mwaka 2020/2021 hadi Shilingi **Bilioni 5.2** Aprili, 2023. Vilevile, Tume imekagua Vyama vya upili 21 na Vyama vya Ushirika vya Msingi 2,972 kati ya vyama 7,300. Kadhalika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) imekagua vyama 6,005 sawa na asilimia 97 ya lengo.

***85. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2023, Tume imeratibu uuzwaji wa tani milioni 1.826 za mazao mbalimbali zenye thamani ya Shilingi **Trilioni 1.752** ikilinganishwa na tani 597,298.58 zenye thamani ya Shilingi **Trilioni 1.552** katika msimu wa 2021/2022. Thamani ya mauzo ya mazao hayo imeongezeka kwa asilimia 11.3.

***86. Mheshimiwa Spika,*** Vyama vya Ushirika 4,661 vimesajiliwa katika Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU). Aidha, maafisa TEHAMA 30, warajis wasaidizi wa mikoa 26, watendaji wa bodi ya mazao 74, maafisa ushirika 421, mameneja 2,482 wa vyama na wahasibu wa vyama 102 wamepatiwa mafunzo kuhusu utumiaji wa Mfumo huo. Vilevile, Tume imeunganisha mfumo wa MUVU kwenye mfumo uunganishi wa Serikali (GeSB) na Mfumo wa mizani ya kidigitali ili kudhibiti wizi wa mazao ya wakulima. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 72 hadi 75 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**1.11 Kuhamasisha Kilimo cha Mashamba Makubwa ya Pamoja**

***87. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Shilingi **Bilioni 3** kwa ajili kuainisha, kutenga, kupima na kulinda ardhi ya kilimo kwa lengo la kuwa na Benki ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa mashamba makubwa ya pamoja yatakayojengewa miundombinu muhimu.

***88. Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya ekari 266,441.6 za mashamba makubwa ya pamoja katika Mikoa ya Kigoma, Mbeya, Njombe, Dodoma na Kagera zimepimwa kwa ajili ya kuyapatia hati miliki. Mashamba hayo yatatumika kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT). Mpango wa Mashamba Makubwa ya Pamoja (Block Farms) ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Machi, 2023, katika shamba la Chinangali lilipo Mkoa wa Dodoma.

**1.12 Ushiriki wa vijana katika Sekta ya Kilimo**

***89. Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2022/2023, ilipanga kuongeza ajira za vijana na wanawake 1,000,000 kwenye Sekta ya Kilimo ifikapo mwaka 2025 kwa kuanzisha programu mbalimbali ikiwemo programu ya vijana ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT).

***90. Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara inatekeleza programu ya miaka minane (8) 2022-2030 ya Jenga Kesho iliyo Bora yenye lengo la kuongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo ya kilimo biashara, kuwahakikishia upatikanaji wa ardhi, mitaji na masoko. Aidha, Programu hiyo, inatekelezwa kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo na Sekta binafsi.

***91. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo, Wizara kupitia tovuti www.bbt.kilimo.go.tz ilitangaza vijana na wanawake wajitokeze kuomba kujiunga na mafunzo ya kilimo biashara yatakayotolewa katika vituo atamizi. Kupitia tangazo hilo, vijana 20,227 waliomba, kati ya hao wanawake ni 4,722 na wanaume ni 15,505.

***92.*** Aidha, baada ya uchambuzi vijana 812 kati ya hao, wanawake ni 282 na wanaume 530 wamekidhi vigezo vya kupata mafunzo ya kilimo biashara katika awamu ya kwanza. Vijana hao wamepelekwa katika vituo atamizi 13 na mafunzo yanaendelea. Mafunzo hayo yanatolewa kwa kipindi cha miezi minne (4) na yatakamilika Agosti 2023. Uchambuzi wa kundi la pili na tatu unaendelea. Baada ya kuhitimu mafunzo hayo, vijana na wanawake hao watapatiwa mashamba yenye ukubwa usiozidi ekari 10 kulingana na aina ya mazao. Mashamba hayo watakayopewa watapewa umiliki (sub leasing) kwa miaka 66.

***93. Mheshimiwa Spika,*** programu hii inahusisha upatikanaji wa vijana, kuwapatia ardhi na mafunzo kwani haina tija kijana kumpa mafunzo na kumrudisha mtaani. Ni ukweli kwamba umiliki wa ardhi ni nyenzo muhimu ya kuwakomboa vijana na wanawake kiuchumi na kama tusipofanya maamuzi ya kuwamilikisha vijana na wanawake ardhi sasa, ipo siku Taifa letu litakuwa na raia ambao wengi wao ni vibarua katika ardhi yao na hawamiliki nyenzo za uzalishaji.

***94. Mheshimiwa Spika***, programu hii itawakaribisha wawekezaji wakubwa katika mashamba hayo watakaonunua na kuongeza thamani ya mazao. Wawekezaji hao watapewa ardhi, watapimiwa afya ya udongo, watapewa *sub leasing tittle* ya miaka 66 na kuingia mikataba ya utendaji na Wizara ya Kilimo. Vilevile, programu hii imeweka msukumo katika mabadiliko ya fikra na mazingira ya kibiashara miongoni mwa vijana na wanawake kwa lengo la kubadili mtazamo wa kuendesha shughuli za kilimo kama shughuli ya kiuchumi na kibiashara na siyo shughuli ya kujikimu ama shughuli ya watu walioshindwa maisha.

***95.*** Pamoja na mpango wa kuwezesha vijana, Wizara inatekeleza mpango wa ujenzi wa miundombinu ya kuongeza thamani na ghala za kuhifadhi mazao. Ujenzi wa miundombinu hiyo unaendelea ikiwemo kiwanda cha kusindika zabibu katika eneo la Chinangali, ghala na kiwanda cha kubangua korosho katika Wilaya ya Manyoni na ugawaji wa mashine ndogo za kubangua korosho katika maeneo ya uzalishaji.

***96. Mheshimiwa Spika***, kama anakuja mwekezaji leo katika Taifa letu tunampokea na kumpatia ardhi, vivutio vyote vya kodi anavyovitaka na sisi viongozi wote tunapiga naye picha. Tutakuwa viongozi wa ajabu kama hatutawawezesha kwa makusudi raia wetu umiliki wa nyenzo za uzalishaji hasa ardhi, fursa za mitaji na teknolojia za kisasa. Ni lazima uchumi wa Taifa letu umilikiwe na Watanzania na ardhi ni silaha namba moja.

***97. Mheshimiwa Spika,*** nitumie Bunge lako tukufu kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kuhamasisha vijana na wanawake kushiriki kwenye kilimo kupitia Progamu ya Jenga Kesho iliyo Bora almaarufu kama *Building a Better Tomorrow* – BBT. Pia, ninamshukuru kwa kuamua kwa makusudi kuanza safari ya kuwamilikisha Watanzania ardhi na kujenga wawekezaji wa ndani ambao watamiliki nyenzo za uzalishaji ili kukabiliana na changamoto za ukoloni mamboleo.

**1.13 Kuimarisha Kilimo Anga**

***98. Mheshimiwa Spika***, matengenezo ya ndege ya kunyunyuzia viuatilifu iliyokuwa Nairobi nchini Kenya yamekamilika na imerejeshwa nchini. Vilevile, manunuzi ya ndege mpya kwa ajili ya shughuli za udhibiti wa visumbufu kwa njia ya anga yamefikia hatua ya upekuzi wa kampuni tatu (3) zilizoainishwa kwa ajili ya utengenezaji wa ndege maalum za udhibiti wa visumbufu.

***99. Mheshimiwa Spika,*** imefika wakati kama nchi kujitegemea katika udhibiti wa nzige, kweleakwelea na visumbufu vingine vya milipuko kwa kutumia ndege zetu za unyunyuziaji badala ya kuendelea kutegemea ndege za mashirika ya nje. ***(Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 75 hadi 83 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**2.0 UZALISHAJI WA MAZAO**

**Mazao Asilia ya Biashara**

***100. Mheshimiwa Spika***, katika msimu wa 2022/2023, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umefikia tani **951,727.77** sawa na asilimia 65.06 ya lengo la kuzalisha tani **1,462,800** na mavuno yanaendelea.

**Mazao ya Chakula**

***101. Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa 2021/2022, uzalishaji wa mazao ya chakula ni tani 17,148,290 ikilinganishwa na tani 18,665,217 mwaka 2020/2021. Kupungua kwa uzalishaji kumetokana na athari za mabadiliko ya tabianchi yaliyopelekea mtawanyiko wa unyeshaji wa mvua usioridhisha.

**1.1 Mazao yenye Mahitaji Makubwa Yanayoagizwa Nje ya Nchi**

**Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari**

***102. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara kupitia Bodi ya Sukari ilipanga kuzalisha tani 4,500,000 za miwa kwa ajili ya kuzalisha sukari tani 450,000. Hadi kufikia Aprili 2023 takribani tani 4,405,350.61 za miwa zimezalishwa ambapo zimezalisha sukari tani 456,019.73 sawa na asilimia 101.34 ya lengo.

***103. Mheshimiwa Spika***, kutokana na uhamasishaji wa uanzishwaji wa viwanda vya sukari nchini, hadi kufikia Aprili 2023 kiwanda cha Sukari Bagamoyo kimeanza uzalishaji ambapo tani 18,127.2 za sukari zimezalishwa. Kadhalika, Kampuni ya Mkulazi Holding Limited inaendelea na usimikaji wa mitambo yenye uwezo wa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka ambapo usimikaji umefikia asilimia 73.

**Zao la Ngano**

***104. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2023 tani 61,968 za ngano zimezalishwa katika msimu wa mwaka 2021/2022. Aidha, uzalishaji wa ngano katika msimu wa mwaka 2022/2023 unaendelea; taratibu za kufufua na kuendeleza mashamba 14 yaliyokuwa chini ya lililokuwa Shirika la NAFCO (hekta 43,538) zinaendelea; na mbegu za awali za ngano tani 51.74 zimezalishwa na TARI ambazo zitazalisha mbegu zilizothibitishwa tani 20,696; na tani 267.65 za mbegu bora za ngano zimezalishwa na ASA na uzalishaji unaendelea. Vilevile, TARI imetathmini aina 322 (lines) za ngano ili kupata aina

zenye mavuno mengi, ustahimilivu wa joto, baridi, ukame na zinazokidhi mahitaji ya soko.

**Mazao ya Mafuta**

**105.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara ilipanga kuzalisha na kusambaza tani 5,000 za mbegu ya alizeti kwa mpango wa ruzuku; kujadiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuweka motisha ya kikodi kwa viwanda vinavyozalisha mafuta ya alizeti nchini kwa kuwaondolea kodi ya ongezeko la thamani; na kuzalisha miche ya chikichi 15,625,000 ifikapo mwaka 2030 sawa na wastani wa miche 2,000,000 kwa mwaka.

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kupitia ASA imesambaza mbegu za alizeti kwa mpango wa ruzuku ambazo zinatosheleza kupandwa katika eneo la ekari 334,667 na kuzalisha mbegu za kukamua tani 234,267 ambazo zitazalisha mafuta tani 58,567.

**107.** ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kulitangazia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) kuanza kazi na itaanza kukutana na wadau wa tasnia ya alizeti ili kupanga bei elekezi ya kununua zao hilo kwa wakulima.

**108.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeweka motisha mahsusi ya kikodi kwa viwanda vya ndani vinavyozalisha mafuta ya alizeti nchini kwa kuwaondolea Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa malighafi na vifungashio vinavyotumiwa kutengeneza mafuta ya kula yanayosafishwa mara mbili (double refine) kwa kutumia mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa nchini. Mpango wa Serikali ni kuimarisha uzalishaji wa ndani ili kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Safari hiyo imeanza ambapo taarifa za Benki Kuu ya Tanzania zinaonesha kuwa hadi Februari, 2022 gharama zilizotumika kuingiza mafuta ya kula (import bill) zimepungua kutoka Dola za Marekani **Milioni 188.7** hadi kufikia Dola za Marekani **Milioni 144.0** Februari, 2023.

**109.** Vilevile, ASA kwa kushirikiana na JKT, Magereza, TARI na Halmashauri za Mikoa saba (7) imezalisha na kusambaza miche ya chikichi 1,158,313 kwa mpango wa ruzuku inayotosheleza kupandwa katika eneo la hekta 9,266.49. Miche hiyo inatarajiwa kuzalisha tani 37,065.96 za mafuta ifikapo mwaka 2030 na kuzalisha ajira takribani 46,000.

**Mazao ya Bustani**

**110.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2022/2023 ilipanga kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani kutoka tani milioni 7.34 hadi tani milioni 8.5; kusimamia uzalishaji wa matumizi ya miche na vipando bora; na kujenga miundombinu ya kuhifadhi mazao ya bustani; kujenga vituo vya huduma ya pamoja (common use facilities) na vyumba vya ubaridi.

**111.** ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uzalishaji wa mazao ya bustani umefikia tani Milioni 7.72 sawa na asilimia 90.8 ya lengo la kuzalisha tani milioni 8.5 na uzalishaji unaendelea. Ili kulinda ubora na kupunguza upotevu wa mazao ya bustani, Wizara imekamilisha usanifu wa ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2) (common use facilities) ambavyo vitajengwa katika Mikoa ya Iringa (Mufindi) na Kilimanjaro (Hai). Vituo hivyo, vitawezesha ukusanyaji, uchambuaji, upangaji wa madaraja na ufungashaji wa mazao ya bustani. Aidha, vituo hivyo vitaendeshwa na Sekta binafsi kwa utaratibu utakaowekwa na Serikali.

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara ilipanga kuhamasisha uzalishaji wa zao la parachichi kufikia tani 215,000; kuwatambua na kuwasajili wazalishaji wa miche ya parachichi; na kuviwezesha vituo vya TARI kuzalisha na kusambaza miche 20,000,000 kwa mpango wa ruzuku.

**113.** ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa zao la parachichi umefikia tani 188,711.8. Vilevile, TARI kwa kushirikiana na Sekta binafsi imezalisha miche ya parachichi Milioni 5.5 ambapo miche Milioni 4.9 inayotosheleza kupandwa katika eneo la hekta 24,019 imesambazwa kwa wakulima na usambazaji unaendelea. Aidha, ifikapo mwaka 2027 tunatarajia mavuno ya parachichi yataongezeka kutokana na usambazaji wa miche hiyo.

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara ilipanga kuhamasisha kuongeza uzalishaji wa zabibu hadi tani 17,430; kuongeza eneo la uzalishaji kutoka hekta 3,426 hadi hekta 3,700; kuhamasisha ufufuaji wa mashamba ya Chinangali II, Gawaye, Hombolo na Dabalo; kuimarisha upatikanaji wa masoko ya zabibu; kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vidogo vya kusindika zabibu; kuongeza uzalishaji wa miche kutoka 120,685 hadi 2,000,000 kwa msimu; na kununua mashine tatu (3) za kusindika zabibu ghafi.

**115.** ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa zao la zabibu umefikia tani 15,513 mwaka 2021/2022; hadi kufikia Aprili 2023 ekari 602 kati ya ekari 1,500 za shamba la Chinangali II kwa ajili ya uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamoja zimeendelezwa; miche ya zabibu 210,523 imezalishwa ambapo miche 98,815 imesambazwa kwa wakulima katika Wilaya nne (4) za Mkoa wa Dodoma na usambazaji unaendelea. Miche hiyo inatosheleza kupandwa katika eneo lenye ukubwa wa ekari 197.25.

**116.** Vilevile, Wizara imeanza ujenzi wa kiwanda cha kusindika zabibu katika Wilaya ya Chamwino ili kuimarisha masoko na kupunguza upotevu wa zao la zabibu na kiwanda hiki kitakabidhiwa kwa Sekta binafsi kukiendesha kwa makubaliano maalum na Serikali. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 83 hadi 105 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, ninapomalizia kutoa taarifa ya utekelezaji katika hotuba yangu kwa muhtasari, ninashukuru sana kwa utashi wa kisiasa na maamuzi ya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge lako Tukufu kwa kuongeza Bajeti ya Wizara kuanzia mwaka huu wa fedha ambapo matokeo ya awali yameanza kuonekana kama ifuatavyo:-

i. Thamani ya mauzo ya mazao nje ya nchi imeongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 994.5 mwaka 2021 hadi Dola za Marekani Bilioni 1.388 mwaka 2023;
ii. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 95,005 unaendelea kutekelezwa;
iii. Ujenzi wa mabwawa 14 yenye jumla ya mita za ujazo 131,535,000 unaendelea;
iv. Tani 44,344.4 za mbegu bora zimezalishwa ikilinganishwa na tani 35,199.4 zilizozalishwa mwaka 2021/2022;
v. Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 90,000;
vi. Ajira za moja kwa moja takribani 486,634 zimezalishwa kutokana na miradi ya maendeleo ya kilimo inayotekelezwa;
vii. Kusambaza pikipiki 5,889 kwa maafisa ugani katika Mikoa 25; na
viii. Kuongezeka kwa ushiriki wa Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi, biashara ya mazao ya kilimo na uzalishaji wa mbegu bora.

**Changamoto**

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, utekelezaji wa Bajeti umekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi ambayo yameathiri uzalishaji wa mbegu bora na uzalishaji wa chakula. Hali hii ndiyo inatupa sababu ya msingi kutenga fedha nyingi kwa ajili ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji, kutafiti na kuzalisha mbegu bora na himilivu, kujenga uwezo wa utabiri na kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mazao na mimea na uhifadhi wa mazao baada ya kuvuna.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele na mipango ya uwekezaji katika Wizara ya Kilimo itaendelea kubakia hivyo kwa miaka minane (8) bali mikakati itaendelea kubadilika kulingana na mahitaji ya wakati.

## 3.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Kilimo inawasilisha bajeti hii mbele ya Bunge lako tukufu wakati dunia ikiendelea kushuhudia ongezeko kubwa la mahitaji ya chakula duniani hususan kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, athari za mabadiliko ya tabianchi, milipuko ya magonjwa ya kuambukiza pamoja na migogoro ya kisiasa ya kikanda inayoendelea sehemu mbalimbali duniani.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (UN - Food and Agriculture Organization) za mwaka 2018, zinaonesha kuwa kutakuwa na ongezeko la idadi ya watu ambapo ifikapo mwaka 2030, idadi ya watu duniani inakadiriwa kufikia Bilioni 8.5 na Bilioni 9.7 ifikapo mwaka 2050. Aidha, idadi ya watu Barani Afrika inakadiriwa kufikia Bilioni 1.6 mwaka 2030 na Bilioni 2.4 mwaka 2050. Vilevile, ifikapo mwaka 2030, Tanzania inakadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 79 na milioni 135 ifikapo mwaka 2050.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watu Afrika inaongezeka kwa asilimia 2.37 na ukuaji wa Sekta ya Kilimo katika bara la Afrika ni asilimia 2.6. Aidha, idadi ya watu Tanzania inaongezeka kwa asilimia 3 na ukuaji wa sekta ya kilimo ni asilimia 3.6 mwaka 2021. Kwa mujibu wa taarifa ya Dakar 2 Summit 2023, Bara la Afrika lina eneo la asilimia 65 linalofaa kwa kilimo lisilotumika ambalo linatosha kuzalisha chakula na kulisha watu Bilioni 9 ifikapo mwaka 2050 duniani.

**123.** Vilevile, taarifa hiyo inaonesha kuwa Afrika ina eneo la Savana peke yake lenye ukubwa wa hekta Milioni 400 zinazofaa kwa kilimo ambapo hekta Milioni 40 sawa na asilimia 10 tu ya eneo lote linalofaa kwa kilimo ndilo linalotumika. Hata hivyo tija ya uzalishaji wa mazao katika eneo linalotumika ni ndogo na kusababisha Bara la Afrika kuagiza chakula kutoka nje ya Afrika zaidi ya tani Milioni 100 zenye thamani ya Dola za Marekani **Bilioni 75** kila mwaka.

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu ina eneo lenye ukubwa wa hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo ambapo hekta milioni 10.8 sawa na asilimia 24.5 ndizo zinazolimwa mazao mbalimbali. Kati ya hizo hekta milioni 29.4 zinafaa kwa umwagiliaji wakati zinazotumika kwa umwagiliaji ni hekta 727,280.6 sawa na asilimia 2.5. Hata hivyo, baadhi ya skimu hizo kiuhalisia zinafanyakazi katika msimu mmoja kwakuwa zinategemea vyanzo vya maji visivyo vya uhakika vinavyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi. Hali hii inasababisha nchi yetu kuagiza ngano kwa thamani ya Dola za Marekani **Milioni 221** na mafuta ya kula kwa thamani ya Shilingi **Bilioni 450** wakati ardhi na nguvukazi tunayo.

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, taarifa ya Dakar 2 Summit 2023 inaonesha zaidi kuwa idadi ya watu duniani wanaokabiliwa na njaa ni Milioni 828 na Bara la Afrika ni Milioni 249. Idadi ya watu duniani wanaoishi chini ya mstari wa umasikini ni takribani Milioni 719, Afrika ni watu Milioni 460 na Tanzania ni watu Milioni 15.8. Aidha, ifikapo mwaka 2050, mahitaji ya chakula Duniani yataongezeka kwa wastani wa asilimia 50 ambapo kwa upande wa Tanzania, mahitaji yanakadiriwa kufikia tani Milioni 33.7.

**126.** ***Mheshimiwa Spika***, hali hii inaleta msukumo wa kipekee kwa nchi yetu kutumia fursa ya biashara ya mazao ya chakula katika soko la Afrika ambayo inakadiriwa kufikia Dola za Marekani **Trilioni 1** ifikapo mwaka 2030. Hatua hiyo, itafungua fursa zaidi za masoko na ajira katika mnyororo wa thamani wa mazao ya chakula na kuondoa watu waliopo kwenye umasikini.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** suala la mifumo ya chakula ni ajenda muhimu kwa nchi yetu kwa sasa. Umuhimu wa ajenda hiyo, unathibitishwa na ushindi tulioupata kuwa mwenyeji wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula barani Afrika (Africa's Food Systems Forum) litakalofanyika tarehe 5 hadi 8 Septemba, 2023 Jijini Dar es Salaam. Tanzania kuwa mwenyeji wa Jukwaa hili ni hatua nyingine ya kuitangazia dunia kwamba nchi yetu ina uwezo wa kuzalisha na kulisha Afrika na Dunia. Matokeo yanayotarajiwa kutokana na jukwaa hili ni pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika Sekta ya kilimo nchini, kukuza utalii na kuimarika kwa biashara ya mazao ya kilimo na teknolojia.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Kilimo ni mwajiri mkuu wa nguvukazi ya taifa na mchangiaji mkuu wa kipato cha wananchi na taifa kwa ujumla. Taarifa ya Sensa ya Kilimo ya mwaka 2019/2020 (National Sample Census of Agriculture) inaonesha kuwa katika msimu wa kilimo 2019/2020 jumla ya kaya za kilimo milioni 3.49 kati ya kaya milioni 7.837 zilitoa taarifa kuwa mauzo ya mazao ya chakula ni chanzo kikuu cha mapato ya biashara nchini ambapo wastani wa kipato kwa kila kaya kilichotokana na mauzo hayo kilifikia Shilingi 1,234,056. Kipato hiki bado ni kidogo na sababu kubwa ni tija ndogo. Hata hivyo, hali hii inadhihirisha umuhimu mkubwa wa kilimo katika jamii yetu.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2023/2024 umelenga kujenga Sekta ya Kilimo endelevu itakayowapa fursa vijana na wanawake kushiriki kwenye kilimo biashara. Lengo ni kutoa fursa za ajira zenye staha na kipato cha uhakika ili kufikia lengo la ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 na kuondoa watu kwenye umasikini na kubaki endelevu kwa miaka 10 kwa kuwekeza kwenye miradi ya muda mrefu kwani uwekezaji kwenye kilimo siyo wa muda mfupi bali matokeo yake ni ya muda mrefu.

**130.** Maeneo makubwa ya uwekezaji ni ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, miundombinu ya uhifadhi, uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamoja, upatikanaji wa pembejeo, utafiti na huduma za ugani. Utekelezaji wa miradi hii, utaimarisha usalama wa chakula wakati wote na kukuza uchumi shirikishi ambao utaboresha maisha ya mkulima na kuleta utajiri kwa Taifa letu.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji huu utachangia upatikanaji wa ajira kwa vijana na wanawake kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 ambayo imeelekeza kutengeneza ajira Milioni nane kwenye sekta zote za uchumi ifikapo mwaka 2025 wakati lengo la Wizara ya Kilimo ni kutengeneza ajira milioni tatu ifikapo mwaka 2030.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji kwenye miradi ya kilimo siyo wa muda mfupi na matokeo yake ni ya muda mrefu. Nimetoa maelezo kutokana na maswali ya mara kwa mara ninayoulizwa na baadhi ya wananchi na viongozi kuwa Ruzuku ya mbolea imepunguzaje bei ya chakula na matokeo ya umwagiliaji ni yapi?.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango huu pia unajikita katika kuhakikisha tunajilisha sisi na kuwalisha wengine kibiashara. Dhamira hii itaongozwa na Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025); Maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kulihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/2022 – 2025/2026); Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013; Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya Mwaka 2010; na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II).

**134.** Aidha, Mpango umezingatia Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs); Mwongozo na Mpango wa Bajeti wa mwaka 2023/2024: na masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, vijana, kutokomeza ajira kwa watoto katika Sekta ya Kilimo, VVU na UKIMWI.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeweka azma ya kujihakikishia usalama wa chakula hususan kujilisha, kunufaika kwa kulisha wengine kibiashara na kuimarisha ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. Ili kuongoza mageuzi ya kilimo na uboreshaji wa maisha ya wakulima yanayokusudiwa, chini ya Mpango wa Agenda 10/30, Wizara inaendelea na azma hiyo kwa kutekeleza vipaumbele vitano (5) ambavyo vitatekelezwa kupitia mikakati 26 kama ifuatavyo;

**i. Kuongeza tija na uzalishaji (Increase Productivity and Production);**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kipaumbele namba moja ni kuongeza tija na uzalishaji ambacho kitatekelezwa kwa kuwekeza kwenye maeneo ya kimkakati yafuatayo:-

a. Utafiti wa mbegu bora;
b. Uzalishaji wa mbegu na miche bora pamoja na usambazaji wa mbegu na miche ya ruzuku;
c. Uwekezaji kwenye huduma za ugani;
d. Kuanza kujenga nyumba za maafisa ugani katika Kata 4,000;
e. Uwekezaji kwenye kupima afya ya udongo na utoaji wa ruzuku ya mbolea na viuatilifu;
f. Uwekezaji kwenye kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji;
g. Uanzishwaji wa vituo Jumuishi vya Kutoa Huduma za Zana za Kilimo (Mechanization centres); na
h. Kuanzisha Kanda saba za Kilimo za Uzalishaji (Tanzania Agriculture Growth Corridor).

**ii. Kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo (Increase decent jobs and enhancing youth and women participation in agriculture sector)**

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipaumbele namba mbili ni kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo ambacho kitatekelezwa kwa kuwekeza kwenye maeneo ya kimkakati yafuatayo:-

a. Kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja (Block farms and Agricultural Parks);
b. Kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo kupitia programu ya Jenga Kesho iliyo Bora;
c. Kuendeleza vituo mahiri vya kusambaza teknolojia; na
d. Kuhamasisha uanzishaji wa kampuni za ugani za vijana.

**iii. Kuimarisha usalama wa chakula na lishe (To improve resilience for food and nutrition security);**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipaumbele cha tatu ni kuimarisha uhimilivu wa usalama wa chakula na lishe ambacho kitatekelezwa kwa kuwekeza kwenye maeneo ya kimkakati yafuatayo:-

a. Uwekezaji kwenye miundombinu ya uhifadhi kuweza kufikia uwezo wa kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030;
b. Kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi hadi kufikia tani 500,000;
c. Kuimarisha na kuanza matumizi ya mfumo wa kidigitali wa Agricultural Stock Dynamic Systems utakaosajili ghala za sekta ya umma, sekta binafsi na Vyama vya Ushirika na kuyapa namba maalum ya utambulisho;
d. Kuratibu Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika - 2023 (Africa's Food Systems Forum) na;
e. Kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini.

**iv. Kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi (Strengthen access to market, agriculture financing and crop exports);**

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipaumbele namba nne ni kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi ambacho kitatekelezwa kwa kuwekeza kwenye maeneo ya kimkakati yafuatayo:-

a. Kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa ajili ya wakulima katika Halmashauri mbalimbali;
b. Kuimarisha uongezaji thamani na uhifadhi pamoja na kuiwezesha Sekta binafsi kwa kuijengea miundombinu ya masoko;
c. Kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi;
d. Kuimarisha upatikanaji wa mitaji (Agricultural finance); na
e. Kuziwezesha maabara za Serikali na Sekta binafsi ziweze kufikia viwango vya uboravinavyotakiwa kimataifa.

**v. Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika (Strengthening Cooperative Development)**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kipaumbele namba tano ni kuimarisha Maendeleo ya Ushirika ambacho kitatekelezwa kwa kuwekeza kwenye maeneo ya kimkakati yafuatayo:-

a. Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika;
b. Kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara na kuvisaidia kupata mitaji;
c. Kuimarisha na kupitia upya mifumo ya upatikanaji wa viongozi wa Vyama vya Ushirika; na
d. Kupitia upya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013.

**i. Kuongeza tija na uzalishaji (Increase Productivity and Production)**

**a. Utafiti wa mbegu bora**

**141.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia TARI imepanga kufanya utafiti wa mbegu aina 10 za mazao ya kimkakati ya nafaka, jamiii ya mikunde na mafuta. Pia, itatafiti na kupendekeza teknolojia mpya 10 za kanuni bora za kilimo katika nyanja za afya ya udongo, magonjwa, wadudu na viuatilifu vya kudhibiti visumbufu vya mimea. Vilevile, TARI itatafiti na kupendekeza teknolojia tano (5) za kuongeza thamani ya mazao ya maharage, miwa, soya, viazi lishe na korosho.

**142.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha upatikanaji wa mbegu na miche bora, TARI itazalisha mbegu za awali tani 450 za mazao ya kipaumbele ya mahindi, alizeti, soya, ufuta, ngano, maharage, kunde, mpunga, mtama, choroko, dengu, shayiri na karanga. Mbegu hizo zina uwezo wa kuzalisha mbegu zilizothibitishwa tani 293,635 ifikapo mwaka 2025.

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kulinda, kutunza, kutafiti na kuzalisha mbegu za asili kwa ajili ya soko maalum, TARI itaendelea kusafisha na kuzalisha mbegu za asili tani 10 za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mbogamboga na itahifadhi vizazi vya mbegu hizo katika vituo vya TARI vya Dakawa, Hombolo, Ifakara na Selian.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, itaendelea kuimarisha vituo vyote vya TARI; kuanza kujenga ghala sita (6) zenye vyumba vya ubaridi katika vituo sita (6) vya TARI zenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,490 za mbegu za awali; na kukamilisha ujenzi wa ghala tano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 2,075 katika vituo vitano (5) vya TARI. Ujenzi huo utakapokamilika TARI itakuwa na uwezo wa kuhifadhi mbegu za awali tani 4,565 zenye uwezo wa kuzalisha mbegu za msingi tani 45,650 zenye uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 1,369,500 ya mbegu zilizothibitishwa.

**145.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza uzalishaji wa miche bora na kudhibiti visumbufu vya mazao, Wizara kupitia TARI itaanza kujenga maabara mpya ya *tissue culture* katika kituo cha TARI Maruku kwa ajili ya kuzalisha miche bora ya migomba na kujenga maabara ya utambuzi na udhibiti wa visumbufu vya zao la korosho katika kituo cha TARI Naliendele. Pia, TARI itakamilisha ukarabati wa maabara ya bioteknolojia ya TARI Mikocheni na ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya mkonge kwa njia ya chupa (tissue culture) katika kituo cha TARI Mlingano.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuzuia uvamizi wa mashamba ya utafiti, Wizara kupitia TARI itaendelea kujenga uzio katika kituo cha TARI Uyole (hekta 1,042) na itaanza ujenzi wa uzio wa mashamba katika vituo vingine 16 vya TARI. Vilevile, TARI itaanza ujenzi wa uzio wa mashamba katika vituo vidogo 18.

**b. Uzalishaji wa mbegu na miche bora pamoja na usambazaji wa mbegu na miche ya ruzuku.**

**147.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora nchini ambapo katika mwaka 2023/2024, itaiwezesha ASA kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kufikia hekta 3,304.8 mwaka 2025 na uzio katika mashamba yote ya mbegu ya ASA.

**148.** ***Mheshimiwa Spika***, ASA itaendelea kujenga miundombinu ya kuhifadhia mbegu (ghala) katika mashamba ya Mbozi, Namtumbo, Msungura na Kilangali. Aidha, itanunua na kufunga mitambo miwili (2) ya kuchakata mbegu katika mashamba ya mbegu ya Mbozi na Namtumbo.

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, ASA itaendelea kufungua maeneo mapya katika mashamba ya Mwele, Luhafwe, Msimba, Kilimi, Namtumbo na Mbozi; itazalisha tani 1,500 za mbegu za ngano na tani 400 za mbegu za soya; na miche ya parachichi 450,000 na kusambaza kwa mpango wa ruzuku.

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kusambaza tani 5,000 za mbegu bora za alizeti na kufikia lengo la tani 15,000 mwaka 2025 na mbegu za ngano kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. Aidha, Wizara kupitia TARI kwa kushirikiana wadau mbalimbali itazalisha miche/vikonyo/pingili milioni 37.5 na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. ***(Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 109 hadi 127 wa kitabu cha hotuba yangu***

**c. Uwekezaji kwenye huduma za ugani**

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, itaendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kununua magari 55 kwa ajili ya maafisa kilimo na Makatibu Tawala Wasaidizi Mkoa wanaoshughulika na kilimo, visanduku vya ugani 4,000, sare 4,000, *soil scanner* 45 na vishikwambi 1,500 na kusambaza kwa maafisa ugani. Aidha, Wizara itafufua na kukarabati Vituo vya Rasilimali za Kilimo (WARCs) na kununua magari matatu (3) ya maabara inayotembea kwa ajili ya kutoa huduma za upimaji wa afya ya udongo na kukamilisha mfumo wa kuhifadhi taarifa za afya ya udongo wa nchi yetu badala ya kuendelea na utaratibu wa kupimiwa afya ya udongo na kampuni binafsi na taarifa hizo kubaki kwenye kampuni hizo.

**152.** Wizara itaendelea kuimarisha Mfumo wa M-Kilimo na matumizi ya Kituo cha Huduma kwa Wateja ili kuwawezesha wadau kupata huduma kupitia ujumbe mfupi, mitandao ya kijamii na barua pepe, simu za mkononi; kuwezesha na kusimamia matumizi sahihi ya vitendea kazi zikiwemo pikipiki pamoja na magari.

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itaimarisha mfumo wa M – Kilimo na kuandaa *Mobile Application* ambayo itawezesha mawasiliano kati maafisa ugani na wadau wa kilimo. Kupitia *Application* hiyo, maafisa ugani na wakulima watakubaliana malipo kulingana na huduma itakayotolewa na wataalam. Aidha, huduma hiyo itasaidia kuongeza ajira na upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima kwa urahisi.

**Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa ya Nanenane**

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kilele cha Maonesho ya Kilimo (Nanenane) mwaka 2022, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza kuanzisha Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo (Tanzania International Agriculture Trade Show) badala ya kutumia utaratibu uliozoeleka. Aidha, Mhe. Rais alielekeza mabadiliko hayo yaanzie na ujenzi wa miundombinu katika kiwanja cha Maonesho cha John Mwakangale (Mbeya) kilichopo katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini ambapo kuna uzalishaji mkubwa wa mazao.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maelekezo ya Mhe. Rais ambayo ni fursa ya kutangaza kilimo na bidhaa zake kimataifa, Wizara katika mwaka 2023/2024 imepanga kuimarisha viwanja viwili (2) vya maonesho ya kilimo vya John Mwakangale (Mbeya) na Nzuguni (Dodoma) kuwa na hadhi ya Maonesho ya Kilimo ya Kimataifa. Mpango huo utahusisha usanifu ili kukarabati na kujenga miundombinu ya viwanja hivyo na kujenga *Tanzania Agricultural Museum*.

**Mafunzo ya Kilimo**

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024, imepanga kudahili wanafunzi 3,000 katika ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada za kilimo. Kati ya hao, wanafunzi 2,500 watagharamiwa mafunzo kwa vitendo katika Halmashauri na Wilaya ili kuwajengea uzoefu wa kufanya kazi shambani na kuwawezesha kuajiriwa na kujiajiri. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia inaendelea kuangalia uwezekano wa wanafunzi hao kufanya mafunzo kwa vitendo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja. Lengo ni kuimarisha ujuzi kwa vitendo na utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima.

**157.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo itatoa mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana 4,000 kupitia programu ya BBT. Lengo ni kuwawezesha vijana kupata maarifa na ujuzi wa namna bora ya kuanzisha na kuendesha kilimo biashara hapa nchini kupitia Mashamba Makubwa ya Pamoja au mashamba binafsi. Mafunzo hayo yatatolewa kwa kuzingatia ikolojia ya kilimo.

**158.** Pia, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo na Vituo vya Mafunzo kwa Wakulima kwa kukarabati na kujenga miundombinu ya Vyuo sita (6) ambavyo ni MATI Uyole, KATRIN, Inyala, Igurusi, Mtwara, Mlingano pamoja na Vituo vinne (4) vya Mafunzo kwa wakulima vya Bihawana, Mkindo, Themi na Ichenga.

**159.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kushirikiana na Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (Sustainable Agriculture Tanzania





- SAT) kupitia Mradi wa Kuwezesha Utekelezaji wa Mitaala Katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo Awamu ya Pili kutoa mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya kufundishia moduli za Kilimo Hai, Jinsia katika Kilimo na Utunzaji wa Mazingira.

**d. Kuanza kujenga nyumba za Maafisa ugani katika Kata 4,000**

160. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024 itaanza kujenga nyumba za Maafisa ugani katika Kata 4,000 ili kusogeza huduma za ugani karibu na wakulima na kurahisisha utoaji wa ushauri wa kilimo wa kitalaam. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta itaanza kuangalia uwezekano wa maafisa ugani ngazi ya Kata kukusanya na kuingiza takwimu za kilimo kwenye Mfumo wa Takwimu za Kilimo (Agriculture Routine Data System – ARDS). (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 127 hadi 132 wa kitabu cha hotuba yangu)***

**e. Uwekezaji kwenye kupima afya ya udongo na utoaji wa ruzuku ya mbolea na viuatilifu**

**Afya ya udongo**

161. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutathmini afya ya udongo nchi nzima, TARI itakamilisha kukusanya na kupima sampuli za udongo 12,000 kutoka katika mikoa nane (8) ili kuandaa ramani inayoonesha afya ya udongo kwa kila Mkoa. Aidha, imepanga kupima afya ya udongo katika skimu tano (5) kwa ajili ya kilimo cha mpunga pamoja na shamba la Magereza lililopo Mkoa wa Simiyu kwa ajili ya kilimo cha alizeti. Pia, TARI itaandaa ramani zinazoonesha maeneo yanayolimwa alizeti na ngano katika ngazi za Wilaya na Kata na kuyatambua rasmi maeneo yote yanayofaa kwa kilimo cha zao la ngano na kushauri matumizi sahihi ya mbolea na teknolojia za umwagiliaji.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kupima afya ya udongo katika mashamba mapya 30 yenye ukubwa wa hekta 200,000 za kilimo katika mikoa mitano (5).

**Ruzuku ya Mbolea na Viuatilifu**

163. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, kupitia TFRA itaendelea kuratibu upatikanaji wa mbolea nchini kwa kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima hadi mwaka 2025/2026 ili kuongeza matumizi ya mbolea (per capita consumption) kutoka kilo 19 kwa hekta hadi angalau kilo 50 kwa hekta, kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza upatikanaji.

164. Wizara kupitia TFRA itaendelea na usajili wa wakulima katika mfumo wa kidigitali ili kulifanya taifa letu kuwa na uhakika wa takwimu na taarifa za wakulima. Vilevile, Wizara kupitia TFRA itaendelea kuratibu uingizwaji wa tani 750,000 za mbolea nchini.

165. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaiwezesha Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) Shilingi Bilioni 40 kama mtaji na kuufanya mtaji wake kuwa Shilingi Bilioni 46 kwa ajili ya kununua mbolea na kununua ardhi ya kujenga kiwanda cha kuchanganya mbolea (Blending Facilities) kwa kushirikiana na Sekta binafsi. Hatua hii inalenga kupunguza utegemezi wa mbolea kutoka nje ya nchi na kuimarisha upatikanaji wa mbolea kulingana na afya ya udongo ya eneo husika.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia TPHPA itanunua viuatilifu lita 101,000 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya mazao na mimea mbalimbali ikiwemo parachichi na machungwa. Aidha, Wizara itavijengea uwezo vituo vya kudhibiti visumbufu vya mazao na mimea ikiwemo KILIMO ANGA na kituo cha kudhibiti panya. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 132 hadi 134 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**f. Uwekezaji kwenye kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji**

167. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kuongeza eneo la umwagiliaji lenye jumla ya hekta 256,185.46 kwa kukamilisha ujenzi wa skimu, kukarabati skimu zilizochakaa, kujenga skimu mpya na mabwawa 100 kwa ajili ya umwagiliaji.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Tume imepanga kukamilisha ujenzi wa miradi 25 na ukarabati wa skimu 30 zenye jumla ya hekta 95,005 pamoja na mabwawa 14 yenye mita za ujazo 131,535,000; na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 42 na mabonde ya kimkakati 22 ambayo utekelezaji wake ulianza mwaka 2022/2023. Aidha, Tume imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa mapya 100 na kuanza ujenzi wa mabwawa hayo yenye takribani mita za ujazo 936,535,700; kuanza ujenzi na kukarabati skimu 59 zenye jumla ya hekta 143,482.

169. ***Mheshimiwa Spika***, Tume imepanga kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde 22 ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 306,361. Baadhi ya mabonde hayo ni eneo la ziwa Victoria, Tanganyika, Rufiji, Manonga - Wembere, Bugwema, Lukuledi, Songwe na Ruvuma. Vilevile, Tume imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Mashamba Makubwa ya Pamoja na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba hayo yenye jumla ya ekari 264,841.5 kupitia programu ya BBT katika Mikoa ya Kigoma, Mbeya, Kagera, Singida, Njombe na Dodoma.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu mpya 240 zenye ukubwa wa hekta 268,436 na mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 255 za kukarabati zenye ukubwa wa hekta 290,095. Ujenzi na ukarabati wa skimu hizo utafanyika katika mwaka 2024/2025.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Vyama vya Umwagiliaji, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika itatoa mafunzo kwa Vyama vya Umwagiliaji 430 vilivyosajiliwa ili kusimamia uendeshaji na utunzaji wa skimu za umwagiliaji; itaanzisha na kusajili Vyama vya Umwagiliaji 200. Tume itawezesha matumizi ya mfumo wa kielekroniki wa ukusanyaji wa ada ya huduma za umwagiliaji katika skimu na kusimamia ukusanyaji wa ada ya huduma za umwagiliaji katika skimu 600.

172. Vilevile, Tume itanunua magari 20 na kuyakabidhi katika ofisi za umwagiliaji za Wilaya pamoja na kufungua ofisi za Wilaya 25 zilizobaki ili kuimarisha usimamizi wa shughuli za umwagiliaji. Pia, Tume itaimarisha ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya umwagiliaji kwa kuweka mfumo wa kielektroniki.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024 na kuendelea Tume ya Taifa ya umwagiliaji itaacha kutumia mifereji ya wazi (open channels) na kutumia mfumo wa mabomba ambao utaongeza ufanisi kwa kupunguza upotevu wa maji na kulinda uharibifu wa miundombinu. Vilevile, Tume itaweka utaratibu wa mita ili kutambua matumizi halisi ya maji kwenye skimu ili kuongeza ukusanyaji wa ada za umwagilaiji na usimamizi. Wakulima ambao hawatakuwa tayari kulipia huduma hiyo, Tume kwa kushirikiana na Mamlaka zinazosimamia rasilimali maji itasitisha huduma za umwagiliaji kwa kufunga maji.

"***Haiwezekani Serikali inawekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya umwagilaji kwa gharama kubwa na kukabidhi miundombinu hiyo kwa wakulima na pale ambapo banio linakatika Serikali inaombwa kuja kurekebisha wakati fedha za kurekebisha Skimu zilikusanywa na watu wachache***"

174. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imedhamiria kuanza kujenga uzio katika skimu zote za umwagiliaji nchini, kuweka ulinzi na kuimarisha usimamizi wa skimu hizo kupitia mameneja wa skimu ili kuongeza tija ya uzalishaji. Ni lazima fedha zinazowekezwa katika ujenzi wa skimu za umwagiliaji zirudi ili ziweze kuendelea kuwekezwa katika ujenzi wa miundombinu mingine na kuhakikisha uendelevu wa miundombinu ya umwagiliaji.

175. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua kuwa wakulima wengi wanauwezo mdogo na gharama za uwekezaji kwenye miundombinu ya umwagiliaji ni kubwa, Wizara kupitia Tume itachimba visima kwa ajili ya wakulima 150 kwa kila Halmashauri ambao ni sawa na jumla ya wakulima 27,600 katika Halmashauri 184. Wakulima hao watapatiwa vifaa vya umwagiliaji (irrigation kits) kwa ajili ya kuhudumia ekari 2.5, tenki la maji la lita 5,000 na kuwawekea mfumo wa sola ambapo jumla ya ekari 69,000 zitaendelezwa kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka, mbogamboga na matunda. Katika kufanikisha utekelezaji wa programu hii, Wizara itaweka vigezo vya kupima utekelezaji, usimamizi, utoaji wa taarifa sahihi na usajili wa wakulima kwa kila Halmashauri. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 134 hadi 138 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**g. Uanzishwaji wa vituo jumuishi vya kutoa huduma za zana za kilimo (Mechanization centres)**

176. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara itaanzisha vituo vitatu (3) vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwenye mashamba makubwa ya pamoja yatakayoanzishwa kupitia Programu ya BBT. Vilevile, itajenga majengo matatu (3) kwa ajili ya kuhifadhi na kuhudumia zana za kilimo kwenye mashamba hayo.

177. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itawatambua wasindikaji wadogo na wa kati 50 wa zao la alizeti na zabibu katika mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara na kuwapatia mafunzo kuhusu usimamizi na utunzaji wa mitambo ya usindikaji. Kadhalika, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi bora ya zana za kilimo katika mnyororo wa uzalishaji kwa kutoa mafunzo kwa watoa huduma ya zana za kilimo kwenye mashamba makubwa ya pamoja yatakazoanzishwa kupitia Programu ya BBT katika mikoa ya Dodoma, Kagera, Kigoma, Njombe, Shinyanga, Singida, Pwani na Mbeya.

**h. Kuanzisha kanda saba za kilimo na uzalishaji (Tanzania Agriculture Growth Corridors)**

178. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT) imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kilimo katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini kwa kuzingatia ikolojia ya kilimo ya mazao husika. Utekelezaji wa miradi katika kipindi chote kwenye ukanda huo ulijikita kuimarisha tija katika mnyororo wa thamani. Hatua hizi zimesaidia kuimarisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima, matumizi ya teknolojia na upatikanaji wa mitaji.

179. Vilevile, SAGCOT imewezesha matumizi ya teknolojia bora za kilimo kwenye eneo la hekta 284,098, wakulima 782,452 wameajiriwa katika mnyororo wa thamani wa mazao mbalimbali na kuongeza kipato kwa wakulima cha Dola za Marekani Milioni 137.

180. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini (SAGCOT), Wizara imepanga kuanzisha Kanda nyingine saba za uzalishaji (Tanzania Agriculture Growth Corridors) nchini. Lengo ni kuongeza uzalishaji na tija, kuimarisha masoko ya mazao ndani na nje ya nchi, kuongeza thamani mazao na kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, mitaji na kuondoa utamaduni wa kutawanya mazao kila kona ya nchi bila kuzingatia msingi imara wa kibiashara. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 138 hadi 140 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**Uzalishaji wa Mazao**

181. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Kilimo katika mwaka 2023/2024 itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuongeza uzalishaji na tija hususani mazao asilia ya biashara, chakula, mazao yenye uhitaji mkubwa yanayoagizwa kutoka nje ya nchi na mazao ya bustani.

**Mazao Asilia ya Biashara**

182. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ya korosho, pamba, tumbaku, kahawa, chai, sukari, mkonge na pareto unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 951,727.77 mwaka 2022/2023 hadi tani 1,578,500 mwaka 2023/2024. Aidha, Bodi ya korosho kwa kushirikiana na wadau itachimba visima vya maji 20 katika maeneo yenye changamoto ya maji ili kuwawezesha wakulima katika shughuli za upuliziaji wa viuatilifu na umwagiliaji. Pia, Bodi ya tumbaku itawezesha uchimbaji wa visima vitano (5) kwa ajili ya wakulima wa zao la tumbaku.

183. Kadhalika, Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania katika mwaka 2023/2024 kwa kushirikiana na Chama cha Wazalishaji wa Pamba Tanzania (Tanzania Cotton Association - TCA) itanunua trekta 100 kwa ajili ya kuanzisha vituo vya kutoa huduma kwa wakulima. Vilevile, Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania itatumia Shilingi Bilioni 5 kwa ajili ya umwagiliaji na kuwezesha wakulima wa zao la pamba.

**Mazao ya chakula**

184. ***Mheshimiwa Spika***, katika msimu wa 2021/2022 uzalishaji wa mazao ya chakula ulikuwa tani 17,148,290, na katika msimu wa 2022/2023 matarajio ni kuzalisha tani 18,700,000. Kati ya hizo, mahindi ni tani 8,500,000 na mchele tani 2,200,000 na mazao yasiyo nafaka ni tani 8,000,000.

185. Wizara itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya chakula ikiwemo mahindi mpunga, muhogo, mtama, mawele na mazao jamii ya mikunde ili kuimarisha upatikanaji wa chakula na biashara ya mazao hayo. Uzalishaji wa mazao ya mahindi, mpunga na muhogo unatarajiwa kufikia tani 7,219,000, 5,011,000 na 10,000,000, mtawalia.

**Uzalishaji wa mazao yenye mahitaji makubwa**

186. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya miwa, ngano na mazao ya mbegu za mafuta ili kuimarisha upatikanaji wake nchini na kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

**Zao la Miwa na Uzalishaji wa sukari**

187. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 uzalishaji wa miwa ulikuwa tani 3,757,255 ambazo zilizalisha sukari tani 379,280; mwaka 2022/2023 uzalishaji wa miwa ulikuwa tani 4,405,350.61 ambazo zilizalisha sukari tani 456,019.73; na uzalishaji wa miwa katika mwaka 2023/2024 unatarajiwa kufikia takribani tani 4,500,000 ambazo zitazalisha tani 465,000 za sukari.

188. Hii itasaidia kupunguza nakisi ya sukari kutoka nje kwa kiwango kilichopo sasa cha tani 30,000 ili kufikia mwaka 2025 kusiwepo uagizaji wa sukari kutoka nje ambapo uzalishaji wa miwa unatarajiwa kufikia tani 7,000,000 ambazo zitazalisha tani 700,000 za sukari. Ili kufikia lengo hilo Wizara imeanza kuchukua hatua stahiki kuanzia mwaka 2022/2023 kama ifuatavyo; kukamilisha upembuzi yakinifu wa mabwawa ya Mandela na Wembele; na kuongeza upatikanaji wa mbegu bora ambapo Bodi ya Sukari Tanzania kwa kushirikiana na TARI itaanzisha kitalu cha hekta 400 katika bonde la Kilombero. Aidha, tumemuomba Mhe. Rais kwa ajili ya kuweka jiwe la msingi.

189. Vilevile, Bodi itaimarisha usimamizi wa matumizi ya kanuni bora za kilimo cha miwa, uvunaji na uchakataji wa miwa. Aidha, Wizara imepanga kuanza kilimo cha umwagiliaji katika zao la miwa kwa wakulima wadogo wa Kilombero. Ili kupunguza gharama za uingizaji wa sukari (Import bill) Wizara itafanya majadiliano na viwanda vyote vya sukari kujadili namna ya kuzalisha sukari ya viwandani na kutumia mfumo wa sukari ya matumizi ya kawaida ili kulinda viwanda vya ndani.

**Zao la Alizeti**

190. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Serikali inawalinda wakulima wa mazao ya mafuta ya kula nchini, Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) imewasilisha mapendekezo Wizara ya Fedha na Mipango kurudisha kodi kwenye mafuta yaliyosafishwa kutoka nje (refined oil) kuwa asilimia 35. Hii ni kufuatia ukweli kwamba, punguzo la kikodi kutoka asilimia 35 hadi asilimia 25 lililotolewa na Serikali katika mwaka 2022/2023 liliathiri soko la mazao ya mafuta ya kula nchini.

191. Hivyo, katika kuwalinda wakulima wa mazao ya mafuta nchini, Wizara ya Kilimo inapendekeza Serikali irudishe kodi ya asilimia 35 kwa mafuta ya kula yaliyosafishwa kutoka nje ya nchi. Aidha, mtu au kampuni yoyote isiyojihusisha na uchakataji wa mazao ya mafuta yanayozalishwa hapa nchini, haitaruhusiwa kuingiza mafuta ya kula kutoka nje na COPRA itasimamia kazi hii.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024, kupitia TARI kwa kushirikiana na wadau ikiwemo IFAD na AGRA itazalisha mbegu za awali za alizeti tani 186 zenye uwezo wa kuzalisha mbegu zilizothibitishwa tani 7,440 na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya TARI Ilonga yenye ukubwa wa hekta 15. Aidha, TARI kwa kushirikiana na AGRA na AMDT itawezesha kampuni za kitanzania za uzalishaji wa mbegu za alizeti ili kuongeza uzalishaji.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kusambaza mbegu za alizeti tani 5,000 kwa mpango wa ruzuku katika mwaka 2023/2024 na tani 15,000 katika mwaka 2025/2026. Usambazaji wa mbegu tani 5,000 utawezesha uzalishaji wa alizeti kufikia takribani tani 1,000,000 ambazo zitazalisha takribani tani 300,000 za mafuta ya kula.

**Zao la Ngano**

194. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kujitosheleza na zao la ngano, Serikali inaendelea kuwekeza fedha ili kuondoa tatizo la uagizaji wa ngano kutoka nje ya nchi ambapo Wizara imejielekeza kutekeleza mikakati ifuatayo:-

i. TARI itazalisha mbegu za awali tani 2,500 ambazo zitazalisha mbegu zilizothibitishwa tani 50,000 kwa kushirikiana na Sekta binafsi ifikapo mwaka 2025/2026;
ii. Kuongeza uzalishaji wa ngano kutoka tani 61,968 hadi kufikia tani 150,000 mwaka 2023/2024, tani 250,000 mwaka 2024/2025 na tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2025/2026;
iii. Kuendelea kutambua na kupima maeneo yote yanayofaa kwa kilimo cha ngano nchini; na
iv. Kuingia mikataba ya ununuzi wa ngano (Memorandum of Understanding – MoU) na kampuni kubwa zinazoagiza ngano nje ya nchi ili kununua ngano yote inayozalishwa na wakulima ndani ya nchi kwa uwiano wa *market share*. Hivyo, kupitia mikataba hiyo waagizaji wa ngano nje ya nchi wataagiza ngano ya kutosheleza mahitaji yao baada ya kukidhi sharti la kununua ngano yote nchini kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani ili ifikapo mwaka 2025/2026 nchi yetu ijitosheleze kwa mahitaji ya ngano na kuzuia uingizaji wa ngano kutoka nje ya nchi. Serikali tusipofanya maamuzi magumu katika zao hili, tutaendelea kuwa wategemezi wa ngano kutoka nchi zingine.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na jitihada za Serikali kutaka kuingia makubaliano na waagizaji wa ngano, kumejitokeza baadhi ya waagizaji hao kugomea hatua hiyo. Kwakua kama nchi tunawekeza fedha za umma katika kuhakikisha tunazalisha ngano kukidhi mahitaji ya ndani, ninaomba nitumie Bunge lako Tukufu kuutangazia umma kwamba Watanzania hawatakufa njaa kwa kukosa ngano na hatuwezi kuendelea kuwa soko la nchi nyingine na niwahakikishie kuwa hawataingiza hata kilo moja ya ngano ifikapo mwaka 2025/2026.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kuwaambia wamiliki wa kampuni zinazochakata ngano nchini kuwa, wasiposaini mkataba wa makubaliano na wakulima wa ngano (MoU), mwenye mamlaka ya kutoa vibali vya kuingiza ngano ni Waziri wa Kilimo hivyo viwanda vyao vitakosa malighafi ya ngano na vitabaki chuma chakavu,ni lazima tumlinde mkulima.

***"Ninaomba niliambie Bunge lako Tukufu kuwa mazao mengi ya kilimo yamekufa kwa kuwa wakulima hawakulindwa na kufungulia milango ya kuagiza mazao kutoka nje bila sababu"***

**Mazao ya Bustani (Horticulture)**

**Zao la Parachichi**

197. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya Mhe. Rais kufungua masoko ya mazao ya kilimo nje ya nchi, Serikali ilipanga kukamilisha mambo mawili; kwanza kuanzisha Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu ambayo tayari imeanza kutekeleza majukumu yake; na pili kuweka utaratibu wa kusimamia tasnia ya parachichi ambapo tayari Mkakati wa Kuendeleza Tasnia ya Mazao ya Bustani (horticulture) mwaka 2021-2031 pamoja na Mwongozo wa Kuendeleza zao la Parachichi umeandaliwa. Hatua hizo zimewezesha kuongeza mauzo ya nje ya zao la parachichi kutoka tani 9,978 mwaka 2020 hadi tani 29,031 mwaka 2022.

198. ***Msheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024, itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa aina za parachichi zinazouzwa nje ya nchi (Exportable Varieties) kutoka wastani wa tani 29,031 zenye thamani ya Dola za Marekani **Milioni 52** mwaka 2022/2023 hadi tani 50,000 zenye thamani ya takribani Dola za Marekani **Milioni 90** ifikapo mwaka 2025. Vilevile, Wizara kupitia TARI kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya pamoja na Sekta Binafsi itazalisha miche 10,000,000 ya parachichi kwa kuendeleza vitalu na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji.

**Zao la Zabibu**

199. ***Mheshimiwa Spika***, Zao la zabibu linalimwa katika mkoa wa Dodoma ambapo katika mwaka 2021/2022 uzalishaji wa zabibu ni tani 15,513 na mahitaji ya mchuzi ni lita Milioni 15 na uzalishaji kwa sasa ni lita Milioni 5. Changamoto ya soko la zabibu inatokana na ukosefu wa miundombinu ya kuhifadhi mchuzi wa zabibu. Katika kuhakikisha uzalishaji wa zabibu unaongezeka Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:- hatua ya kwanza ni kuwanunulia wazalishaji matenki ya kuhifadhi mchuzi wa zabibu; hatua ya pili Serikali itaboresha mfumo wa zamani wa mashamba kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya zabibu; hatua ya tatu ni kuimarisha usimamizi ikiwemo ujenzi wa uzio katika shamba la zabibu Hombolo; na kuweka utaratibu wa kuchangia gharama za umwagiliaji.

200. Mikakati mingine ni pamoja na kuhamasisha Sekta binafsi kuzalisha juisi kwa kutumia zabibu ya ndani ambapo Kampuni ya Jambo imeanza uzalishaji wa juisi. Vilevile, Wizara itaendeleza shamba na kiwanda cha zabibu Chinangali na kukabidhi kwa Sekta binafsi kukiendesha. Pia, Wizara kupitia TARI itazalisha na kusambaza miche 500,000 ya zabibu kwa wakulima ambayo itatosha kupandwa katika hekta 192.7. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 140 hadi 158 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**v. Kuongeza Ajira zenye staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo (Increase decent jobs and enhancing youth and women participation in agriculture sector)**

**a. Kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja (Block farms and Agricultural Parks)**

201. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Wizara itaendelea kuwawezesha vijana na wanawake kwa kuwajengea uwezo na kuwapatia mitaji na maeneo ya uzalishaji yenye miundombinu ya umwagiliaji. Aidha, Wizara itahamasisha uanzishwaji wa Mashamba Makubwa ya Pamoja kwa ajili ya kuwawezesha vijana kushiriki katika kilimo na kuleta sekta binafsi ambao watashiriki pamoja na vijana hao katika mashamba hayo ili kununua mazao, kuongeza thamani na ajira.

202. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeweka lengo kufikia mwaka 2025 kuwa na jumla ya hekta 1,000,000 ambazo ni sawa na ekari 2,500,000 kwa ajili ya kuwapatia vijana na wanawake. Aidha, gharama za usafishaji, upimaji wa shamba na afya ya udongo, usawazishaji wa mashamba na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa hekta moja ni wastani wa Shilingi 16,800,000. Katika kutekeleza lengo hilo, Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi na Taasisi za Fedha itawekeza Shilingi Trilioni 16.8 ifikapo mwaka 2030. Eneo hili likikamilika la hekta 1,000,000 litatengeneza ajira 1,500,000.

203. ***Mheshimiwa Spika***, eneo hili la hekta 1,000,000 litakuwa na miundombinu ya uzalishaji kwa teknolojia za kisasa ambalo litatumika kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka na bustani. Eneo hili litaongeza uzalishaji wa mazao ya nafaka kwa tani 3,500,000 na kuwawezesha wakulima kupata kipato cha wastani wa Shilingi Trilioni 1.75 ambayo ni sawa na Shilingi 7,000,000 kwa kila mkulima kwa uzalishaji mmoja.

204. Pia, Wizara itatambua na kuainisha mashamba mapya 30 yenye ukubwa wa hekta 200,000 za kilimo katika mikoa yote nchini kwa kushirikiana na Halmashauri husika.

**b. Kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo kupitia programu ya Jenga Kesho iliyo Bora**

205. ***Mheshimiwa Spika***, BBT ni programu ya miaka 8 kuanzia mwaka 2022 - 2030 na itatekelezwa nchi nzima kwa ushirikiano kati ya Serikali, Washirika wa Maendeleo na Sekta binafsi. BBT ni miongoni mwa programu muhimu katika Sekta ya Kilimo ili kufikia malengo ya ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 (Ajenda 10/30).

206. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha ushiriki wa Sekta binafsi kwenye utoaji wa huduma mbalimbali kwenye mashamba makubwa ya pamoja kwa ajili ya vijana na mashamba ya mbegu. Huduma hizo ni pamoja na ukodishaji wa zana za kilimo, utoaji wa huduma za ugani, pembejeo za kilimo, mikopo, upangaji wa madaraja, usafirishaji, usindikaji, ufungashaji na masoko. Huduma hizo zitatolewa kwenye maeneo maalum ambapo zitajengwa *pack houses* kwa kushirikiana na Sekta binafsi.

**c. Kuendeleza Vituo Mahiri vya kusambaza teknolojia**

207. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha vijana na wanawake wanapata elimu ya teknolojia, ubunifu na mbinu za kilimo bora kwa mwaka mzima, Wizara kupitia TARI itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika vituo nane (8) mahiri vya usambazaji wa teknolojia katika viwanja vya maonesha ya wakulima (Nanenane) vya Nyakabindi, John Mwakangale, Nzuguni, Ngongo, Fatma Mwasa, Themi, Mwl. J. K. Nyerere na Nyamhongolo.

**d. Kuhamasisha uanzishwaji wa Kampuni za Ugani za Vijana**

208. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024 Wizara itapitia upya miongozo ya ugani iliyopo na kuandaa mfumo wa kisheria utakaoruhusu uanzishwaji wa kampuni za ugani za vijana. Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza upatikanaji wa ajira kwa wahitimu wa kozi mbalimbali za kilimo nchini na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za ugani katika Sekta ya Kilimo. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 158 hadi 162 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**vi. Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe (To improve resilience for Food and Nutrition Security)**

**a. Uwekezaji kwenye miundombinu ya uhifadhi kuweza kufikia uwezo wa kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030**

209. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024 itaendelea kuimarisha uwezo wa nchi wa kuhifadhi mazao ya chakula kwa kukamilisha ujenzi wa ghala 38 zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 33,000 katika Mikoa ya Ruvuma (28), Tabora (6), Geita (1) na Shinyanga (3). Vilevile, Wizara kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi unaotekelezwa na NFRA itakamilisha ujenzi wa ghala na vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 165,000 katika kanda za Songea, Mbozi, Makambako, Dodoma na Shinyanga.

210. Wizara itaandaa Mwongozo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Ghala ili kuhakikisha ghala zilizojengwa zinatumika na kuendeshwa kwa tija. Kadhalika, ghala zinazojengwa na Wizara kupitia mradi wa TANIPAC zitasimamiwa na NFRA.

211. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara itafanya tathmini ya kuangalia uwezekano wa kuiongezea NFRA uwezo wa kuhifadhi chakula. Tathmini hiyo itahusisha kutambua ghala zote zilizojengwa na Serikali na namna bora ya kushirikisha Sekta binafsi katika uhifadhi wa chakula ili kuimarisha usalama wa chakula nchini. Lengo la tathmini hiyo ni kubaini uwezo wa Sekta ya umma na Sekta binafsi wa kuhifadhi chakula ili kukidhi mahitaji ya chakula ya ndani ya nchi na kulisha wengine kibiashara.

**b. Kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi hadi kufikia tani 500,000**

212. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usalama wa chakula, Wizara kupitia NFRA itanunua na kuhifadhi tani 400,000 za nafaka. Kati ya hizo, mahindi ni tani 200,000 mpunga tani 200,000. Pia, Wizara itachimba visima virefu (boreholes) vitano (5) vya maji katika ghala za Mbogokomtonga, Kigugu, Mvumi, Msolwa Ujamaa na Njage katika Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya kuwezesha uendeshaji.





**c. Kuimarisha na kuanza matumizi ya mfumo wa *Agricultural Stock Dynamics Systems***

**213. *Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, itaimarisha na kuanza matumizi ya mfumo wa kidigitali (Agricultural Stock Dynamics Systems) kwa ajili ya kufuatilia kiasi cha mazao ya kilimo kilichohifadhiwa katika ghala hapa nchini. Mfumo huo utasajili ghala za sekta ya umma, sekta binafsi, vyama vya ushirika na masoko kwa kuyapa namba maalumu ya utambulisho. Mfumo huu utawezesha shughuli za biashara ya kilimo na kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi za chakula kwa ajili ya usalama wa chakula nchini.

**d. Kuratibu Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika - 2023**

**214. *Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Kilimo nchini, itaendelea na maandalizi na kushiriki Kilele cha Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika 2023 (Africa's Food Systems Forum) utakaofanyika tarehe 05 hadi 08 Septemba, 2023 katika Ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere Dar es Salaam.

**215.** Mkutano huo umelenga kuleta matokeo muhimu katika kuendeleza mifumo ya chakula na kilimo nchini na barani Afrika. Matokeo yanayotarajiwa ni pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika Sekta ya kilimo nchini, kukuza utalii, kuimarika kwa biashara ya mazao ya kilimo na teknolojia.

**e. Kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kukabiliana na Matatizo ya Lishe nchini**

**216. *Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Lishe katika Kilimo (Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan – NSAAP) ili kuchangia kupunguza matatizo ya lishe nchini ikiwemo udumavu, ukondefu na upungufu wa wekundu wa damu. Katika mwaka 2023/2024, Wizara itahamasisha wakulima kuzalisha na kutumia mazao yaliyoongezwa virutubishi kibaolojia ili kukabiliana na changamoto ya lishe duni nchini. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 162 hadi 166 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**vii. Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Mauzo ya Mazao nje ya Nchi (Strengthen access to market, agriculture financing and crop exports)**

**a. Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi**

**Ujenzi wa Masoko ya Kimkakati**

**217. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Wizara itaendelea na ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati yaliyokuwa chini ya mradi wa DASIP yaliyopo katika Halmashauri za Kahama MC (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo), na Tarime (Sirari).

**Ujenzi wa Vituo vya Masoko (Market sheds)**

**218. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024 imepanga kuainisha maeneo na kujenga vituo vitatu (3) vya masoko ya kilimo (market sheds) katika maeneo ya mipakani. Vituo hivyo vitawezesha wakulima kukusanya na kuuza mazao yao sehemu rasmi inayotambulika na mamlaka husika.

**b. Kuimarisha uongezaji thamani na uhifadhi pamoja na kuiwezesha Sekta binafsi kwa kuijengea miundombinu ya wezeshi**

**219. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia mradi wa TANIPAC itakamilisha ujenzi wa Kituo Mahiri cha Usimamizi wa Mazao Baada ya Kuvuna (Mtanana – Kongwa) na Maabara Kuu ya Kilimo Jijini Dodoma. Pia, Wizara itaendelea na ujenzi wa Kituo Jumuishi cha kukusanya, kuchambua, kupanga madaraja, kufungasha na kusafirisha mazao ya bustani katika mikoa ya Iringa, Kilimanjaro na Dar es Salaam. Aidha, Wizara itawezesha ujenzi wa kiwanda na kusimika mitambo ya kusindika zabibu ghafi katika Halmashauri ya Jiji – Dodoma.

**220. *Mheshimiwa Spika***, ili kujenga Sekta binafsi imara na masoko ya uhakika, ni wajibu wa Serikali kuisaidia na kuiwezesha sekta yake ya ndani. Katika kulitekeleza hilo, Wizara katika mwaka wa fedha 2023/2024 itaendelea na kukamilisha kiwanda cha kuchakata zabibu kilichopo Chinangali na kununua matenki ya kuhifadhi mchuzi wa zabibu. Kiwanda hiki kitaendeshwa na Sekta binafsi.

**221.** Katika hatua ya awali Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania ili kufikia lengo la kutokuuza korosho ghafi ifikapo mwaka 2026/2027 imeanza kutenga kiasi cha Shilingi Bilioni 10 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa wa eneo la ubanguaji wa korosho, kiwanda cha kubangua korosho. Pia, Bodi itawezesha ukusanyaji wa korosho sehemu moja ili kurahisisha upatikanaji wa malighafi hizo kwa ajili ya wabanguaji wa ndani.

**222. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Bodi itajenga ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 3,000 za korosho katika Wilaya ya Manyoni, kuweka mashine za ubanguaji na kukamilisha ujenzi wa ofisi za Bodi na ofisi za wasimamizi wawili katika mashamba ya pamoja ya korosho yaliyopo katika Wilaya hiyo. Vilevile, Wizara itaendelea na ujenzi wa *common use facilities* katika mikoa ya Iringa, Kilimanjaro na Dar es Salaam ambazo zitaendeshwa na Sekta binafsi.

**223.** Katika hatua nyingine ili kukabiliana na changamoto ya kuuza kahawa ghafi Wizara imejiwekea program ya miaka mitatu kuanzia mwaka 2023/2024 ya kufanya upembuzi yakinifu, kuhakikisha inaipatia mtaji na kubadili teknolojia ya Kampuni ya Kahawa ya TANICA ambapo mpango uliopo ni kubadilisha *business model* kwa kuunda mfumo ambao ni wa kimkakati na ushindani. Wizara itaanzisha Dar es Salaam Multiple Commodities Centre (DMCC) ili kuwezesha uuzaji wa mazao ya kilimo ambapo upembuzi yakinifu utaanza mwaka 2022/2023 kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo. Baada ya kukamilisha ujenzi, Sekta binafsi itakabidhiwa kwa ajili ya uendeshaji.

**224. *Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuboresha mfumo wa utendaji kazi wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Katika mwaka 2023/2024, Bodi itaachana na utaratibu wa kufungua maduka mitaani na badala yake ijiendeshe kibiashara na itaanza kutumia mfumo wa mawakala.

**c. Kuongeza Mauzo ya Mazao ya Kilimo Nje ya Nchi**

**225. *Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Taasisi, Bodi na Sekta binafsi itaongeza mauzo ya mazao mbalimbali kwa asilimia tano (5) kufikia Dola za Marekani Milioni 1,457.65. Mpango huu utawezesha kuongezeka mauzo baadhi ya mazao asilia ya biashara kama ifuatavyo: - pamba kutoka Dola za Marekani Milioni 227.1 hadi Dola za Marekani Milioni 238.46 na tumbaku kutoka Dola za Marekani Milioni 355 hadi Dola za Marekani Milioni 372.75.

**d. Upatikanaji wa mitaji (Agricultural Finance)**

**226. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024, itaendelea kushirikiana na taasisi za fedha katika kuimarisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwenye Sekta ya Kilimo. Wizara kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) itatoa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuwezesha vijana kupata mitaji kupitia programu ya BBT kwa riba isiyozidi asilimia 4.5.

**227.** Vilevile, Serikali baada ya kukamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo itaendelea na ukusanyaji wa mapato ya mfuko kwa ajili ya kuendeleza kilimo ikiwemo kinga ya bei (stabilization fund), pembejeo za kilimo (input support), miundombinu ya uhifadhi, utafiti na uongezaji wa thamani. Aidha, Wizara itaingia makubaliano na Mamlaka ya Udhibiti wa Bima (Tanzania Insurance Regulatory Authority-TIRA) ili kuandaa skimu mahususi kwa ajili ya utekelezaji wa bima ya mazao.

**228. *Mheshimiwa Spika,*** Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) itaongeza idadi ya taasisi za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana kutoka taasisi 15 hadi 21 ili kurahisisha utoaji wa mikopo; itawezesha miradi mipya 25 ya uchakataji, sita (6) ya ghala, miwili (2) ya vyumba vya ubaridi, minne (4) ya miundombinu ya umwagiliaji, mitatu (3) ya Mashamba Makubwa ya Pamoja, ununuzi wa matrekta 42 pamoja na *combine harvester* 10.

**229. *Mheshimiwa Spika,*** TADB itatoa mikopo ya pembejeo kwenye miradi 20 ya kilimo, itawajengea uwezo wakulima wadogo 1,400 kwenye kanda sita (6) kuhusu elimu ya fedha na itaanzisha kampeni ya kuwashawishi vijana kushiriki katika kilimo. Vilevile, TADB itaendelea na utoaji wa mikopo katika mnyororo wa thamani wa kilimo ikiwa ni pamoja na kushiriki katika utekelezaji wa Programu ya "Building a Better Tomorrow" - BBT inayolenga kuvutia vijana kushiriki katika uzalishaji na biashara ya mazao ya kilimo.

**e. Kuziwezesha maabara za Serikali na sekta binafsi ziweze kufikia viwango vya ubora vinavyokidhi soko la kimataifa**

**230. *Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024 kupitia TPHPA itaanza kuboresha miundombinu ya maabara za afya ya mimea za Kurasini, Kibaha, Tengeru na TPHPA makao makuu ili ziweze kupata ithibati na kuwezesha kutoa vyeti vya ubora vinavyokubalika kimataifa. Hatua hiyo itaboresha upatikanaji wa huduma hapa nchini na kupunguza gharama kwa wafanyabiashara wa mazao ya kilimo. Vilevile, itawezesha kufungua masoko ya mazao ya kilimo katika nchi mbalimbali ikiwemo soko la tangawizi nchini Marekani na China na soko la pilipili na parachichi nchini China pamoja na soko la ndizi (plantain) nchini Afrika Kusini. Aidha, Wizara kupitia TPHPA itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta binafsi ikiwemo kukamilisha maabara hizo kutoa vyeti vya ubora. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 166 hadi 173 wa kitabu cha hotuba yangu.***

**viii. Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika (Strengthening Cooperative Development)**

**a. Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika**

**231. *Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika kwa kuhamasisha ununuaji wa hisa za benki ya KCBL. Lengo ni kupata mtaji wa Shilingi Bilioni 15 ili benki hiyo isajiliwe rasmi kuwa Benki ya Taifa ya Ushirika ifikapo Juni, 2024. Aidha, Tume itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Mfuko wa bima ya akiba na amana za wanachama wa SACCOS utakaotumika kama kinga ya akiba na amana za wanachama iwapo SACCOS zao zitashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 na Kanuni zake za mwaka 2019.

**232. *Mheshimiwa Spika,*** Tume kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Leseni za Ghala (Warehouse Receipt Regulatory Board - WRRB), Soko la Bidhaa (Tanzania Mercantile Exchange - TMX), Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji imepanga kuweka mfumo rasmi na jumuishi wa biashara na masoko kwa mazao mbalimbali kutokana na mahitaji ya soko, miondombinu stahiki na kibali maalumu kutoka Wizarani.

**233. *Mheshimiwa Spika,*** Tume itaendelea kusimamia na kudhibiti Vyama vya Ushirika kwa kukagua vyama 7,300 na kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo Maafisa Ushirika, viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika. Aidha, Tume itaendelea kusambaza na kusimamia matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa kuongeza ufanisi, uwazi na kuboresha utendaji.

**234. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Wizara itaendelea kuiwezesha COASCO kutekeleza majukumu yake ili kupunguza utegemezi wa tozo za ukaguzi kutoka kwenye Vyama vya Ushirika. Mpango huu unalenga kuongeza uwazi na uwajibikaji katika shughuli za ukaguzi wa Vyama vya Ushirika ambapo mpango uliopo ni kuhakikisha Serikali itagharamia kwa asilimia 100 gharama za ukaguzi.

**235. *Mheshimiwa Spika,*** Tume itaendelea kutumia Mfumo wa Udhibiti wa Vyama vya Ushirika (MUVU) kuwezesha wakulima na wanaushirika kupata taarifa za uwekezaji, uzalishaji na masoko, malipo, upatikanaji wa pembejeo, mikopo na marejesho. Kadhalika, COASCO itakagua Vyama vya Ushirika 5,000 na kukarabati ofisi zake katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Shinyanga, Dar es Salaam na kujenga ofisi ya Songea.

**b. Kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha Kibiashara**

**236. *Mheshimiwa Spika,*** Tume itaendelea kuhamasisha vyama vya Ushirika kuongeza thamani ya mazao kwa kuratibu uanzishwaji wa viwanda ikiwemo kiwanda cha kubangua korosho cha TANECU Ltd na Kiwanda cha vifungashio kinachojengwa na SONAMCU Ltd. Aidha, Tume itaendelea kuratibu ufufuaji wa vinu vya kuchakata pamba vya Sola (Simiyu), Mugango na Buyagu (Mara) na Manawa (Mwanza).

**237. *Mheshimiwa Spika,*** Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itavijengea uwezo vyama vipya vya ushirika 121 vya mazao ya bustani katika Mikoa ya Mbeya, manyara, Iringa, Kilimanjaro, Songwe, Njombe, Arusha na Katavi kwa kutoa mafunzo ya biashara na kuwaunganisha na masoko ili wajiendeshe kibiashara.

**c. Kuimarisha na kupitia upya Mifumo ya Upatikanaji wa Viongozi wa Vyama vya Ushirika.**

**238. *Mheshimiwa Spika,*** Tume itaendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu katika Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na kupitia upya sifa za watendaji katika Vyama vya Ushirika na kuratibu ajira zote katika vyama. Aidha, Tume itaanzisha mfumo wa kielectroniki wa ajira katika Vyama vya Ushirika ili kuongeza uwazi katika upatikanaji wa ajira za Vyama vya Ushirika nchini.

**d. Kuendelea Kupitia upya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013.**

**239. *Mheshimiwa Spika,*** Tume itaendelea kupitia na kuboresha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 ili iweze kuendana na wakati. Lengo ni kuongeza uwajibikaji wa Vyama vya ushirika nchini. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 174 hadi 177 wa kitabu cha hotuba yangu)***

**Maeneo mengine muhimu yakayotekelezwa na Wizara**

**a. Kupitia Sheria za Kilimo**

**240. *Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2023/2024, itakamilisha tathmini ya mfumo wa kisheria uliopo kwenye Sekta ya kilimo kwa ajili ya kutungwa kwa Sheria ya Kilimo. Baadhi ya maeneo muhimu yatakayozingatiwa katika Sheria hiyo ni pamoja na kulinda ardhi ya kilimo, matumizi ya zana za kilimo, kilimo cha mkataba na uratibu wa ushiriki wa Kampuni na Asasi zisizo za Serikali katika Sekta ya kilimo.

**241. *Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Wizara itakamilisha mapitio ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 5 ya Mwaka 2013 na Sheria nyingine pamoja na miongozo ya utoaji wa huduma za ugani iliyopo kwa ajili ya kutungwa kwa Sheria Mpya ya Umwagiliaji na Huduma za Ugani. Baadhi ya maeneo yatakayozingatiwa katika Sheria hiyo ni pamoja na uratibu, uendelezaji na usimamizi wa kilimo cha umwagiliaji, uwezeshaji na usimamizi wa sekta binafsi katika masuala ya umwagiliaji, usimamizi wa maafisa ugani ili kufikia malengo mapana yaliyowekwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Mheshimiwa Spika, hatua ya kuwa na Sheria itakayosimamia maafisa ugani inatokana na ukweli kuwa hakuna jenerali ambaye anaweza kuendesha vita bila kuwasimamia askari wake waliopo mstari wa mbele na hawa ni maafisa ugani wa shughuli za kilimo***.

**b. Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo**

**242. *Mheshimiwa Spika,*** mbele ya Bunge lako tukufu ninaomba niseme wazi kuwa hakuna Serikali isiyoweka jitihada za kurasimisha Sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo hapa nchini inaonekana kama sekta isiyo rasmi kutokana na kukosekana kwa mifumo ya kisheria hususan katika usimamizi wa biashara za mazao ya kilimo na kutofautiana kwa mifumo ya ukusanyaji wa takwimu za kilimo iliyopo Serikalini. Hali hiyo, inasababisha kuwepo kwa misimu ya kilimo yenye sura tofauti kila mwaka, matukio ya watu kulalamika kutapeliwa na kampuni mbalimbali zilizoingia makubaliano ya kilimo na mauzo ya mazao pasipo kushirikisha Wizara ya Kilimo.

**243.** Aidha, nchi yetu inauza mazao mengi ya kilimo nje ya nchi lakini imedhihirika kuwa kuna baadhi ya wafanyabiashara wanauza mazao hayo pasipo kuwa na ushahidi wa kiasi cha fedha kilichopatikana na kuonekana kwa miamala ya malipo katika akaunti za benki za kampuni au wafanyabiashara husika. Hivyo ni lazima tuimarishe urasimishaji wa Sekta ya Kilimo kwa kuweka utaratibu wa kisheria utakao simamia shughuli zote za Sekta ya Kilimo.-

**244. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara itafanya tathmini ya mahitaji ya taasisi za Wizara ya Kilimo ili kuziunganisha itakapohitajika. Katika mchakato huo, Wizara pia itaainisha taasisi zinazojishughulisha kibiashara na taasisi wezeshi katika masuala ya biashara za kilimo, utafiti, uendelezaji na usimamizi wa tasnia husika na kuwasilisha mapendekezo yatakayoainisha taasisi zitakazoendelea kuwa chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na zitakazokuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo.

**245.** Miongoni mwa taasisi wezeshi katika masuala ya utafiti , uwezeshaji wa biashara ya mazao ya kilimo na uendelezaji wa mazao ni Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bodi za Mazao na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI). Taasisi hizo ni wezeshi katika masuala hayo ili kukidhi matakwa ya viwango vya kimataifa kama vile mkataba wa kimataifa wa masuala ya afya ya mimea (International Plant Protection Convection) na Skimu za Uthibitishaji wa Ubora wa Mbegu za OECD (Organization for Economic Cooperation Development Seed Schemes). Aidha, taasisi zinazofanya biashara ni Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) ambazo zinaweza kuendelea kuwa chini ya usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**246. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2023/2024, itaimarisha usajili wa wadau wa kilimo ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na watoa huduma nyingine katika shughuli za kilimo ikiwa ni pamoja na huduma za ugani, bima ya mazao na pembejeo za kilimo. Wizara inawaelekeza wadau wote kuendelea kujisajili katika mifumo iliyopo ikiwa ni pamoja na mfumo wa usajili wa wakulima utakaoonesha ukubwa wa mashamba yao, mazao wanayolima, pembejeo wanazotumia na taarifa nyingine muhimu.

***"Ninaomba nitoe rai kuwa mdau wa kilimo atakayekiuka mifumo ya kisheria itakayowekwa na ambaye atakayekuwa hajajisajili kwa ajili ya kutoa huduma yoyote ile kwenye sekta ya kilimo hatafanya shughuli hiyo hadi hapo atakapotambuliwa kwenye mfumo rasmi"***

**a. Kuimarisha Uratibu na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi, Mipango na Programu za Wizara**

**247. *Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Kujadili Mpango wa Kilimo na Chakula (Country Compact) uliofanyika tarehe 25-27 Januari, 2023 Jijini Dakar, nchini Senegal imeridhia Azimio la kuundwa kwa Baraza la kumshauri Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu uendelezaji wa Sekta ya Kilimo (Presidential Food and Agriculture Delivery Council).

**248. *Mheshimiwa Spika***, kupitia Bunge lako Tukufu ninapenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa nchi yetu ni ya kwanza kutekeleza azimio hilo kwa kuunda Baraza. Baraza hilo linaongozwa na Mh. Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni mtoto wa mkulima na Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo Mhe. Hailemarian Dessalegn Waziri Mkuu mstaafu wa Ethiopia.

**249. *Mheshimiwa Spika***, kutokana na Azimio hilo, Wizara ya Kilimo katika mwaka 2023/2024 itaunda timu ya Ufuatiliaji wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara (Agriculture Delivery Unit - ADU). Lengo ni kuongeza ufanisi na uwajibikaji miongoni mwa watendaji katika kutekeleza Mikakati, Mipango na Programu za Wizara ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Agenda 10/30. (***Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 177 hadi 184 wa kitabu cha hotuba yangu).***

**250. *Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2023/2024 umejikita katika maeneo matano (5) ya kipaumbele na mikakati ya utekelezaji 26 ambapo matokeo yafuatayo yanatarajiwa:-

i. Kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 727,280.6 mwaka 2021/2022 hadi hekta 1,078,471.06 mwaka 2024/2025 kwa miradi inayoendelea kutekelezwa;
ii. Kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 44,344 mwaka 2022/2023 hadi tani 127,650 mwaka 2023/2024;
iii. Kuongeza thamani ya mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 1.388 mwaka 2023 hadi hadi Dola za Marekani Bilioni 1.457 mwaka 2024;
iv. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 17.14 mwaka 2022 hadi tani milioni 18.7 mwaka 2023;
v. Kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea;
vi. Kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara; na
vii. Kutengeneza ajira takribani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030.

**251. *Mheshimiwa Spika,*** ni muhimu kutambua wazi kuwa mkulima mdogo hataweza kupima afya ya udongo, kuzalisha mbegu bora na kujenga miundombinu ya umwagiliaji. Hivyo, tusipowekeza kwenye kilimo kama tunavyowekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, SGR, Bwawa la Mwl. Nyerere na ununuzi wa ndege tusitarajie miujiza.

**252. *Mheshimiwa Spika***, hatuna budi kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, ghala, uzalishaji wa mbegu bora na kuongeza thamani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imelenga kuwekeza Jumla ya Shilingi **Trilioni 8.5** kwenye Sekta ya Kilimo katika kipindi cha miaka nane ijayo ili kuhakikisha mkulima wa nchi hii anapata huduma stahiki za kilimo.

**Hitimisho na Shukrani**

**253. *Mheshimiwa Spika,*** shughuli za kilimo hapa nchini ni muhimu kwa maisha na ustawi wa watu na uchumi wetu. Kimsingi, kilimo ni nyenzo muhimu katika mapambano dhidi ya umaskini wa kipato na umaskini wa chakula. Kilimo kinapanua fursa za ajira kwa kushirikisha wananchi wengi katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo na hususan biashara ya mazao ya kilimo ndani ya nchi na kimataifa. Kwa msingi huo, mageuzi tarajiwa kuelekea uchumi wa viwanda, kipato cha kati na kujitajirisha yatategemea jitihada zetu tulizoziweka kwenye kilimo.

**254. *Mheshimiwa Spika,*** Hata hivyo, mchango wa sekta hii katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii hausadifu fursa kubwa tuliyonayo kama nchi. Kwa kiasi kikubwa hali hii inachangiwa na mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wetu, hususan kuwa na fikra kwamba mkulima wa nchi hii atajiendesha mwenyewe bila msaada wa Serikali.

**255. *Mheshimiwa Spika***, tumedhamiria kuondokana na fikra hizi zinazotawala kwenye akili zetu kwa kufanya mageuzi makubwa katika uendeshaji wa shughuli za kilimo. Kwanza tumeamua kuweka msukumo katika mabadiliko ya fikra na mazingira ya kibiashara kwa sekta ya kilimo kwa lengo la kubadili mtazamo wa uendeshaji kilimo kama shughuli ya kujikimu na badala yake iendeshwe kibiashara kwa faida ya nchi na wakulima wetu.

**256. *Mheshimiwa Spika,*** dhamira hii ya Serikali ni endelevu na ya kweli. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuanza utekelezaji wa hatua hii ya mageuzi kwa ari na mifano ya dhati ambapo ameongoza ujumbe wa Tanzania katika mikutano lukuki ya kilimo kikanda na kimataifa na kufanya uzinduzi wa shughuli kadhaa za kilimo ikiwemo Mpango wa Mashamba Makubwa unaotekelezwa chini ya Programu ya BBT. Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa maelekezo ya kuondoa kero na vikwazo visivyostahili walivyowekewa wakulima kwa miaka mingi kwani kuna dhana kuwa mazao ya mkulima ni mali ya umma naomba niseme hapa mazao ya mkulima ni mali yao na watauza wanapotaka.

**257. *Mheshimiwa Spika,*** kwa maelekezo hayo mimi sioni sababu za kusita kuchukua hatua na kutekeleza maelekezo yote ya Mhe. Rais. Tutaweka mfumo mpya wa usimamizi wa kilimo kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi kwa uendeshaji kibiashara na kuwezesha wakulima kuwa na sauti katika uendeshaji na biashara ya mazao yao.

**258. *Mheshimiwa Spika,*** katika Taifa lolote duniani usalama wa kwanza wa nchi ni kujitosheleza kwa chakula, hakuna maendeleo ya kweli kama hakuna chakula, lakini hakuna chakula kama hakuna wakulima. Mimi na Wizara ninayoiongoza nitaendelea kulinda maslahi ya wakulima na wadau wa sekta ya kilimo. Hivyo, ninawaomba kwa heshima na taadhima waheshimiwa Wabunge muiunge mkono Serikali katika mageuzi haya ya muda mrefu.

**MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2023/2024 FUNGU 43, 24 na 05**

**a. Makusanyo ya Maduhuli**

**259. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi **16,677,254,000** kupitia Fungu 43 na 05 kutokana na ukaguzi wa mazao, ada ya huduma za umwagiliaji na uuzaji wa nyaraka za zabuni.

**b. Fedha kwa Mafungu yote (43, 24 na 05)**

**260. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 970,785,619,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 ikiwa ni ongezeko la asilimia 29.24 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2022/2023.

**c. Fedha kwa Fungu 43**

**261. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Shilingi **577,717,997,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **465,698,366,000** ni kwa ajili ya kuendeleza Miradi ya maendeleo ambapo Shilingi **365,642,532,000** ni fedha za ndani na Shilingi **100,055,834,000** ni fedha za nje. Aidha, Shilingi **112,019,631,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **56,554,950,000** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi **55,464,681,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara, Bodi na Taasisi.

**d. Fedha kwa Fungu 05**

**262. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **373,511,998,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **299,964,223,000** ni fedha za Maendeleo na Shilingi **73,547,775,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**263. *Mheshimiwa Spika***, kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, Shilingi **288,464,223,000** ni fedha za ndani na Shilingi **11,500,000,000** ni fedha za nje. Aidha, kati ya Shilingi **73,547,775,000** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zinazoombwa, Shilingi **66,332,659,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi **7,215,116,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Tume.

**e. Fedha kwa Fungu 24**

**264. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **19,555,624,000.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **17,383,074,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **9,057,615,000** ni mishahara (PE) ya watumishi na Shilingi **8,325,459,000** ni matumizi mengineyo (OC). Aidha, Shilingi **2,172,550,000** zinazoombwa kutekeleza miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, Shilingi **1,000,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **1,172,550,000** ni fedha za nje.

**265. *Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara: ***www.kilimo.go.tz***

**HITIMISHO**

**266. *Mheshimiwa Spika***, NINAOMBA KUTOA HOJA

# Wajasiriamali walivyojipanga kuwasomesha wenye uhitaji

• Wanufaika waandaa kitabu kilichobeba maono ya binti

Na Halfani Chusi

KATIKA kuunga mkono jitihada za serikali kuona kuwa kila mtoto anapata elimu na kutimiza ndoto zake, Shirikisho la Vikundi vya Ujasiriamali Tanzania (SHIVUTA), lipo kwenye mchakato wa kufadhili na kuwasomesha watoto yatima 35 ili waweze kufikia malengo yao kielimu.

Mkurugenzi wa SHIVUTA, Andrew Koti, akiwa na watoto wanaowafadhili, wazazi na wanavikundi vya ujasiriamali anasema mbali na eneo hilo, taasisi ina endesha miradi mingine mingi.

Anataja 'mpe nafasi' ulioanzishwa na kikundi cha wazazi 16 wa watoto wenye ulemavu ili kuwapa elimu na kuwasaidia ili wapate nafasi ya kuonyesha uwezo wao.

Mradi mwingine anasema ni 'mwalimu ng'ara', unaolenga kumtia moyo na kuongeza thamani ya mwalimu ambaye ni msingi wa mafanikio ya kada zote wakiwamo viongozi na wataalamu, anasema Koti.

Anautaja pia mradi wa 'binti kinara' unaolenga kumwibua mtoto wa kike anayefanya vizuri kwenye masomo na mwenye ndoto za kufanikiwa na kuisaidia jamiii yake.

"Mpaka sasa tunawaandaa mabinti vinara 10, na tayari wameanza uandishi wa kitabu cha ushairi ambacho kitajikita katika kuelezea mambo mtoto wa kike anatakiwa kufanyiwa ili atimize malengo yake. Na mradi utazinduliwa rasmi na Miss Tanzania 2021 Juliana Lugumisa na lengo lake ni kutengeneza wataalamu wenye moyo wa kujali, kusaidia na kuthamini wale wanaohitaji huduma yao," anafafanua Koti.

Mkurugenzi anaendelea na ufafanuzi kuwa baada ya kukamilika kwa uandishi wa kitabu hicho Septemba mwaka huu, watakipeleka kwenye ngazi ya juu ya serikali ili waweze kukitumia kama mwongozo wa kujua nini mtoto wa kike anapaswa kufanyiwa ili afikie malengo na kwamba maono ya SHIVUTA, ni kutanua huduma na ili waweze kuwafikia watu wengi zaidi, hatimaye kutengeneza kizazi chenye kujivunia utu wao taifa lao na kuwapenda wale wanao wahudumia.

"Mbali na kuwafadhili kimasomo, pia watakuwa wanakutanisha watoto hao na watu ambao wamefikia ndoto ambazo walengwa hao wanatarajia kuzifikia. Kama ni udaktari wale wanaotaka fani hiyo tutawapeleka Hospitali ya Muhimbili kukutana na madaktari bingwa ili waweze kuuliza kile wanachokitaka," anasema Koti.

"Yupo anayetamani kuwa mwanajeshi, tutampeleka jeshini akaone kwa macho nini kinafanyika kule, ili aweze kushawishika na kupata matamanio ya kufikia malengo yake," anasema na kuongeza kuwa wanaamini mtoto akishapelekwa maeneo ambayo anatamani kuyafikia, itampa moyo na kumwongeza matumaini na hivyo atasoma kwa bidii ili afikie haja ya moyo wake.




Aliyekuwa Miss Tanzania 2021, Juliana Lugumisa, akishiriki katika matukio ya uzinduzi wa miradi ya binti kinara na mfuko wa kusaidia watoto wenye mahitaji kupata elimu pamoja na kujitoa kuwa mlezi wa mfuko huo. Kushoto ni Mkurugenzi wa SHIVUTA, Andrew Koti. **PICHA: HALFANI CHUSI**

> **"Tunataka wazazi, jamii na viongozi wa serikali kuhakikisha watoto wanafikia malengo tutahakikisha watoto wa kike wanafikia ndoto zao.**

Anakumbushia kwenye kitabu cha ushairi ambacho kinaandaliwa kuwa kinaandikwa na wanafunzi wenyewe kwa kushirikiana na walimu wao, wakiamini mtoto mwenyewe ndiye anayejua nini akifanyiwa kitamfikisha kwenye lengo lake, lakini kitatawanywa kote nchini ili wazazi na walezi waone na wajue nini watoto wanapaswa kufanyiwa ili kufikia malengo yao, kwa hiyo tumeona njia rahisi kuandika kitabu.

"Nimefurahi sana kuwapo mahali hapa, na nilipokuta picha yangu kwenye bango pale nikashtuka kwa kuona mnachokifanya ni kwa ajili ya jamii kama ilivyo kwangu mimi ni mwanataaluma wa viungo bandia, pia ni mwanzilishi wa taasisi ya kusaidia watu wenye ulemavu wa viungo. "Nimefurahi kuwapo mahali hapa, najaribu kufupisha lakini nitasema machache mwanzoni nilitamani kuwa daktari lakini nilikuwa nikikumbuka kumchoma mtu sindano au kushuhudia damu zinavyomwagika niliogopa, lakini nikatafuta namna ya kumsaidia mtu bila kukutana na adha hiyo," ni kauli ya Juliana Lugumisa.

"Ndiyo maana nikaamua kuingia kwenye kusaidia watu wenye ulemavu kupata viungo bandia maana kule unakutana na mtu mguu umepinda mara mkono angalau hapo nikaona patanifaa," anasema mshindi huyo na kuongeza:

"Binti kinara mnawaona ndugu zenu, mama, baba walezi wanafanya haya yote kwa ajili yenu, wanataka mfanikiwe mnaweza mkawa na ndoto zenu lakini mkawa hamna uhakika ndio maana wametengeneza programu tofauti tofauti kuwapeleka kutembelea maeneo mbalimbali."

Anaendelea kuwasihi mabinti hao akitamka "Mnapelekwa sehemu ambazo nyie mnatamani kuzisomea ili mfike, wengine ambao hawajafadhiliwa wanatamani sana lakini bahati imekuwa kwenu, hii ni safari, ya kipi unataka kuja kukifanya. Kitu chochote ukikipenda kutoka moyoni na ukakisomea utakuwa na amani ya moyo kwa kuwa umesomea kitu ambacho unakipenda," anashauri Juliana.

### MATARAJIO YAO

Mwenyekiti wa SHIVUTA, Ayubu Naftali, anasema matarajio ya baada ya miaka mitatu ni kuwafikia wanafunzi wengi zaidi na kuwafadhili.

"Tunatarajia kama shirikisho kuwafikia wanafunzi wengi zaidi, hasa wale wenye uhitaji lakini hawana uwezo wa kusoma kwenye shule za vijijini ambazo wengi wao wanaziita kayumba.

"Tunataka wazazi, jamii na viongozi wa serikali kuhakikisha watoto wanafikia malengo tutahakikisha watoto wa kike wanafikia ndoto zao," anasisitiza mwalimu huyo wa wajasiriamali.

Msajili wa Vikundi wa Jiji la Dar Salaam Mwanaisha Ali, anampongeza shirikisho hilo kwa kusaidia jamii huku akitoa wito kwa wengine kuiga mfano huo na kusema licha ya vikundi hivi kujiunda kwa ajili ya kusaidiana lakini vinapaswa kukumbuka jamii na kuwafikia wale wenye uhitaji ili waweze kufikia malengo kama inavyofanya SHIVUTA.



# Homa ya nguruwe tishio Nyanda za Juu Kusini

**Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI 11 kati ya 15 za mikoa mitano ya Nyanda za Juu Kusini, zimebainika kuwapo kwa tatizo la ugonjwa wa homa ya nguruwe huku mifugo 2,000 ikiripotiwa kufa kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Mei, mwaka huu.

Hayo yalithibitishwa jana na Ofisa Mfawidhi wa kituo cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo Nyanda za Juu Kusini (ZVC), Dk. Jeremia Choga kwenye kikao cha kuwajengea uwezo wafugaji namna ya kukabiliana na ugonjwa wa homa ya nguruwe.

Aliitaja mikoa ambayo halmashauri zake zimeathirika kwa kiwango kikubwa kuwa ni Mbeya, Iringa, Njombe, Katavi na Rukwa na kwamba sababu kubwa ya kuenea kwa ugonjwa huo kuwa ni usafirishaji holela wa nguruwe.

"Kuna baadhi ya wafugaji na wafanyabiashara sio waaminifu wamekuwa wakisafirisha mifugo kinyemele kuuza maeneo mbalimbali yakikwepa kufuata taratibu za upimaji wanyama hao pamoja na ushuru hali iliyosababisha kuenea kwa ugonjwa huo.

Alifafanua kuwa kwa kipindi cha Januari hadi Mei, zaidi ya nguruwe 2,000 sawa na asilimia 40 zimekufa na zimekuwa zikizalishwa na kusafirishwa katika maeneo mbalimbali.

Dk. Choga alitaja mikakati ya kukabiliana nayo ni pamoja na kuagiza wataalamu wa mifugo kufuatia maeneo ya mashamba ya ufugaji, ukaguzi wa mabanda na kuchukua hatua.

"Tunajitahidi kudhibiti ndani ya mikoa husika ili usianze kusambaa maeneo mengine ikiwamo kuwataka wafugaji kuwa na mchango mkubwa wa kuwafichua baadhi yao wanaochochea kusambaa kwa vimelea kwa kasafirisha kwa njia za kipanya," alisema Dk. Choga.

Aliongeza kuwa serikali imeweka mikakati ya kuboreshwa uzalishaji wa sekta hiyo ikiwamo kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi na ndiyo maana wameweka mkazo wa kukabiliana na ugonjwa huo usienee maeneo mengine.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Nguruwe Tanzania (TAFIPA), Doreen Maro, alisema chanzo cha kusambaa kwa ugonjwa huo mikoa ya Nyanda za Juu ni kutokana na ufugaji holela usiozingatia kanuni na ukosefu wa mabanda ya kuhifadhia.

Mfugaji na mfanyabiashara, Joachim Noel, alisema tatizo kubwa ni wataalamu wa afya ya mifugo kutofanya ukaguzi wa mabanda na kutoka vibali kiholela na ndiyo tatizo kubwa la ufugaji holela na kusababisha milipuko ya mara kwa mara.




Ofisa Habari na Uhusiano Mwandamizi Mkuu, Mabel Masasi, wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) akigawa vipeperushi kwenye basi la abiria (daladala) jijini Mbeya ikiwa ni kampeni ya 'Tuma Chap ya Utumaji wa Vifurushi na Vipeto' kwenye viunga vya jiji hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aagiza sehemu za starehe kuwekwa kondomu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameagiza wamiliki wote wa hoteli, baa, kumbi za starehe kuweka kondomu katika maeneo hayo ili kudhibiti maambukizi ya Virusi vya Ukimwi.

Alitoa agizo hilo jana kwenye kikao cha kujadili utekelezaji wa miradi ya Afua mbalimbali za kukabiliana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi unaotekelezwa na Shirika la Henry Johnson Foundation Medical International Research (HJFMRI) na wadau wengine wa kupambana na Ukimwi.

Alisema kasi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi bado ni kubwa, kwa utafiti uliofanywa hivi karibuni rika balehe, wanawake na vijana zaidi ya 100,000 wanadhaniwa kuwa na Ukimwi sawa na asilimia 87.

Alisema licha ya Shirika la HJFMRI kuisaidia serikali katika mapambano hayo kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya kuwasaidia vijana na wanawake kuepukana na maambukizi mapya, njia nyingine ni wamiliki wa kumbi za starehe, baa na hoteli kuweka kondomu ili w a t u wazitumie kwa ajili ya kujikinga.

"Kuanzia sasa wamiliki wote wa kumbi za starehe (klabu) hoteli na baa lazima muweke maboksi ya kutosha ya kondomu ili watu wazitumie kukabiliana na maambukizi ya Ukimwi, nawataka waganga wakuu wote wa Mkoa wa Mbeya kulisimamia hili kuhakikisha linatekeleza maana msako utaanza mara moja," alisema Homera.

Pia, katika kutelekeza afua mbalimbali za kukabiliana na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi, aliliomba Shirika la HJFMRI kuongeza wigo wa utoaji huduma na kuzifikia wilaya zote za mkoa huo badala ya Kyela, Mbarali na Halmashauri ya Jiji la Mbeya pekee.

Mratibu wa Huduma za Virusi vya Ukimwi na Ukimwi kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya maambukizi nchini, Abdul Mashauri, alisema nchi za Kenya na Uganda zimekuja nchini kwa lengo la kujifunza namna Tanzania inatekeleza afua mbalimbali za maambukizi ya virusi hivyo.

Alisema ugeni huo ambao upo jijini Mbeya utajifunza Shirika la HJFMRI Tanzania linavyotekeleza miradi yake katika mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi.

Vile vile, serikali imeanzisha programu za kukabiliana na Ukimwi ikiwamo kutoa elimu za mabadiliko ya tabia, uzazi na namna ya kujikinga na maambukizi.

"Sababu kubwa ya mabinti wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 24 kuwa katika hatari kubwa ya kupata Ukimwi ni kutojitokeza kupata huduma za VVU, hofu na mtazamo wa jamii mabinti hao kupata maambukizi wakiwa kwenye umri mdogo.

# Wanafunzi wakike Chuo Mzumbe kujengewa mabweni

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHILINGI bilioni 5.8 zinatarajiwa kukusanywa na Chuo Kikuu cha Mzumbe kutoka kwa wadau mbalimbali kujenga mabweni ya wanafunzi wa kike wa chuo hicho ndaki ya Mbeya.

Uamuzi huo unatokana na kuwapo kwa idadi kubwa ya wanafunzi wa kike kuishi nje ya mazingira ya shule hali inayohatarisha usalama wao na kuharibu ndoto zao ikiwamo mimba na ubakaji.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa William Mwegoha, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari, kutangaza matembezi ya hisani ili kukusanya fedha hizo kujenga mabweni ya wanafunzi.

Prof. Mwegoha alisema kwa sasa Chuo cha Mzumbe Ndaki ya Mbeya ina hosteli ya kubeba wanafunzi 410 ambayo wanawake 260 na wanaume 150 idadi ni ndogo ikilinganishwa na wanafunzi waliopo ambao ni 34,011. "Tumeona vikwazo wanavyovipata wanafunzi wa kike kukaa nje ya shule, sasa ili kuwasaidia viongozi wa Mkoa wa Mbeya pamoja na chuo tumeanzisha matembezi ya hisani kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa hosteli za wanafunzi hao.

Alisema matembezi hayo yanatarajiwa kufanyika Mei 25, mwaka huu, katika eneo la Kabwe kuelekea Chuo cha Mzumbe na kila mwananchi anakaribishwa kuchangia chochote alichonacho ili kukamilisha ujenzi huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameshazindua mpango huo ambao alisema utasaidia wanafunzi wa kike kusoma kwa amani na utulivu ili kutimiza ndoto zao.

Homera alisema kukamilika kwa hosteli hiyo kutasaidia kuchukua wanafunzi 800 watakaosoma kwa uhuru.

Alisema kila mwananchi anakaribishwa kuchangia na wauzaji wa vifaa vya ujenzi, viwanda vya kutengeneza saruji wamiliki wa magari ya kubeba mchanga wameombwa kushiriki.

"Mei 25 ujenzi utaanza rasmi maana tayari tutajua ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa, eneo tayari lipo kinachosubiriwa sasa ni fedha, nawaomba wadau mtuunge mkono ili kukamilisha ujenzi huu ambao tayari na mimi nimechangia kwa namba ya malipo 994180331310.

Mkuu wa Chuo cha Mzumbe Ndaki ya Mbeya, Profesa Henry Molel, aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi kuchangia ujenzi wa chuo hicho ili wanafunzi wote wa kike chuoni hapo wakae shuleni.

## Wazee watakiwa kushirikiana kuenzi watoto wao

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee, Hassan Ibrahim Suleiman, amewataka wazee kushirikiana kuwaelimisha vijana wao kuwaenzi watoto ambao ndiyo nguzo muhimu katika jamii.

Akifungua mafunzo ya Mabaraza ya Wazee kuhusu umuhimu wa kuwatunza wazee katika jamii, alisema vijana kuwatunza wazee kunawafanya nao pia kutunzwa na watoto wao wakati watakapozeeka.

Aliwataka wazee kuyatumia vizuri mafunzo wanayopatiwa ili iwe chachu ya kuwaenzi wazee katika jamii inayowazunguka.

Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Wazee, Bikame Sheha Ussi, alisema lengo la mafunzo hayo ni kukumbushana umuhimu wa kuwatunza wazee kwa mabaraza hayo ya wazee ili nao kusaidia kuwaelimisha na wingine katika shehia zao.

Aidha, aliwataka washiriki hao kuwa mabalozi wazuri wa kuelimisha wingine katika jamii ili lengo lililokusudiwa kufikiwa.

Akiwasilisha mada ya wazee, Ofisa Wazee kutoka Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee, Pili Mussa Saadala, alisema mzee ana umuhimu mkubwa katika jamii hasa katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Wakitoa michango yao juu ya haki za wazee, baadhi ya washiriki walisema wazee wana haki ya kupatiwa elimu, kushirikishwa katika vikao vya ushauri pamoja na kupatiwa unafuu wa nauli za usafiri pamoja na kupewa fursa katika sehemu mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kuwezeshwa.

# Wanaoidai FBME kupatiwa ufumbuzi fedha zao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KILIO cha muda mrefu cha wananchi wanaodai fedha zao katika Benki ya FBME baada ya benki hiyo kufungwa kinatarajiwa kupatiwa ufumbuzi.

Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB), Isack Kihwili, alisema benki hiyo ipo katika ufilisi, ambayo tayari imeshalipa fidia.

Alisema mchakato wa ufilisi unasubiri uamuzi wa kesi iliyofunguliwa kupinga mkataba na unatarajia kutolewa mwezi huu (Mei) ili mchakato wa ufilisi na malipo uanze.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari walioshiriki mafunzo yaliyoandaliwa na Benki Kuu Tanzania (BoT), ambayo yamelenga kuwajengea uwezo wa kutambua majukumu yake.

Alisema FBME makao yake makuu yalikuwa Tanzania, lakini ilikuwa na biashara nyingi nchini Cyprus juhudi za ufilisi zilifanyika, lakini kulikuwa na mkwamo kutokana na matatizo ya kisheria.

Alisema mkwamo ambao ulikuwapo kwa muda mrefu umekwisha baada ya Desemba 12, mwaka jana DIB kufikia makubaliano na Benki Kuu ya Cyprus (CBC) kuhusu ufilisi wa tawi la FBME Cyprus.

Alisema kwa sasa fedha zilizopo ni zaidi ya asilimia 55 na zikikusanywa kutakuwa na kiwango kitakachotoka Cyprus kwa ajili ya kujazia kinachopungua.

Alisema Sh. bilioni 341 zinazodaiwa katoka benki hiyo iliyokuwa na wateja 6,660, Tanzania Bara wanadai Sh. bilioni 12.7, Zanzibar Sh. bilioni 20.5 na wateja wa nje Sh. bilioni 308. 2.

"Ili kuondoa changamoto zilizojitokeza kama FBME, kwa sasa DIB na BoT wamekubaliana iwapo kuna benki ikitaka kwenda kufanya kazi zake nje ya nchi iende kama tanzu na sio tawi ili ikitokea kuanguka nchi iwe na mamlaka ya kuchukua hatua zote," alisema.

Alizitaja benki zingine ambazo DIB inaendelea na ufilisi ni Greenland, Delphis, Covenant Bank for Women, Meru Community Bank, Kagera Farmers' Cooperative Bank, Njombe Community Bank, Efatha Community Bank Ltd na Mbinga Community Bank Plc.

Akizungumzia kuhusu kiwango cha juu cha kinga kwa wenye amana katika benki alisema serikali imeongeza kiwango kutoka Sh. milioni 1.5 hadi Sh. milioni 7.5 iwapo benki ikiwekwa chini ya mufilisi.

"Kiwango hiki kimeanza kutumika Februari mosi, mwaka huu ikiwa na maana benki ikianguka mwenye amana ya kiasi chochote hadi Sh. milioni 7.5 atalipwa amana yake yote bila kusubiri kukamilika mchakato wa ufilisi," alisema.

"Bodi ya bima imefanya uchambuzi wa hali halisi ya thamani, tukaona ni kiasi kidogo na sisi kama DIB tukashauri serikali nayo imesikia kilio cha wananchi ikatoa maelekezo kwa kuangalia hali halisi ya uchumi," alisema Kihwili.

Hata hivyo, alisema mteja mwenye kiwango kinachozidi hicho iwapo benki husika itaanguka, atasubiri utaratibu wa ufilisi waanze kufidiwa.

Julai 14, 2014 Benki Kuu ya Tanzania iliiweka chini ya usimamizi maalum FBME hatua inayotokana na notisi ya Julai 15, 2014 iliyotolewa na Marekani inayopambana na uhalifu wa kifedha unaotokana na utakatishaji wa fedha haramu.

Meneja wa Idara ya Uchumi wa BoT, Motto Lugobi, alisema Benki Kuu ni taasisi ya Muungano ambayo ipo kwa ajili ya kuzishauri serikali zote mbili kuhusu hali ya mwenendo wa uchumi na masuala ya sarafu na noti.

Aidha, alisema Benki Kuu ya Tanzania ndiyo msimamizi wa benki zote ya biashara nchini ikiwamo katika kutoa leseni huku ikiwa msimamizi mkuu katika kuona taasisi hizo zinaendesha biashara zake vizuri na kuleta tija kwa wateja.




Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Raya Issa Mselem, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuanza kwa vikao vya baraza hilo jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Baraza la Wawakilishi kuanza kujadili bajeti 2023/24

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUTANO wa 11 wa Baraza la 10 la Wawakilishi unatarajiwa kuanza kesho na kujadili mambo mbalimbali ikiwamo mwelekeo wa bajeti ya serikali ya mwaka 2023/2024.

Akitoa taarifa ya shughuli za baraza hilo jana, kwa vyombo vya habari, Katibu wa Baraza hilo, Raya Issa Msellem, alisema katika kikao hicho ofisi imepokea maswali 246 yameratibiwa kuulizwa na wawakilishi wa majimbo mbalimbali.

Katibu Raja alisema shughuli nyingine ni kuwasilishwa kwa miswada minne ya sheria na kujadiliwa ikiwamo Mswada wa Sheria ya Fedha (Finance Bill) na Mswada wa Sheria ya kuidhinisha matumizi ya serikali kwa mwaka 2023/2024.

Aidha, alisema muswada mwingine ni wakufuta Sheria ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi Zanzibar namba 1 ya mwaka 2012 na kutunga upya sheria ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi Zanzibar na mambo mingine yanayohusiana na hayo na mswaada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar na kuweka masharti yanayohusiana na huduma ya miundombinu ya TEHAMA na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Alisema shughuli nyingine ni kujitokeza kwa jambo lolote yatasomwa kwa ruhusa ya Spika wa Baraza hilo, Zubeir Ali Maulid na kusomwa kwa mara ya kwanza kwa miswada itakayojitokeza.

Akizungumzia Baraza kuendelea kutumia vishkwambi, alisema wajumbe wote 77 wanaendelea kutumia vifaa hivyo na asilimia 75 imepunguza utumiaji wa karatasi na kupunguza matumizi ya fedha kwa baraza na serikali.

Pia wameweka mfumo maalum wa uingiaji na utokaji wa ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, sasa mfumo utamtambua moja kwa moja mjumbe na watu maalum na sio kama zamani kila mtu kuingia.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA KADI YA BAJAJI

**LEGAN JOHNSON MBEMBATI ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya **BAJAJ** mali ya **MECK NEHEMIA SANGA** yenye namba za usajili **MC 898 BSD** Chasis Namba: **MD2A25BZ9GWD81357.** Engine Namba: **AZZWGD58016.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/156911/2023.**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NO.81/2022**
**LUCIA DANIEL MWANG'OMBE:::::MDAI**
**DHIDI YA**
**1.ENITAR SAINETI MWANGILE:::MDAIWA**
**2.SAMSON DANIEL MWANG'OMBE:::MDAIWA**
**3.ELENAUS VALENTINO SANGA:::MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA:SAMSON DANIEL MWANG'OMBE**
Fahamu kwamba LUCIA DANIEL MWANG'OMBE amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 10/05/2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere mwenyekiti wa baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 03/05/2023.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**03/05/2023**

---

## KUPOTELEWA NA CHETI



**RUKIZA FRANCIS CLAVERY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S.1185/0081** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **DAR ES SALAAM BAPTIST SEKONDARI** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: DAR/URA/RB/156633/2023.**

---

## KUPOTELEWA KADI YA GARI

**GHAWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 881 CCX TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis namba JTERB71J500064323. Engine namba IHZ 4164mL.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Taarifa ya polisi: PWA/KIS/RB/151829/2023.**

---

## KUPOTEA KWA CERTIFICATE OF REGISTRATION

**ASKOFU DR. CHARLES GADI** Anatangaza kupotelewa na Certificate of Registration chenye usajili wa So.NO.12183 kilichotolewa na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 2005. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa polisi: **OB/RB/5391/2013. Au Piga No. 0756479024/0754364356.**

---

## KUPOTELEWA KADI YA GARI

**SHARIF ALLI HAMAD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI ESCUDO** yenye usajili namba **T369 ARG, CHASSIS NAMBA: TD01W152121** na **ENGINE NAMBA: G16A361943 T369ARG.** Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/157565/2023**

---

## KUPOTELEWA NA CHETI



**CHARLES FABIAN SEBHO** anatangaza kupotelewa na cheti chenye jina **CHARLES FABINA SEBHO** chaTaaluma ya Uuguzi na Ukunga ngazi ya Stashahada Reg. HAS/023/052/2008 kilichotolewa na Wizara ya Afya kupitia **CHUO CHA UUGUZI NA UKUNGA KABANGA CHA KISULU** Mwaka 2011. Yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/157808/2023.**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MKUYUNI**
**WILAYA YA NYAMAGANA**
**SHAURI LA MIRATHI NA.141 YA 2022**
**FELISTER D/O JOSEPH NKONO............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**EMMANUEL S/O KAHINDI NGHUMBA......MAREHEMU**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: 1. HELENA EMMANUEL**
**2. DEBORAH EMMANUEL**
**3. HAPPYNESS EMMANUEL**
**4. JOHN EMMANUEL**

**POPOTE WALIPO**
Mahakama hii inawafahamisha kwamba Mwombaji (Felister d/o Joseph Nkono) amefungua shauri la mirathi nakala yake inapatikana katika mahakama hii.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 08/05/2023 saa 2:30 asubuhi na mnatakiwa kuwepo bila kukosa.
Zingatieni kwamba kutokufika kwenu tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya ninyi kuwepo na maamuzi kutolewa upande mmoja.
Imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 02 mwezi 05 mwaka 2023.

J.D. OPUDO
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MKUYUNI
MWANZA

---

## KUPOTEA KWA PASPOTI YA KUSAFIRIA



**ANNETH JONATHAN ELIAHU** anatangaza kupotea kwa paspoti ya kusafiria yenye namba **TAE 121652** iliyotolewa **DAR ES SALAAM PCO** JUNI **14, 2019.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**TAARIFA POLISI: DAR/URA/158294/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 32 YA 2023**
**ISMAIL IBRAHIM KULENGWA...........MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1. ZAINABU HUSSEIN..............MJIBU MAOMBI**
**2. ATHUMANI NGEDERE.........MJIBU MAOMBA**

**ATHUMANI NGEDERE** Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro tarehe 23/05/2023 mbele ya Mwenyekiti E.MOGASA wewe mwenyewe binafsi au Utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa **MKONO** wangu na **MUHURI** wa Baraza leo tarehe 05 mwezi May 2023

E.MOGASA
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO

---

## TANGAZO LA NOTISI MDAIWA SUGU

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Sitini (60) kwa wadaiwa sugu wafuatao:-

1. Jonas Vedastus Butingo – Kiseke ward (Mwanza)
2. Kanuti Ernesti Kimaro – Kishiri ward (Mwanza)
3. Valentine Kundael Tarimo- Kangaye 'A' Nyakato (Mwanza), mdhamini wa Kanuti .E. Kimaro

Hivyo wanatakiwa kulipa madeni yao ya mikopo wanayodaiwa na kampuni ndani ya muda ulioidhinishwa. Hii ni baada ya kushindwa kulipa madeni yao kulingana masharti na makubaliano ya mkataba.

Notisi hii itatumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili gazetini.

Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa dhidi yanu endapo kama mtashindwa kulipa madeni ya mikopo ndani ya muda ulioainishwa (siku sitini).

Ikiwa ni pamoja na kuruhusu dalali kuuza mali zanu ambazo zimetumika kudhamini mkopo mliochukua.

**Kwa Mawasiliano piga:**
**+255 222774742-3/0677001063**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

# OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HATIMAYE KICHOCHEA MIMBA, NDOA UTOTONI SHINYANGA CHAGUNDULIWA

**NA MARCO MADUHU,**

**SHINYANGA**

MIMBA na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga huenda zikaendelea kuwa tatizo, kutokana na wahusika wa ubakaji kuwalaghai mabinti na wanafunzi kisha kutokufungwa gerezani.

Shinyanga inatajwa katika utafiti wa mwaka 2012 unaofanywa na Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) kuwa inaongoza kwa mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na mkoa wa Tabora asilimia 58 na wa tatu ni Mara wenye asilimia 55.

Ikimaanisha kuwa katika kila mabinti 100 mkoani humo 59 ni waathirika wa mimba na ndoa za utotoni jambo ambalo linalifanya eneo hilo lisiwe mahali salama kwa wasichana wa chini ya miaka 18.

Kwa mujibu wa Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga Lydia Kwesigabo, mapambano ya kutokomeza mimba na ndoa za utotoni yanakwamishwa na ukosefu wa nyumba au eneo salama la kuwahifadhi waathirika.

Anasema licha ya watuhumiwa kukamatwa kwa madai ya kuwapa mimba wanafunzi, kesi zinapofikishwa mahakamani wanafunzi hurubuniwa na wazazi au walezi wao kuwakana na kuwalinda wahusika baada ya kuelewana na kusababisha washtakiwa kuachiwa huru kwa kukosa ushahidi.

Anasema uwepo wa nyumba salama au maeneo ya kuhifadhi waathirika au wajawazito ili wasirudi nyumbani kuchangamana na jamii wakiwamo washtakiwa kutapunguza kuharibu ushahidi na wahusika kufungwa jela.

"Waathirika wa mimba za utotoni wakibaki kuishi kwenye nyumba salama wakati kesi inaendelea, hakutakuwa na wakuwarubuni kubadili maelezo ya awali ambayo wameyatoa dhidi ya washtakiwa waliowampatia ujauzito,"anasema Lydia.

"Tatizo hili linachangiwa na washtakiwa kutokufungwa jela, lakini tukiwafunga wengi wataogopa kuwarubuni wanafunzi na watoto kwa kuhofia kuishi gerezani hivyo kufanikisha kumaliza shida hiyo," anaongeza.

Lydia anasema kutokana na kukua kwa tatizo, wanachokifanya sasa ni kuwahifadhi wasichana hao kwenye makazi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

"Mkoa wa Shinyanga tuna nyumba hizo sita kwa ajili ya kuhifadhi watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu, na tuna watoto 114 ambao wanaishi maeneo hayo wakiwamo waliopewa ujauzito tukiwatunza kuhifadhi na kulinda ushahidi," anafafanua Ofisa Ustawi wa Jamii.



Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Shinyanga, Asha Mwetindwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

Anaeleza kuwa japo nyumba hizo si rasmi kuhifadhi waathirika wa mimba na ndoa za utotoni, kwani wanapaswa kuwa na sehemu yao maalum ya kuishi, hadi kesi zitakapotolewa hukumu na wanahitaji matunzo ya kipekee.

Mratibu wa mpango mkakati wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) mkoani Shinyanga Tedson Ngwale, anasema katika mikakati yao ya miaka mitano ya kutokomeza tatizo la mimba na ndoa za utotoni ni pamoja na kuwa na nyumba hiyo salama.

Anasema tatizo linalowakwamisha hadi sasa ni ukosefu wa fedha na kuwaomba wadau wajitokeze kuunga mkono serikali katika mapambano hayo na kujenga nyumba hiyo salama, ambayo itakuwa ni msaada wa kuwanasa wanaowapatia mimba wanafunzi.

"Serikalini tumeshaandika maandiko ya kuomba ufadhili wa ujenzi wa nyumba salama ya kuhifadhi wenye mimba na ndoa za utotoni, lakini tunaomba na wadau watushike mkono hili tatizo ni letu sote na bila ushahidi huwezi kumtia hatiani mshtakiwa,"anasema Ngwale.

Ngwale ambaye ni Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Shinyanga, anawaomba wasimamizi wa sheria mahakamani kuwa licha ya ushahidi kukosekana, wasiwe wanafunga kesi bali wasubiri mwanafunzi ajifungue mtoto na baada hapo wahusika waliotajwa wapimwe vinasaba (DNA) ili kujiridhisha kama si au ni wahusika.

"Kitu kingine ambacho kinapaswa kutiliwa mkazo ni wale watu ambao wamekuwa wakidhamini watuhumiwa wa mimba na ndoa za utotoni na wahusika wanapokimbia wao hutozwa faini na kuachwa, ambapo wanapaswa kuwekwa ndani hadi mhusika apatikane sababu imekuwa kama mchezo na kuchochea vitendo hivi kuendelea," anaeleza Ngwale.

Anasema licha ya ujenzi wa nyumba hiyo salama, mkakati mwingine wa serikali ni kutunga sheria ndogo ambayo itakuwa ikitumika kuanzia ngazi za chini kudhibiti wanaume kuwa karibu na wanafunzi hasa katika mazingira ya hatari na kupigwa faini.

Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga Dafroza Ndalichako, anaelezea takwimu za wanafunzi ambao mwaka 2022 wamepewa ujauzito na kuacha masomo kuwa ni 147, shule za msingi ni 28 na wakati sekondari walikuwa 119.

Anafafanua kuwa kati ya wanafunzi 28 wa shule za msingi ambao walipewa ujauzito, kesi zilizoko mahakamani ni mbili na 26 bado upelelezi haujakamilika, huku wenye mimba 119 wa shule za sekondari kesi 21 ndizo zilizopelekwa mahakamani, tatu zilitolewa hukumu, 22 zinaendelea kusikiliza na 38 upelelezi haujakamilika.

Mkuu wa Dawati la Jinsia wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Monica Sahere, anasisitiza pia kuwa ukosefu wa hifadhi salama kwa waathirika ambao ndiyo mabinti mashahidi umekwamisha vita hivyo.

Anasema mtoto akirudi nyumbani siku anapokuja kutoa ushahidi anaeleza vitu vingine tofauti na alivyotolea maelezo ya awali.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Shinyanga Asha Mwetindwa, anataja takwimu za mashauri ya kesi za ukatili yaliyofunguliwa kuanzia mwaka 2020 hadi 2022 zikiwamo kesi za mimba za utotoni kuwa ni mashauri 295.

Amesema kati ya kesi hizo 295, mashauri 182 yameshatolewa maamuzi na 103 yameondolewa kortini baada ya kushindwa kusikilizwa kutokana na ukosefu wa ushahidi huku kesi nyingine 10 zikiwa bado mahakamani.

"Mikakati ambayo mahakama ni kwamba siku inafunguliwa kesi na siku hiyo hiyo tunaanza kuisikiliza, na ushahidi utakaotolewa ndiyo tutautumia kuendeshea kesi hadi hukumu," anasema Hakimu Mwetindwa.

"Tatizo ambalo tumelibaini ni kwamba kesi inafunguliwa na siku ya kusikilizwa inapangwa, hapo ndipo hutumika mwanya wa kumalizana wazazi na walezi wa pande zote mbili na kumrubuni binti yao kumkana mshtakiwa na mwisho wa siku kesi inakosa ushahidi na kufutwa," anaongeza Hakimu Mwetindwa.

Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga, Donasian Kessy, anasema suala la upotevu wa ushahidi ni mianya ya rushwa, lakini hakuna taarifa ambayo inatolewa sababu pande zote mbili hulifanya kwa kuelewana.

Anasema ushauri ambao anautoa juu ya kesi hizo za mimba na ndoa za utotoni, kwamba siku ukamataji umefanyika na mwanafunzi kutoa ushahidi kwa kumtaja mhusika, kuwa siku hiyo hiyo ushahidi huo uchukuliwe na kuendelea kuendesha kesi hadi hukumu.

Mkurugenzi wa Shirika la Agape la kutetea haki za watoto mkoani Shinyanga, John Myola, anasema watuhumiwa wa mimba za utotoni wanapokosa kufungwa jela, hurudi uraiani na kuanza kutamba, huku familia hizo mbili zikiendelea na mikakati ya kulipana mahari.

Mwathirika wa mimba za utotoni mkazi wa Usanda, (jina tunalo) anasema alipopata ujauzito na kesi ilipofunguliwa na aliporudi nyumbani wazazi walimtaka amkane mhusika kwasababu akifungwa jela hakuna wa kumlea mtoto wake.

"Mzazi akikushawishi umkane mtuhumiwa inabidi ukubali, sababu mimi ni mwanafunzi na sina kazi na nimeshapoteza mwelekeao, sina kipato nani atamlea mtoto? Inabidi nikubali kumlinda mtuhumiwa,"anasema.

# SIMBA QUEENS KUOKOA JAHAZI LA MATAJI MSIMBAZI

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA Watetezi wa Ligi Kuu ya Soka Wanawake, Simba Queens, leo watashuka Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kucheza dhidi ya Baobab Queens, ikiwa ni mechi muhimu ya kujaribu kutetea ubingwa wake ambao uko rehani dhidi ya JKT Queens.

Timu hiyo inaweza kuwa ndiyo mkombozi wa wanachama na mashabiki wa klabu hiyo ambao wametangaza rasmi kumaliza msimu wa 2022/23 bila taji lolote kwa upande wa wanaume.

Hata hivyo, bado Simba Queens inategemea zaidi kupoteza kwa JKT Queens au sare kwenye mechi mbili zilizobaki dhidi ya Fountain Gate Princess na Mkwawa Queens.

Mashabiki wa Simba Queens wanaitegemea zaidi Fountain Gate kuizuia JKT Queens katika mechi kali itakayochezwa kesho kwenye uwanja huo huo wa Jamhuri, lakini hayo yote yatategemea kama itashinda mechi yake ya leo ikiwa ugenini.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema maandalizi yamekamilika, lakini akikiri ubingwa wa safari hii wa ligi ya wanawake utaamuliwa kwenye mechi ya mwisho.

"Nilisema tangu mwanzo kuwa msimu huu bingwa atapatikana kwenye mechi ya mwisho, timu zote zimekamilika, na zilijiandaa vizuri hasa hizi timu tatu za Simba Queens, Fountain Gate Princess na JKT Queens ziko sawasawa na hata pointi zao hazijapishana sana na ni lazima mechi ya mwisho ndiyo itaamua bingwa.

"Niwaambie tu watu kuwa yeyote atakayekuwa bingwa msimu huu, akienda kucheza michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) pia anaweza kuwa bingwa huko, kwa sababu ametoka kwenye ligi ngumu sana," alisema kocha huyo raia wa Uganda.

Baada ya mechi ya leo, Simba Queens itabakisha mechi moja tu dhidi ya Ceasiaa Mei 17, mwaka huu.

Mpaka sasa JKT Queens ina pointi 40 ikiongoza ligi, Simba Queens 39 nafasi ya pili na Fountain Gate 38 ikiwa nafasi ya tatu.

**CHUMA HICHO...**



Kiungo wa Simba, Sadio Kanoute, akiifungia timu yake bao la kusawazisha kwa kichwa dhidi ya Azam FC kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA, iliyopigwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara juzi na kumalizika kwa Azam kushinda mabao 2-1. **MPIGAPICHA WETU**

# Hitimana atajwa na nafasi Malale JKT

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kurejesha timu Ligi Kuu Tanzania Bara kuelekea msimu mpya wa 2023/24, uongozi wa Klabu ya JKT Tanzania upo katika mchakato wa kumpa ajira, aliyekuwa Kocha Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, kukinoa kikosi hicho kwa msimu ujao, imefahamika.

Licha ya uongozi wa JKT Tanzania kutoweka wazi suala hilo huku wakidai kuwa wataendelea na Kocha Hamsini Malale aliyeipandisha timu hiyo Ligi Kuu endapo anahitaji kuendelea kubaki katika timu hiyo, lakini taarifa za ndani zilizolifikia gazeti hili klabu hiyo ipo katika mazungumzo na Hitimana.

Hata hivyo, Malale alipoulizwa juu ya mustakbali wake juu ya maboresho ya kikosi chake, alisema hawezi kuweka mipango yake ya usajili ya msimu ujao kwa sababu hajui hatima yake.

Taarifa zilizolifikia Nipashe jana, kutoka chanzo chetu ndani ya uongozi wa timu hiyo, zimeeleza tayari wameanza kukaa vikao kumjadili Hitimana kuwa sehemu ya benchi lao la ufundi kukinoa kikosi cha timu hiyo.

Ilisema Hitimana ameanza kujadiliwa na kuna mazungumzo ya siri ambayo yanaendelea kati ya viongozi wa timu hiyo pamoja na kocha huyo kuwa sehemu ya benchi la ufundi kukinoa kikosi cha timu hiyo.

Nipashe lilipomtafuta Hitimana kuhusu kujua ukweli wa taarifa hizo, aliweka wazi kwamba hakuna timu iliyomfuata hadi sasa na yupo hapa nchini kwa ajili kukamilisha mambo yake ikiwamo kumalizana na viongozi wa KMC FC ili kurejea kwao.

"Hakuna kiongozi aliyenifuata kwa ajili ya mazungumzo yoyote, hilo suala kama lipo, kwangu ni vizuri kwa sababu hakuna mtu anayekataa kazi anapoipata," alisema Hitimana.

## Kali atoa siri Dube kuitungua Simba SC

**Na Hadija Mngwai**

KAIMU Mkuu wa Azam FC, Kali Ongalla, ametoa siri ya mshambuliaji wao, Prince Dube, kuwatungua Simba mara kwa mara, akisema ni kutokana na kujua mbinu za mabeki wa timu hiyo.

Azam juzi ilifanikiwa kutinga fainali ya Kombe la Azam Sports Federation, maarufu Kombe la FA baada ya Dube kuifungia bao la ushindi dakika ya 75 akitokea benchi huku akiwa mwiba mkali kwa mabeki wa Simba katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara.

Akizungumza na Nipashe jana, Kali alisema kuwa, siri ya Dube kuwatungua Simba ni kutokana na kuwa na njaa ya kufunga magoli huku akitambua mbinu za mabeki wa Simba kwa kuwafuata nyuma kila mara.

"Prince anakuwa na njaa ya magoli, staili yake ya kucheza na aina ya mpira wanaocheza Simba inakuwa nzuri kwake, anapenda kukimbia nyuma ya mabeki wa Simba ambao hawapendi mshambuliaji kukimbia nyuma yao, hivyo ndio maana anawasumbua na kufanya vizuri.

"Ni aina ya mchezaji ambaye huwa hapendi kushindwa ukimpa maelekezo anakwenda kuyafanyia kazi," alisema Kali.

Aidha, akizungumzia mchezo huo aliongeza: "Tumepambana na kufanya vizuri, mechi ya kwanza na Simba na hii zina utofauti mkubwa, hivyo tumeangalia kitu gani kinaweza kutusaidia tushinde na tumekifanyia kazi na tumepata matokeo mazuri, hakuna mazingaombwe, watu wamejituma na kujitoa".

Azam FC ni mara yake ya kwanza kuiondoa Simba katika michuano ya Kombe la FA, kwani mara tatu walizokutana kabla ya juzi, zote Wekundu wa Msimbazi hao waliibuka na ushindi.

Kwa matokeo hayo Azam FC sasa inasubiri mshindi kati ya Yanga na Singida Big Stars katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa Liti mkoani Singida Mei 21, mwaka huu, ili kujua timu watakayokutana nayo fainali kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GUNDOGAN NA BARCA
KLABU ya Barcelona ina uhakika wa kukamilisha dili la kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan, 32. ***(90min)***

### VILLA WAMTAKA VLAHOVIC
ASTON Villa inajiandaa kumnunua fowadi wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 23 kutoka Juventus. ***(Football Insider)***

### SPURS YATAKA BEI YA KSSIE
KLABU ya Tottenham Hotspur imeitaka Barcelona kutaja bei yao kwa kiungo wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie, 26. ***(Sport)***

### ALLISTER NA LIVERPOOL
KLABU ya Liverpool haijawasiliana na Brighton kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Alliste, 24. ***(Athletic)***

### OSIMHEN AGOMEWA NAPOLI
RAIS wa Napoli, Aurelio de Laurentiis, amesema mabingwa hao wa Serie A hawatamuuza mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, mwenye miaka 24, ambaye amekuwa akihusishwa na baadhi ya klabu kubwa barani Ulaya, msimu huu wa majira ya joto. (***Cinque Minuti, via Mail***)

### AUBAMEYANG KUREJEA BARCA
NAHODHA wa zamani wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, mwenye miaka 33, ataondoka Chelsea - na anataka kurejea Barcelona. ***(Fabrizio Romano)***

### PALHINHA ATAKIWA VILLA
ASTON Villa ipo tayari kulipa dau la pauni milioni 60 kwa Fulham ili kumsajili kiungo wa kati wa Ureno, Joao Palhinha, mwenye miaka 27 kutoka klabu hiyo ya London. ***(Football Insider)***

### CANCELO KUTUA BARCA
WAKALA wa mchezaji wa Kimataifa wa Ureno, Joao Cancelo, mwenye umri wa miaka 28, amekutana na Barcelona kuhusu klabu hiyo kumsajili beki huyo wa Manchester City, ambaye yuko kwa mkopo Bayern Munich. ***(Sport)***

### RYAN AWANIWA CITY
KLABU ya Manchester City itaangalia uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Bayern Munich, Mholanzi Ryan Gravenberch, mwenye miaka 20, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool, iwapo watashindwa kumnunua kiungo wa kati wa Uingereza, Jude Bellingham, mwenye miaka 19, kutoka Borussia Dortmund. ***(Mirror)***

### HAZARD YUPO SANA REAL
MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Eden Hazard anatarajia kumaliza mwaka wa mwisho wa mkataba wake katika Klabu ya Real Madrid, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, kutokuwa na namba katika kikosi cha kwanza. ***(Cadena Cope, via Marca)***

### AOUAR SAFI ROMA
AS Roma imekubaliana mkataba mpya na kiungo wa kati wa Ufaransa, Houssem Aouar, ambao utamfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ajiunge na klabu hiyo ya Italia msimu wa majira ya joto wakati mkataba wake na Lyon utakapokamilika. ***(Sky Sports Italia)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL ITAPAMBANA HADI MWISHO - ARTETA

Kitu pekee tunachoweza kufanya ni kuendelea kusisitiza na tusigeuze migongo yetu na...

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, ametoa changamoto kwa wachezaji wake "kuendelea kupambania" taji la Ligi ya England baada ya ushindi dhidi ya Newcastle, Jumapili.

Arteta, ambaye alionesha sehemu za video za kikosi chake cha kichapo cha mabao 2-0 katika Uwanja wa St James Park msimu uliopita kutoka filamu ya Amazon All or Nothing, asubuhi ya mchezo huo, anaamini kuwa bado wana nafasi ya kuchuana na vinara Manchester City.

Akizungumza baada ya ushindi wa mabao 2-0 Jumapili, alisema: "Tupo, sasa tunataka kuendelea kupambana. Zawadi ipo, si mbali sana.

"Kitu pekee tunachoweza kufanya ni kuendelea kusisitiza na tusigeuze migongo yetu na kupoteza mwelekeo wa kitu kingine, kudhamiria kila siku. Tuendelee na tuone kitakachotokea."

'Washikabunduki' hao walipata pointi zao kupitia kwa Martin Odegaard aliyefunga kipindi cha kwanza na Fabian Schar bao la kujifunga baada ya mapumziko.

Alipoulizwa ikiwa uchezaji wao umethibitisha kwamba watapigana hadi mwisho, Arteta alijibu: "Inathibitisha kwamba tumefanya hivyo leo. Sasa lazima tuthibitishe kuwa tunaweza kuifanya dhidi ya Brighton.

"Tumeifanya kwa miezi nane na nusu na lazima tuendelee kuifanya. Tupo na sasa tunajisikia tofauti sana na siku 10 zilizopita na inabidi sasa tuhakikishe kwamba kasi iko pale pale."

"Tumefanya kile tulichohitaji kushinda mchezo na nimeufurahia sana."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 575,

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 2.92
X | 3.31
2 | 2.25

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG AMTETEA DE GEA



**LONDON, England**

ERIK ten Hag amemtetea golikipa, David De Gea licha ya uzembe wake kusababisha Manchester United kupoteza dhidi ya West Ham United juzi.

Kipa De Gea yuko kwenye mazungumzo kuhusu mkataba mpya pale Old Trafford, lakini aliruhusu kombora la Said Benrahma kutoka umbali wa yadi 20 liruke juu ya glovu zake na kuiwezesha West Ham kuibuka na ushindi wa 1-0.

Sasa wako pointi moja pekee mbele ya Liverpool inayosonga mbele kwa kasi, ingawa wana mechi moja mkononi, baada ya kushindwa kwa mara ya nane wakiwa ugenini msimu huu na mara ya pili ndani ya siku nne kufuatia kupoteza katika dakika za mwisho kutoka kwa Brighton.

"Inafadhaisha? Ndio, nimeiona kwa njia ile ile. Nadhani tulianza vizuri, tulipanga mchezo, tukatengeneza nafasi, hatukuchukua na kisha tukatengeneza kosa moja," alisema Ten Hag.

"Makosa mara mbili ya mtu binafsi na unapoteza michezo. Lakini ndivyo ilivyo. Sasa tuna wiki nzima, tunapaswa kujipanga upya na kuendelea.

"(De Gea) ndiye ambaye hajafungwa mabao zaidi kwenye Ligi Kuu, tusingekuwa katika nafasi hii bila yeye. Hakuna wasiwasi.

"Tunataka abaki na kuongeza mkataba wake."

"Hakuna kilichobadilika. Tungeweza kuifanya iwe rahisi kwa ushindi. Tunahitaji ushindi kila kitu kiko mikononi mwetu."

# Kane ataka taji la Europa

**LONDON, England**

HARRY Kane amesisitiza Tottenham Hotspur inapaswa kuona Ligi ya Europa kama nafasi ya kumaliza ukame wa mataji ikiwa itashiriki katika mashindano hayo msimu ujao.

Spurs wana nafasi ya kucheza mashindano ya Ulaya baada ya ushindi wa bao 1-0 Jumamosi dhidi ya Crystal Palace ambapo bao la kichwa la kipindi cha kwanza la Kane liliisaidia kupanda hadi nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Brighton, walio katika nafasi ya saba, bado wanapewa nafasi kubwa ya kufuzu Ligi ya Europa ikizingatiwa wana mechi tatu mkononi na wamepitwa pointi mbili na Tottenham.

Nahodha huyo wa England amesema: "Tumebakisha mechi tatu, mchezo mkubwa ni dhidi ya Villa wiki ijayo ugenini.

"Ni wazi kwamba Brighton wana mechi chache mkononi kwetu. Ikiwa tunaweza kuondoka msimu huu na soka la Ulaya, hiyo ni tuzo muhimu kwetu.

"Tutapigania hilo na kupigana katika mechi tatu kujaribu kupata ushindi mara tatu.

"Mwisho napenda kucheza michezo ya mpira wa miguu bila kujali ni mashindano gani. Hicho ndicho unachostahili kutoka pale unapomaliza msimu.

"Huwezi kudharau mashindano yoyote ambayo unacheza. Ni mojawapo ya hayo, ikiwa utaishia kwenye Ligi ya Europa Conference ni sawa.

"Lakini unapokuwa katika klabu ambayo hatujashinda kombe kwa miaka 15, ikiwa tutaishia humo, inaweza kuwa fursa nzuri."

Bao la 209 la Kane kwenye Ligi Kuu England lilimaliza mechi ngumu na Palace baada ya Tottenham kusawazisha kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu tangu Februari 26.



# 472,890

## JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 10/05/23 | 22:00 | AC Milan vs Inter | 2.96 | 3.01 | 2.39 |
| 02. 11/05/23 | 01:00 | Coquimbo vs Univ de Chile | 2.58 | 3.32 | 2.43 |
| 03. 11/05/23 | 02:00 | Rangers vs San Luis Quillota | 2.64 | 3.00 | 2.58 |
| 04. 11/05/23 | 02:00 | FC Cincinnati vs New York City | 2.24 | 3.47 | 2.74 |
| 05. 11/05/23 | 03:30 | Cruzeiro vs Fluminense | 2.83 | 3.22 | 2.29 |
| 06. 11/05/23 | 05:30 | LA Galaxy vs Seattle Sounders | 2.44 | 3.21 | 2.64 |
| 07. 11/05/23 | 16:00 | Pontedera vs AC Siena | 2.37 | 2.78 | 3.04 |
| 08. 11/05/23 | 19:00 | Sonderjyske vs Vejle BK | 2.72 | 3.39 | 2.23 |
| 09. 12/05/23 | 01:00 | Coritiba vs Vasco da Gama | 2.40 | 3.17 | 2.72 |
| 10. 12/05/23 | 01:00 | Botafogo RJ vs Corinthians | 2.14 | 3.21 | 3.12 |
| 11. 12/05/23 | 01:00 | Univ de Concepcion vs Antofagasta | 2.85 | 2.96 | 2.43 |
| 12. 12/05/23 | 13:30 | FC Tokyo vs Kawasaki Frontale | 2.83 | 3.19 | 2.26 |
| 13. 12/05/23 | 19:00 | Slaven Belupo vs Lokomotiva Zagreb | 2.51 | 3.09 | 2.57 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 09/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1024 | Daegu vs Pohang Steelers | 2.98 | 3.18 | 2.18 |
| 13:30 | 5700 | FC Seoul vs Gwangju | 2.17 | 3.08 | 3.08 |
| 14:35 | 2812 | Shenzhen vs Shanghai Shenhua | 4.94 | 3.86 | 1.54 |
| 14:35 | 2875 | Henan Jianye vs Wuhan Three Towns FC | 5.77 | 4.12 | 1.44 |
| 14:35 | 2969 | Dalian Aerbing vs Shijiazhuang | 2.08 | 3.18 | 3.18 |
| 15:00 | 1080 | Cardiff City U21 vs Crewe U23 | 1.55 | 4.24 | 4.55 |
| 15:00 | 1851 | Singapore W vs Laos | 2.80 | 3.45 | 2.04 |
| 15:00 | 2764 | Watford U21 vs Burnley U23 | 2.06 | 4.09 | 2.70 |
| 15:00 | 3205 | Cambodia vs Thailand W | 26.90 | 7.03 | 1.09 |
| 15:00 | 4423 | Bahir Dar Kenema FC vs Ethiopia Bunna SC | 1.65 | 3.79 | 4.36 |
| 15:00 | 5210 | Bristol City U23 vs Coventry U23 | 1.51 | 4.56 | 4.56 |
| 15:30 | 2934 | QPR U23 vs Wigan U23 | 2.05 | 3.63 | 2.96 |
| 16:00 | 3677 | Charlton U23 vs Hull City U23 | 2.32 | 3.99 | 2.39 |
| 17:00 | 3445 | Mladost Lucani vs Radnik Surduluca | 2.38 | 3.03 | 2.77 |
| 17:00 | 3652 | Bkma Yerevan vs Lernayin Artsakh | 1.71 | 3.32 | 4.67 |
| 17:00 | 3663 | FK Tukums 2000/Tss vs Rigas Futbola Skola | 16.60 | 6.43 | 1.13 |
| 18:00 | 1305 | Honka vs Haka | 1.74 | 3.44 | 4.11 |
| 18:00 | 2563 | USM Khenchela vs JS Kabylie | 2.30 | 2.75 | 3.32 |
| 18:00 | 2925 | FC Slovan Rosice vs Slovacko B | 1.73 | 3.55 | 3.55 |
| 18:00 | 3422 | Jelgava vs FS Metta/Lu | 2.56 | 3.26 | 2.49 |
| 18:00 | 4179 | Ethiopia Electricity vs Dire Dawa Kenema FC | 2.69 | 3.00 | 2.53 |
| 18:00 | 4205 | AC Oulu vs KuPS Kuopio | 3.55 | 3.24 | 1.92 |
| 18:00 | 4375 | FC KTP vs HJK Helsinki | 5.34 | 3.85 | 1.51 |
| 19:00 | 1440 | Dila Gori vs Saburtalo Tbilisi | 1.81 | 3.36 | 3.99 |
| 19:00 | 1559 | Pyramids vs Ismaily SC | 1.73 | 3.31 | 4.92 |
| 19:00 | 3914 | SK Hranice vs Blansko | 2.29 | 3.27 | 2.80 |
| 19:00 | 4235 | Sitra Club vs Al Shabbab | 1.95 | 3.01 | 3.94 |
| 19:00 | 4399 | Al Taawon vs Al Raed Club | 1.71 | 3.84 | 4.48 |
| 19:00 | 4930 | AL Faiha vs Al Fateh (KSA) | 2.72 | 3.51 | 2.40 |
| 19:00 | 5232 | Akritas Chlorakas vs AEL Limassol | 2.59 | 3.37 | 2.52 |
| 19:00 | 5365 | Puerto Montt vs Santiago Morning | 2.22 | 3.00 | 3.15 |
| 19:15 | 1592 | AL Qaisoma vs Jeddah Club | 1.88 | 3.08 | 3.95 |
| 19:15 | 2546 | FK Napredak vs Radnicki Nis | 2.82 | 2.87 | 2.45 |
| 19:45 | 5589 | Viktoria Griesheim vs Bayern Alzenau | 2.95 | 3.50 | 1.93 |
| 20:00 | 1344 | IFK Varnamo vs Varbergs Bois | 1.78 | 3.30 | 4.07 |
| 20:00 | 2909 | Hammarby vs Mjallby | 1.61 | 3.54 | 4.83 |
| 20:00 | 3942 | MC Alger vs CR Belouizdad | 2.59 | 2.70 | 2.91 |
| 20:00 | 5172 | Landskrona Bois vs Helsingborg | 2.40 | 3.35 | 2.82 |
| 20:45 | 3881 | Al Ahli Jeddah vs AL Arabi (SA) | 1.35 | 4.10 | 6.60 |
| 21:00 | 4839 | Colchester U21 vs Peterborough U21 | 2.32 | 3.85 | 2.22 |
| 21:30 | 1528 | Centro Espanol vs Juventud Unida SM | 2.48 | 2.90 | 2.85 |
| 21:30 | 2378 | Deportivo Muniz vs Sportivo Barracas | 3.36 | 3.10 | 2.09 |
| 21:45 | 2734 | Annan Athletic vs Dumbarton | 2.19 | 3.38 | 2.91 |
| 21:45 | 3910 | Alloa Athletic vs Hamilton | 2.88 | 3.24 | 2.28 |
| 21:45 | 4199 | Airdrieonians vs Falkirk FC | 2.40 | 2.87 | 3.03 |
| 21:45 | 5651 | Partick Thisle vs Queens Park | 1.86 | 3.36 | 3.99 |
| 22:00 | 2865 | Real Madrid vs Manchester City | 2.92 | 3.31 | 2.25 |
| 22:00 | 5277 | East Fife vs Clyde | 2.76 | 3.38 | 2.29 |
| 22:30 | 5892 | Magallanes vs Curico Unido | 1.87 | 3.37 | 3.73 |
| 23:30 | 3355 | Molinos EL Pirata FC vs Juan Aurich | 2.23 | 3.24 | 2.83 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MAYELE AWAITA MASHABIKI KWA MKAPA 'WAKATETEME'

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Fiston Mayele, amewataka mashabiki wa timu hiyo kujaa kwa wingi kwenye mchezo wao wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants na kuahidi 'kutetema' kwenye mchezo huo.

Mayele, amesema anataka kuwa sehemu ya historia ya klabu hiyo wakati huu wakishiriki kwenye hatua hiyo ya mashindano ya CAF kwa kufunga magoli na kuiwezesha timu hiyo kutinga hatua ya fainali kwa mara ya kwanza.

"Itakuwa furaha kubwa kuona Yanga wakicheza fainali na mimi nikiwa sehemu ya historia ya klabu hii, naamini tutafanya vizuri kwenye mchezo wetu wa wiki hii pale kwa Mkapa, mashabiki waje kwa wingi, uwapo wao utatuzidishia hamasa na nitajitahidi kufunga ili tuteteme wote," alisema Mayele.

Aidha, alisema anafahamu hautakuwa mchezo mwepesi na wapinzani wao watakuwa wamechukua muda kuwasoma kama ambavyo wao, Yanga wanafanya.

"Hatua hii ni ya matokeo zaidi, ushindi pekee ndio utatuvusha kwenda mbele, wachezaji tunalitambua hili, tumejipanga na tunaendelea kujiandaa kuhakikisha tunafanya vizuri hapa nyumbani kabla ya kwenda kurudiana nao kwao," alisema Mayele.

Mayele alisema kwake litakuwa jambo la kuumiza moyo kama watashindwa kupata ushindi kwenye mchezo huo wa kesho utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Mashabiki siku zote ni mchezaji wa 12, kama wachezaji tunaomba waje kwa wingi kutupa sapoti na sisi hatutawaangusha, tunataka kucheza fainali ya michuano hii," aliongezea Mayele.

Mayele kesho anategemewa kuongoza safu ya ushambulizi ya Yanga kwenye mchezo huo wa mkondo wa kwanza nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini, utakaochezwa majira ya saa 10:00 jioni kabla ya kurudiana wiki moja baadaye nchini Afrika Kusini.

# Yanga yaitumia Mamelodi...

INATOKA UK. 24

ruhusu kufungwa au sare ili watakapokwenda Afrika Kusini kwenye mchezo wa marudiano, wasicheze kwa presha kubwa ya kutafuta matokeo jambo linaloweza kuwasababishia kutolewa mashindanoni.

Aidha, alisema wapo tayari kwa mchezo huo na kazi kubwa wameifanya kwenye mazoezi na sasa ni zamu ya wachezaji wao kuifanya kazi yao na kuwafurahisha mashabiki wao na kuweka heshima ya klabu hiyo juu.

Kuelekea mechi hiyo, Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, amewataka mashabiki wao kuonesha nidhamu ya hali ya juu katika mchezo huo na kutotumia miale ya moto (fataki) katika ushangiliaji. Hiyo ni baada ya Yanga kutozwa faini kwa makosa mbalimbali yanayodaiwa kufanywa katika mechi yao ya robo fainali dhidi ya Rivers United ya Nigeria, iliyochezwa Aprili 30, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ambapo Rivers walitoa malalamiko yao siku moja kabla ya mechi hiyo baada ya kumaliza mazoezi yao uwanjani hapo.

Rivers United walilalamika gari yao kuvunjwa vioo na kuibiwa dola 5000 huku wakidai pia kupuliziwa dawa, hivyo Kamati ya Maadili ya Caf, iliyokutana Mei 4, mwaka huu, ikaipiga faini Yanga kiasi cha dola 10,000 za Marekani kwa kosa la kuwasha vitochi na kupiga mafataki uwanjani na dola 25,000 kwa madai ya kupuliza dawa kwenye gari la timu ya wapinzani wao huku wakitakiwa kulipa faini hizo ndani ya siku 60 tangu kutolewa kwa adhabu hiyo, lakini pia imetoa nafasi kwa klabu hiyo kukata rufani ndani ya siku tatu.

Kamwe alisema barua hiyo imewafikia na kwamba imeainisha makosa hayo na jana viongozi walitarajiwa kukutana kupitia baada ya hapo watatoa taarifa rasmi.

"Ni kweli barua hiyo kutoka Caf tumeipokea, niwaombe mashabiki wanapokuja uwanjani katika mechi yetu ya Jumatano dhidi ya Marumo Gallants, wasitumie zile fataki ili kulinda klabu yetu maana tayari tumetozwa faini kwa sababu ya mechi iliyopita," alisema Kamwe.




# Robertinho awaangukia mashabiki Simba

INATOKA UK. 24

lilikuwa kufika angalau nusu fainali, kwenye michuano ya FA tuliishia nusu fainali sawa na msimu huu, tulipoteza ubingwa wa Ligi Kuu na msimu huu dalili ni hizo hizo, ukiangalia hapo na kulinganisha utaona hakuna hatua tuliyopiga," alisema Ahmed.

Kutokana na hayo alisema uongozi wa klabu hiyo utakaa na kuangalia aina ya wachezaji walionao na kuona wapi wanatakiwa kuboresha ili msimu ujao wavuke walipoishia misimu miwili mfululizo.

"Lazima tuwe na wachezaji ambao wanauwezo wa kututoa hapa tulipo kufika mbele zaidi, uongozi na benchi la ufundi utakaa na kuliangalia hili kwa kina, tutarudi kwa kishindo kikubwa msimu ujao," alisema Ahmed.

Msimu huu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba waliondolewa hatua ya robo fainali na Wydad Casablanca ya Morocco huku kwenye ligi ikiwa imezidiwa kwa pointi saba na wapinzani wao, Yanga walioukaribia ubingwa huku ikiwa imebaki michezo mitatu kabla ya ligi kumalizika. Yanga wanahitaji ushindi kwenye mchezo mmoja tu kati ya hiyo kutwaa ubingwa.

Michezo
Jumanne Mei 9, 2023
Nipashe



UKURASA 21

## Arsenal itapambana hadi mwisho - Arteta

# YANGA YAITUMIA MAMELODI KUNASA MBINU ZA MARUMO

### ●●● Nabi atoa tahadhari, Mayele awaita kwa Mkapa kutetema, mashabiki waonywa...

**Saada Akida na Faustine Feliciane**

WAKATI uongozi wa Yanga ukikutana jana kujadili faini ya jumla ya Dola 35,000 za Marekani, ambazo ni zaidi ya Sh. milioni 82 za Tanzania, walizotozwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi, amesema tayari amepata mbinu za kuivaa Marumo Gallants FC katika mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kesho.

Yanga kwa sasa ipo kambini ikiendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo wa nusu fainali mkondo wa kwanza dhidi ya Marumo Gallants FC ya Afrika Kusini, utakaopigwa kesho katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam majira ya saa 10:00 alasiri, ambapo wapinzani wao hao wakitarajiwa kutua nchini leo alfajiri.

Akizungumza na Nipashe jana, Nabi alisema wanaendelea kufanyia kazi madhaifu na ubora wa wapinzani wao kulingana na walivyowaona juzi wakicheza mchezo wa Ligi Kuu ya Afrika Kusini dhidi ya Mamelodi Sundowns.

Alisema wameona ubora wa safu yao ya ushambuliaji na ulinzi, na kwamba licha ya wapinzani wao hao kupoteza kwa mabao 2-0 katika mechi yao ya nyumbani ya ligi, wamekuwa na matokeo mazuri katika michuano ya kimataifa.

"Tunaingia katika huu mchezo kwa nidhamu kubwa, tunaenda kucheza na timu nzuri na haitabiriki kwenye michezo yao, na tunatakiwa kucheza kwa tahadhali kubwa kulinda wapinzani wetu wasipate nafasi ya kuwafunga na kuyatumia madhaifu yao ya safu ya ulinzi kumaliza mechi nyumbani kabla ya kwenda Afrika Kusini.

"Tumewafuatilia mechi waliyocheza juzi ya ligi nchini kwao na kufungwa mabao 2-0, hii haitatufanya kuwaona wapinzani wetu ni wabovu kwa sababu wamefanikiwa kufika katika hatua hii ya nusu fainali si timu ya kubezwa," alisema Nabi.

Aliongeza kuwa malengo yao ni kumaliza mechi hiyo nyumbani, kwa kuto-

INAENDELEA UK. 23



Mayele

## Robertinho awaangukia mashabiki

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kutupwa nje kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho nchini, maarufu FA Cup, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, amewaomba radhi wanachama na mashabiki wa klabu hiyo na kusema hawakuwa na 'bahati' kwenye mchezo wao dhidi ya Azam FC.

Simba juzi ilijikuta ikitupwa nje ya michuano hiyo kwa kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Azam kwenye mchezo wa nusu fainali uliopigwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho, alisema kwenye mchezo huo walikosa bahati kutokana na nafasi nyingi walizozipoteza kabla ya bao la kipindi cha pili la mtokea benchi, Prince Dube, kufuta matumaini yao ya angalau kutoka na taji moja msimu huu.

"Haya mambo yanatokea kwenye mpira, matokeo yameumiza Wanasimba wote, pamoja na kucheza vizuri hatukuwa na bahati, tulitengeneza nafasi nyingi lakini hatukuzitumia vizuri..., kwenye mchezo kama huu unaohitaji matokeo unapaswa kutumia vema kila nafasi unayoipata, niwaombe radhi mashabiki wa timu yetu kwa matokeo haya ambayo hatukuyategemea," alisema Robertinho.

Alisema kama kiongozi wa benchi la ufundi atakutana na uongozi wa klabu hiyo kuangalia nini cha kufanya kuhakikisha msimu ujao wanarudi kwa kasi kubwa.

Wakati Robertinho akisema hayo, uongozi wa Klabu ya Simba kupitia kwa Meneja habari wake, Ahmed Ally umekiri kuwa hakuna hatua waliyopiga msimu huu kutokana na kuondolewa kwenye mashindano yote huku wakiwa hawana uhakika wa ubingwa wa Ligi Kuu.

Ahmed, alisema kuwa hakuna walichoongeza kulinganisha na msimu uliopita ambapo kwenye michuano yote waliishia hatua waliyoishia msimu huu.

"Msimu uliopita kwenye mashindano ya CAF tuliishia hatua ya robo fainali kama ilivyo msimu huu,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >